SUPA JACKPOT
TZS. 1,059,844,733
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 3

**ABIRIA** wasimulia magumu ya usafiri


Ukurasa 14

MATESO TABIANCHI
TGNP yabainisha ubaya, namna yanavyochochea ukatili kijinsia

Ukurasa 15

MABALOZI KIDUCHU
Rais Samia anakumbushwa afanye kitu, uchache wanadiplomasia wanawake

Ukurasa 19

siasa
JUMATANO DESEMBA 21, 2022
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU

MLUNGULA KOMBE LA DUNIA ULIVYOBOMOA BUNGE ULAYA

NYOTA YA BIBI TITI HIYO
**UWT yatamani kiwepo kigoda kumuenzi, hakuwa msomi, ila amefanya maajabu**

Na Sabato Kasika

BIBI TITI Mohamed ni mwanamama shupavu anayeenziwa na wengi Tanzania Bara na Visiwani na katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini kwa kushiriki kwa hali na mali kwenye harakati za ukombozi na kufanikisha kupatikana uhuru.

Kwa mchango wake huo, Bibi Titi anapata heshima kubwa miongoni mwa Watanzania kwa mchango wake mkubwa katika maendeleo ya nchi, kulinda uhuru, amani na haki za wanawake nchini na hata bara zima la Afrika.

Ni baada ya miaka 22 ya kifo chake, akifarika Novemba mwaka 2000, wiki iliyopita linafanyika kongamano la kumuenzi, linaloandika historia wilayani Ikwiriri Rufiji mkoani Pwani, kuibua na kujadili mchango wa mwanasiasa huyo mahiri kwa taifa.

Likiandaliwa na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT), Mary Chatanda anatoa ahadi za kumuenzi.

Anasema UWT itafuata nyayo zakekwa kuondokana na mawazo ya kusubiri kuwezeshwa, badala yake kujiamini na kuonyesha uwezo walionao ili wafike mbali bila msukumo mkubwa kutoka nje.

Anasema Bibi Titi alikuwa ni jasiri, anayejiamini na mwenye kuonyesha uwezo wake na kwamba wana UWT hawana budi kufuata nyayo hizo, ili kusaidia nchi kusonga mbele kimaendeleo.

"Katika miaka ya 1950, alikuwa miongoni mwa wale waliopigania uhuru wa Tanganyika kutoka kwa Muingereza akiwa na Baba wa Taifa Mwalimu Juliu Nyerere, Waziri Mkuu Rashid Kawawa na viongozi wengine wa TANU," anakumbusha Mary.

Mary Chatanda Mwenyekiti wa UWT Taifa; akizungumza kwenye Kongamano la Bibi Titi Mohamed. **PICHA: CCM**

Anaongeza:"Bibi Titi alikuwa mwanamke wa kwanza kujiunga na harakati mbalimbali za kupigania uhuru wa Tanganyika, na kwamba mwanzoni mwa harakati zake za kisiasa alishawishi wanawake kujiunga pamoja naye kudai uhuru."

"Kama kiongozi wa tawi la wanawake wa TANU, alikuwa na jukumu la kushawishi wanawake kuunga mkono sera na maoni ya chama, nasi hatuna budi kufanya hayo ili kushawishi wengine kujiunga na CCM," anasema Mary.

**KUANZISHIWA KIGODA**

Mwenyekiti wa UWT anasema ipo haja ya kuanzisha taasisi ambayo itajihusisha na Bibi Titi kama ilivyo Kigoda cha Mwalimu Nyerere, lakini pia kuwa na siku maalum la kuadhimisha siku ya mwanasiasa huyo.

"Ikiwezekana, kiandikwe kitabu cha kumwelezea kiongozi huyo shupavu, mwanaharakati na mpigania uhuru wa Tanganyika na ninaipongeza wizara kwa kuandaa kongamano na tamasha hili," anasema.

Kufanyika kwa kongamano hilo, ni ishara kwamba wizara hiyo ina mchango mkubwa, katika historia ya kuwaenzi wapigania uhuru na kuendeleza masuala ya maendeleo, hasa ya wanawake.

"UWT inaamini katika kaulimbiu ya kongamano hili ya mwanamke ni jeshi imara katika kuleta mabadiliko, tumuenzi. Huo ndio ukweli, kwani chini ya Rais Samia Suluhu Hassan tumeona mambo makubwa anayofanya," anasema.

Anamtaja kuwa tangu nchi kupata uhuru, na Rais Samia ndiye anapaswa kuitwa Bibi Titi wa leo.

"Tunaweza kumwita Bibi Titi wa leo, kwa sababu katika uongozi wake wa miaka miwili tumeona namna ambavyo ameleta mageuzi ya kihistoria katika kuendesha nchi," anasema.

Anasema serikali yake imejenga miundombinu ya huduma za afya, elimu ikiwamo vyuo vya VETA na shule ya wasichana ya Mkoa wa Pwani iliyopewa jina la Bibi Titi Mohamed.

"Mambo yote hayo na mengine yanaonyesha kweli kwamba Rais Samia ni Bibi Titi wa sasa anaeyaishi maono ya waasisi wa taifa hili na kuwa jasiri katika

INAENDELEA UK. 20

# Nipashe

Jumatano Desemba 21, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581166

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

UKURASA 13





# Samia avunja ukimya mikopo

**AFUNGUKA** fedha zinakokwenda, asema kukopa ni lazima...

*Endelea Uk. 2*

## Mwanafunzi afa kwa radi akimfungua mbuzi kwenye mti

UKURASA 3

## Adaiwa kumuua mke na kumfukia shimo la choo



Jeneza lililobeba mabaki ya mwili wa marehemu Jeniviva Athanas likiwa kanisani kwa ajili ya ibada ya mazishi. **PICHA: NEEMA HUSSEIN**

UKURASA 2




**MICHEZO** FRED VUNJABEI AMKANA JOKETI UK. 27 **KATUNI** UK. 6



Wanakikundi wa kundi sogezi la WhatsApp la Mada Moto Faraja, wakiweka shada la maua kwenye kaburi la aliyekuwa Balozi wa Tanzania nchini Austria, Celestine Mushy, aliyefariki dunia kwenye ajali ya gari eneo la Mkata, Handeni, wakati akielekea Moshi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Rais Samia avunja ukimya mikopo

**Na Christina Mwakangale**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amevunja ukimya kuhusu mikopo ambayo serikali inapokea kutoka kwa mataifa na mashirika mbalimbali huku akibainisha kuwa fedha hizo zinatumika katika miradi ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa reli ya kisasa (SGR).

Licha ya kuanika hayo, Rais Samia amesema baadhi ya watu wamekuwa wakidai kuwa serikali ya awamu hii imekopa zaidi bila kujua fedha hizo zinavyotumika na kusisitiza kwamba mikopo hiyo haiepukiki kwa kuwa ndiyo iliyokamilisha ujenzi wa SGR na mingine mikubwa iliyoachwa katika awamu iliyopita.

Rais Samia aliyasema hayo jana, wakati wa akishuhudia utiaji saini wa mkataba wa SGR kipande cha Tabora – Kigoma jijini Dar es Salaam huku akiweka bayana kuwa miradi kama hiyo ni vigumu kukamilika kwa kutumia fedha za ndani.

"Miradi hii tusingeweza kufanya ilibidi tukope kwa awamu hii. Tunakopa ili tujenge leo kwa maendeleo endelevu na baadaye. Kwa hiyo kila tunapohisi pana faida tutaendelea kukopa. Waseme sana awamu hii imekopa sana, waseme pia ndiyo awamu iliyojenga sana.

"Wanasema awamu hii imekopa sana lakini wamefanya nini hawasemi. Hii ni mikopo lazima tulipe. Kwa walio maeneo tofauti ya kukusanya fedha, tukaze mkanda. Mwezi huu kulikuwa na maeneo fedha hakuna lakini kuna mikopo iliyoiva kwa pamoja na imebidi tulipe," alisema.

Rais alisisitiza kuwa Wizara ya Fedha na Mipango, iweke wazi takwimu za mikopo ziendane na utoaji na kwamba ili kulinda heshima ya nchi na kwamba mikopo yote ni lazima ilipwe ikiwamo ya ujenzi wa miradi hiyo.

"Tawi la kutoka Uvinza kwenda Msongati lazima tujenge. Kuna mtu ameshajitokeza atatumia fedha zake kujenga tutakatana kwenye usafirishaji. Lengo ni kuunganisha Tanzania na Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC)," alisema Rais.

Alisema mradi huo hadi sasa umefikia dola bilioni 10.04 sawa na Sh. trilioni 23.3 na kwamba ujenzi huo utaifungua nchi kwa kuwa reli hiyo itafika maeneo ambako kuna usafirishaji mkubwa wa mizigo.

"Gharama za usafirishaji kwa kontena moja kutoka Dar es Salaam hadi DRC inakadiriwa kuwa kati ya Dola za Kimarekani 6,000 na 15,000 kutegemea unakokwenda ukichukua zaidi ya mwezi mmoja. Reli hii ikikamilika mwaka 2027 gharama zitapungua hadi Dola 4,000 na muda wa usafirishaji kuwa saa 27 hadi 30 kwa treni ya mizigo," alisema.

Rais Samia alisema miradi ya kimkakati itaendelea kufanyika ikiwamo uwekezaji wa reli za zamani kwa kuzifufua na kuzikarabati, hususani kwenye maeneo yaliyo na bandari hasa Mtwara na Tanganyika.

"Lengo la serikali ni kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara na usafiri na iwapo miradi itakamilika kwa wakati, miradi ya kimkakati, hususan huu umeshatoa fursa za ajira za moja kwa moja 20,000 na mishahara kulipwa Dola milioni 102," alisema rais.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Masanja Kadogosa, akitia saini mkataba na kampuni ya ujenzi wa mradi huo awamu ya pili, wenye kilomita 506 kipande cha sita Tabora hadi Kigoma, alisema utakuwa na stesheni 10 za abiria na vituo vikubwa viwili Uvinza na Katosho.

Alisema mradi huo unaifanya Tanzania kuwa yenye reli ndefu ya aina hiyo barani Afrika na kwamba bei za mradi na vifaa vitakavyotumika haitaathiri mabadiliko ya bei na uchumi duniani.

"Nchi ambayo imejenga reli ya SGR ya kilomita 500 haijajenga kwa gharama kama tuliyoitumia Tanzania. Rais tunakushuru kwa kuliamini shirika na kuendeleza mradi huu," alisema.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, alisema Tanzania inaweka rekodi kuwa na mtandao wa reli ya kisasa kama ilivyo utekezaji wa ajenda ya Umoja wa Afrika (AU) katika ujenzi wa reli aina hiyo kwa nchi wanachama.

## Adaiwa kumuua mke wake na kumfukia kwenye shimo la choo

**Na Neema Hussein,** MPANDA

JESHI la Polisi mkoani Katavi linamshikilia Augustino Joseph (31), kwa tuhuma za kumuua mke wake, Jeniviva Athanas (30), kisha kuutupa mwili wake kwenye shimo alilochimba kwa ajili ya ujenzi wa choo.

Akizungumza jana na Nipashe kwa simu baada ya maziko ya mwanamke huyo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi, Ali Makame, alisema tukio hilo lilitokea miezi sita iliyopita na mwili huo ulifukuliwa Jumamosi na kuzikwa baada ya utambuzi wa kisheria kukamilika.

Makame alisema mwanamke huyo aliripotiwa kupotea katika mazingira ya kutatanisha miezi sita iliyopita na familia yake na walipofuatilia ndipo mume alishukiwa na alipohojiwa, alikiri na kuwaonyesha polisi alikozika mwili huo.

"Tulipokwenda kufukua, tulikuta kuna mifupa kwa sababu kipindi ni kirefu palibakia mabaki hayo ya mifupa na tukajiridhisha kuwa ni kweli, hilo tukio limetendeka na si tu kupotea bali aliuawa," alisema Kamanda Makame.

Akizungumza na Nipashe, baba mzazi wa marehemu, mzee Ndikumwami Ndihabwa, alisema walipoteza mawasiliano na ndugu yao miezi sita iliyopita na walipojaribu kumtafuta kwa njia ya simu alikuwa hapatikani.

"Mwanangu niliishi naye vizuri nilimwozesha kwa mtu huku Katavi. Katika miezi sita hatukuwa na mawasiliano naye. Nimekuja kugundua baada ya usaidizi wa polisi mtuhumiwa kutaja kuwa alimuua na kwenda kutuonyesha alipomuulia na baadaye alifukuliwa na kuonyesha viungo vyake," alisema.

Baba huyo alisema baada ya mwili wa marehemu kufukuliwa, nguo zake zote zilichomwa pamoja na simu yake, ili kupoteza ushahidi lakini baada ya kufukua mwili wake, zilikutwa baadhi ya nguo za marehemu walizozitambua.

Kaka wa marehemu, Nicodemus Fidelis, akisoma historia ya maisha ya dada yake, alisema alikuwa mkazi wa Kijiji cha Mkabogo, lakini baada ya kuolewa alihamia katika kijiji cha Kaseganyama, Tanganyika mkoani Katavi alikoishi na mume wake hadi mauti yalipomkuta.

Alisema katika kipindi cha maisha yao ya ndoa, walipata watoto wawili wa kike na wa kiume na kutengana kwa muda kutokana na mke kumtuhumu mume wake kwa ugoni na alihamia kijiji cha Ikola na mwanamke anayedaiwa kuwa ni hawara yake.

"Baada ya muda, yule mwanamke ambaye ni dada yangu wakawa na maisha magumu pale Kaseganyama, ikabidi aombe nauli kwa wazazi wake ili arudi Kigoma na baadaye watoto wakawa wanamsumbua wanamhitaji baba yao, ikabidi mama afanye mawasiliano na mume wake, ili aongee na watoto wake.

"Baada ya mazungumzo ikaonekana mama awalete watoto kwa mume wake, lakini baba mkwe (baba wa marehemu) alimzuia kwamba asiende mpaka mume aje Kigoma ili wasuluhishwe ugomvi wao na miezi sita, mwanamume alikwenda Kigoma kupata suluhu.

"Wakati huo mke wake aliyeshikwa naye ugoni, walihama naye kutoka kijiji cha Kaseganyama kwenda kijiji cha Kanoge Barabara ya Kumi Halmashauri ya Nsimbo mkoani Katavi. Baada ya kutoka Kigoma, mtuhumiwa alirudi na mke wake siku hiyo hiyo, walimpiga na kumuua na kumdumbukiza kwenye shimo la choo ambalo walikuwa wakilitumia kipindi wapo Kanoge," alisema.

Fidelis alisema baada ya ndugu kuona muda mrefu umepita bila kuwa na taarifa za mtoto wao, walifika mkoani Katavi kutoka Kigoma walikokuwa wakifanya jitihada za kumtafuta. Baada ya kufika waliondoka wakiwa na watu wanne kwenda kijiji walichokuwa wakiishi kumtafuta mume wake.

Kwa mujibu wa kaka huyo, baada ya kufika Kanoge, walifanya upelelezi na kufanikiwa kuwapata mume na mke, huku mume alionekana kufichwa ndani na mke wake na baada ya kuhojiwa, mwanamke alikiri mume wake yuko ndani.

Baada ya kubanwa sana na Jeshi la Polisi, alisema "kweli mimi nimemuua tukiwa na mke wangu aliyekimbia tukamfukia ndani. Twendeni nikawaonyeshe".

"Kwa hiyo juzi (Jumamosi iliyopita) tukiwa na askari na wataalamu wa afya na hakimu, tukaenda naye hadi alipofanyia tukio, tukafukua mafuvu yale tukayakusanya, kisha tukarudi naye, tunafanya mazishi ya kuzika hiyo mifupa (juzi jioni)," alisema.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Rungwa, mjini hapa kulikofanyika msiba, Mwelela Nkonkwa, alisema Jeniviva alikuwa na ugomvi wa muda mrefu na mume wake baada ya kumfumania na mwanamke mwingine.

Mwili wa marehemu Jeniviva ulizikwa juzi katika makaburi ya Kazima, Manispaa ya Mpanda ambako Nipashe ilikuwapo ikishuhudia ndugu wa marehemu wakizimia makaburini.

## HABARI KITAIFA

# Abiria wasimulia magumu ya usafiri

**Na Mwandishi Wetu**

ABIRIA wanaosafiri kwenda mikoani hususani mikoa ya Kaskazini wamelalamikia utaratibu unaofanywa na mawakala wa mabasi kwa kukataa kuwakatia tiketi za siku mbili au tatu kabla ya kusafiri na kuwataka wafike siku hiyo hiyo ya safari.

Abiria anayetaka kukata tiketi ya siku mbili au tatu kabla ya safari anatakiwa kuongeza kiasi cha fedha ambacho hakiandikwi kwenye risiti jambo linalosababisha wengi kulanguliwa.

Wamelalamikia abiria kukatiwa kiti kimoja zaidi ya mtu mmoja huku wanaosafirisha watoto wamelalamika watoto wao kuondolewa kwenye siti njiani na kupandishwa watu wazima.

"Nataka kusafiri tarehe 22, nimeambiwa magari yamejaa hadi wiki ijayo, nimesogea pembeni nimeongea na mtu mmoja yeye kakatiwa tiketi anasema dada jiongeze utoe Sh. 10,000 utapewa tiketi ya siku unayotaka, hata kesho hawataki, wanataka uje siku hiyo asubuhi ndipo ukatiwe tiketi kwa bei halali," alisema Neema Kimario akiyekuwa eneo la Shekilango, jijini Dar es Salaam.

Baadhi ya mawakala wamelalamikiwa kutumia kipindi hiki cha sikukuu kujipatia kipato cha ziada kwa kuwatoza abiria nauli zaidi kinyume na bei elekezi ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA).

Mmoja wa abiria aliyekwenda kukata tiketi ya kusafiri Desemba 23, mwaka huu, alisema sio kweli kwamba mabasi yamejaa, kwa sababu alikwenda tarehe 18 kukata tiketi kwa ajili ya kusafiri leo akajibiwa magari yamejaa, lakini alipokwenda jana alikuta watu wanakatiwa tiketi za siku hiyo.

"Tunawaomba LATRA wafanye uchunguzi wao wawe kama abiria wafike waombe kukatiwa tiketi, wakamate wanaolangua itakuwa funzo kuliko hivi tunavyowasikia wanasema hakuna ulanguzi nasi tukifika huku tunalanguliwa na kusumbuliwa, nimekaa kwenye foleni hapa kwenye hizi ofisi za hili basi na sijapata tiketi," alisema.

Theodory Shayo, aliyekwenda kukata tiketi ya safari ya Desemba 23, alisema mawakala hao wanatumia njia hiyo ili wapate pesa za ziada.

"Mimi alinifuata wakala mmoja akanambia nimpe Sh. 10,000 katika kila tiketi, ili aniwekee nafasi katika gari linaloondoka Alhamisi kwa kuwa niliambiwa magari hayo yamejaa, akaniambia hayajajaa wanaepuka usumbufu kutokana na kujaza sana sasa hivi," alisema Theodory.

Michael Msemvu alisema mabasi kuongeza bei za nauli kunawaathiri kiuchumi na kusababisha kutokula sikukuu kama walivyotarajia.

Rhoda Enea alilalamikia baadhi ya mawakala kukatisha tiketi zaidi ya moja kwa siti moja na wengine kuwasimamisha watoto na kuwapa siti hizo watu wazima licha ya kulipiwa nauli kamili.

"Nilisafirisha watoto peke yao kutoka Tanga, kufika Segera mmoja akaambiwa asimame, ile siti kumbe aliandikishwa abiria mwingine, imebidi watoto wapakatane kutoka Segera hadi Dar es Salaam, kwa kweli niliumia sana ukizingatia niliwakatia nauli kama abiria wengine," alisema Rhoda.

Akizungumza na Nipashe Desemba 13, mwaka huu, Meneja Usalama na Mazingira wa LATRA, Geoffrey Silanda, alisema wanaendeleza jitihada za kumaliza adha ya usafiri ikiwamo kutoa leseni za muda kwa mabasi yatakayopeleka abiria mikoani na kwamba zimeshatolewa 42.

Alisema vilevile wanashirikiana na Shirika la Reli Tanzania (TRL), ambalo limekubali kuongeza mabehewa ambayo yatapachikwa kwenye treni za kwenda mikoani ili kuongeza nguvu na kupunguza adha ya usafiri wanayopitia abiria kipindi hicho.

Wiki iliyopita TRL ilisema imeongeza mabehewa 10 kwenda mikoa ya Kaskazini na kufanya jumla kuwa 16, huku kwenda Kigoma yatakuwa 22, lengo ni kuwapunguzia wananchi usumbufu wa usafiri.

Katika eneo la Shekilango na Kituo cha Magufuli, Nipashe ilishuhudia Coaster zikiita abiria, lakini wengi walionekana kutaka kusafiri na mabasi makubwa.

# Mwanafunzi afa kwa kupigwa radi akifungulia mbuzi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MWANAFUNZI wa kidato cha pili katika Shule ya Sekondari Lugalo mkoani Iringa, Calister Haule (15), mkazi wa Kijiji cha Lifua, wilayani Ludewa, Njombe, amefariki dunia kwa kupigwa na radi wakati akifungulia mbuzi chini ya mti.

Mbali na kifo cha mwanafunzi huyo, nyumba 16 zimeezuliwa na upepo mkali ulioambatana na mvua kubwa huku sita zikibomoka kabisa.

Akizungumza na Nipashe, Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya ya Ludewa, Daniel Ngalupela, alisema tukio hilo lilitokea Desemba 17, mwaka huu, majira ya saa 11:00 jioni katika kijiji cha Lifua Kata ya Luilo.

"Madhara makubwa yaliyojitokeza ni kifo huyo binti mwanafunzi wa kidato cha pili amepigwa radi akiwa anafungulia mbuzi waliokuwa wamefungwa kwenye mti mkubwa wa mkorosho. Pia mbuzi alikufa.

"Kitu cha kwanza kama wilaya tumefanya tathmini ya athari zilizojitokeza. Baada ya hapo kukutana na wadau kwa ajili ya kuwachangia ili kuwasaidia kupata vifaa kama mabati, mbao ili kuzirudisha hizo nyumba katika hali ya kawaida," alisema Ngalupela.

Alisema jitihada ya dharura ambayo imechukuliwa ni pamoja na kuwaomba baadhi ya wananchi kuwahifadhi watu ambao wamepata madhara.

Kwa mujibu wa mashuhuda wa tukio hilo akiwamo Allen Ngatunga, tukio hilo lilimkuta binti huyo akiwa amelala chini pamoja na mbuzi hao.

Ngatunga alisema binti huyo alipigwa na radi hiyo na kufa papo hapo sambamba na mbuzi aliokuwa akiwafunga.


SERENGETI BREWERIES

MAOMBI YA MAPENDEKEZO YA USAMBAZAJI VIFAA VYA BIOMASI

Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) inatafuta mapendekezo kwa ajili ya usambazaji vifaa endelevu vya biomasi katika kituo chake mjini Moshi. Vifaa vya biomasi ni vyovyote vyenye uwezo wa kuzalisha nishati isiyo na taka za kisukuku (non-fossil fuel waste).

**Kampuni zitakazo vutiwa zinapaswa kutoa taarifa zifuatazo hapo chini:**

1. Jina la Muuzaji
2. Uthibitisho wa wasambazaji wa usajili wa kampuni na umiliki wa kampuni
3. Maelezo ya mawasiliano ya wasambazaji ikiwa ni pamoja na namba ya simu
4. Cheti cha TIN na cheti cha ukubalifu kodi
5. Nyaraka zinazoidhinisha kampuni kusambaza vifaa vya biomasi.
6. Aina ya vifaa vya biomasi ulivyonavyo
7. Wingi wa biomasi inayoweza kupatikana kwa mwezi (katika kilo)
8. Eneo la chanzo cha nyenzo za biomasi
9. Umbali wa chanzo cha nyenzo za biomasi kwa SBL- Moshi

Mapendekezo yanapaswa kutumwa kabla ya **11 Januari, 2023** saa **1200** (Afrika Mashariki) kupitia barua pepe SBLBiomass@diageo.com.

Nakala ngumu hazikubaliwi.
Mawasiliano yatafanyika kwa kampuni zitakazo pitishwa tu.
Makundi maalum na makampuni yanayomilikiwa na wanawake yanahimizwa kuomba.

Johnnie Walker Keep Walking · SMIRNOFF · Bongo DON Spirit · Captain Morgan · GUINNESS MADE OF MORE · Pilsner Lager · CÎROC · Serengeti Lite · Serengeti · GORDON'S SHALL WE?

17202101

# Miili ya walioangukiwa na ghorofa yatambuliwa

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

WAKATI kazi ya uokoaji wa watu waliofukiwa na vifusi kwenye jengo la ghorofa mbili lililoporomoka katika Kijiji cha Sembeti, Kata ya Marangu Mashariki, Wilaya ya Moshi ikiendelea, baadhi ya miili ya waliofariki dunia imetambuliwa.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi (ACP), Simon Maigwa, miili iliyotambuliwa mpaka sasa ni mitatu kati ya mitano. Aliwataja waliotambuliwa kuwa ni Erasmus Mchau, Godfrey Peter na Richard Kamili. Majeruhi waliotambuliwa ni Tumaini Frank, Cheusi fundi, Ezekiel Shayo, Haji Hamisi, Mark Lyimo na Yahaya Issa.

Jengo hilo lilianguka usiku wa Desemba 18, mwaka huu, wakati ujenzi ukiendelea na kuua watu watano, kati ya wafanyakazi 30 waliokuwa katika ghorofa hilo linalojengwa na mfanyabiashara mmoja wa Dar es Salaam.

Juzi, Kamanda Maigwa alinukuliwa akisema umma utataarifiwa kuhusu chanzo cha tukio hilo baada ya uchunguzi kukamilika, kwa kuwa mmiliki wa jengo hilo hayupo na inasemekana ni mkandarasi yuko jijini Dar es Salaam.

"Mmiliki naye tunamhitaji tuendelee kumhoji, kwa sababu sisi pia tumefungua jalada la uchunguzi, ambalo tunaendelea nalo. Tumeandika maelezo ya vibarua mbalimbali ambao walikuwa wanafanya kazi pale ili tuweze kujua nani ni foremen (msimamizi wa ujenzi).

"Je ni nani aliyekuwa anahusika na ujenzi, je taratibu zilifuatwa? Kujua chanzo ni baada ya ile tume iliyoundwa, ambayo itahusisha wataalamu ambao watatoa majibu yaliyo sahihi," alisema Kamanda Maigwa.

Kwa mujibu wa ACP Maigwa, ripoti ya uchunguzi huo itakapokamilika na kuonyesha watu hao walipelekwa kujenga jengo hilo, bila ya kufanya maandalizi mazuri, sheria itachukua mkondo wake, baada ya kuonekana uzembe uko upande gani.

Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000, inaelekeza kuwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa (Halmashauri), ina jukumu la kutoa kibali cha ujenzi ndani ya siku 30 kwa mwombaji aliyekubaliwa.

Kutokana na ajali hiyo, serikali imetangaza kuunda timu maalum ya wataalamu wa kada mbalimbali, kuchunguza chanzo cha kuanguka kwa jengo hilo na kusababisha vifo hivyo vya watu watano.

Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Abbas Kayanda, ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Moshi akitoa taarifa ya awali kuhusu tukio hilo alisema: "Kama serikali, tutaunda timu ya kuchunguza sababu kubwa iliyosababisha jengo hilo kuanguka na kusababisha hao wenzetu watano kupoteza maisha.

"Kwenye hilo jengo kulikuwa na wafanyakazi 30 ambao ni vibarua na mafundi ujenzi, ambapo wafanyakazi 16 kati yao ndio wamesalimika."


**Stakeholders consultation meeting for the Carbon Voluntary Project Activity "Protect the environment, use clean cookstoves!" under the "Green Tanzania Cookstoves Programme"**

OffgridSun in collaboration with Inuka Youth Development Organization develops a clean cooking project in Tanga Region called "Tunza Mazingira, tumia jiko banifu! – Protect the environment, use clean cookstoves!". The project is an activity (VPA) under the Gold Standard Programme of Activities (PoA) "Green Tanzania Cookstove Programme" implemented by OffgridSun with the goal is to improve livelihoods of local population and protect environment in Tanzania by distributing improved cookstoves across the country to reduce CO2 emission derived by the use of biomass fuel for domestic purposes. The programme is developed under the Gold Standard framework and seeks to obtain Verified Emissions Reductions (VER).

The project Tunza Mazingira, tumia jiko banifu is implemented in ten villages in Mazingara, Mkata and Kwachaga Wards within Handeni District, Tanga Region, for a total of about 10.000 households targeted.

OffgridSun is welcoming stakeholders to provide their feedback through the organization of a stakeholders' consultation meeting to gather suggestions. The meeting will be held in Mkata, Handeni District at Ukumbi Wa Halmashauri (VETA) on the **20th of January 2023** from **8.00 am to 13.00 pm time local time.**

Interested people are invited to participate by contacting the number below. Those who wish to send their feedback or to ask more information about the project, can contact OffgridSun by writing a mail to **projects@offgridsun.com** or calling the numbers **+255682701460 or +393516142230 (whatsapp).**

*217203002*




Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Dk. Athuman Ngenya (kushoto), akimkabidhi Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya GF Vehicle Assemblers Limited, Imran Karmali, Tuzo ya Ubora wa Kitaifa wa Kampuni Bora ya Mwaka 2022\2023 kwa kampuni kubwa katika hafla ya kukabidhi tuzo hizo jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Meneja Mkuu wa GF Vehicle Assemblers, Ezra Mereng. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kikwete, Dk. Tax waongoza mamia maziko Balozi Mushy

**Na Mary Mosha,** MOSHI

RAIS Mstaafu wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Stergomena Tax, jana waliongoza mamia ya waombolezaji kutoka ndani na nje ya nchi katika mazishi ya aliyekuwa Balozi wa Tanzania nchini Australia, Celestine Mushy.

Maziko ya mwanadiplomasia huyo, aliyefariki dunia katika ajali ya gari eneo la Mkata, Handeni mkoa wa Tanga, Desemba 12, mwaka huu, baada ya gari alilokuwa akisafiria kugongana uso kwa uso na lori la mizigo na kuteketea kwa moto, yalifanyika katika eneo la Sambarai, Moshi mkoani Kilimanjaro.

Balozi Mushy alipata ajali hiyo majira ya saa 4:00 usiku akiendesha gari aina ya Toyota Crown lenye namba za usajili T175 DMF kutoka Dar es Salamu kwenda Moshi kwa ajili ya sikukuu za mwisho wa mwaka.

Balozi Mushy ambaye ameacha watoto wawili na mke, aliteuliwa na Rais Samia Suluhu kuwa Balozi wa Tanzania nchini Austria Januari, 2022 na Mei 5, 2022 akawasilisha hati za utambulisho kwa Rais wa Jamhuri ya Austria, Alexander Van der Bellen.

Katika maziko hayo yaliyosheheni viongozi wa kitaifa, mabalozi nchi mbalimbali, viongozi wa kisiasa, kijamii, wananchi na viongozi wa kijamii, yaliongozwa na Paroko wa Parokia ya Bikira Maria Mtolewa Hekaluni Karanga, Padre Serafine Kilawe.

Padri Kilawe alisema Balozi Mushy alikuwa mwema kutokana na kulelewa katika malezi ya kiroho na wazazi wake pamoja na kanisa.

Alisema ni wajibu wa wazazi na walezi, vijana kuwekewa misingi imara ya malezi kwa watoto badala ya kuwasukumia katika shule za kulala katika kujiletea pamoja na mitandao ya kijamii.

"Leo (jana) tunasikia taifa linasikitika kumpoteza Balozi Mushy kutokana na uwajibikaji wake. Ameweza kuwa mtiifu, mwadilifu na mzalendo kwa nchi yake, tuwalee watoto wetu katika malezi hayo ili kupata kizazi kinachojitambua, kisichokuwa na mazoea ya kuchukua kitu cha mtu," alisema.

Akitoa salamu za serikali, Dk. Tax alisema kuondoka kwa Balozi Mushy kumeacha pengo huku akiwakumbusha watumishi wa umma kufanya zaidi ya pale wanapotakiwa kufanya.

"Hakuna mtu mwenye jitihada ambazo hazitazaa matunda. Tunaona manufaa ya Balozi Mushy na yameweka alama isiyosahaulika kutokana na jitihada na uzalendo wake kazini. Alikuwa mchapakazi, mshirikishaji na aliyependa kueleweza mara kwa mara bila kuchoka wala kukata tamaa," alisema.

Rais mstaafu Kikwete alisema Balozi Mushy atakumbukwa kwa uzalendo, uchapakazi na ucha Mungu na kuongeza kuwa hakuna sababu ya watu kujiuliza maswali mengi na balada yake kuiiga yale yaliyomema kutoka kwake.

"Nilikuwa porini lakini nashukuru leo (jana) nimepata nafasi ya kumsindikiza mwenzetu Balozi Mushy. Kila mmoja ana sababu ya kifo chake, hivyo tujikite katika kumwombea dua njema," alisema.

Akitoa salamu za Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika mazishi hayo, Katibu wa Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, alisema chama kitamkumbuka Balozi Mushy kama nyenzo kuu ya mchango wa maendeleo katika taifa.

"Chama Cha Mapinduzi kimepokea kwa majonzi na masikitiko makubwa hasa kutoana na mchango mkubwa wa Balozi Mushy katika kuimarisha na kuelimisha ushirikiano wa kimataifa. Chama kinathamini mchango alioutoa. Watumishi wengine waliobakia tumesikia Balozi Mushy akizungumziwa wema na mazuri hasa alama aliyoiacha katika maeneo aliyofanya kazi. Ni matumaini yetu mwenzetu ametangulia lakini funzo kwetu kubwa ambalo tumepata ni kwamba tupande na tuweke alama na mbegu ya wema," alisema.

"Wema huo ni matumaini yetu kwamba watumishi waliobakia wa serikali lakini wa siasa tutaishi katika nyayo ambazo Balozi Mushy alipigania," alisema.

Balozi Mushy alikuwa mwanadiplomasia mahiri katika taifa na alikuwa mtoto wa tano kwa mama yake na kwenye familia ya Joseph Mushi aliyekuwa mkulima na kiongozi wa mtaa kwa wakati huo, alibatizwa na kukulia mazingira ya Kisambarae, wazee na wakazi wengi wa Sambarae alijulikana kama Sele.

Alianza safari yake ya elimu mwaka 1976 alipojiunga na Shule ya Msingi Karanga Manispaa ya Moshi. Mwaka 1984 alijiunga na Uru Seminari kwa masomo ya sekondari hadi alipohitimu kidato cha nne mwaka 1987 na baadaye Arusha kuendelea kidato cha tano na sita na kuhitimu mwaka 1990.

Mwaka huo huo hadi mwaka 1991, Mushy alijiunga na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Kambi ya Oljoro kwa mujibu wa sheria, mwaka 1992 alijiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) akisomea Shahada ya Kwanza ya Sayansi na Uchumi na kutunukiwa mwaka 1996.

Kati ya mwaka 1999 na 2000 alijiunga na Chuo cha Diplomasia, Kurasini, Dar es Salaam na kuhitimu Stashahada ya Diplomasia na Uhusiano wa Kimataifa, mwaka 1999 hadi 2002 alipoteuliwa kuwa mtetezi wa Tanzania kwenye masuala ya uchumi na fedha kwenye ofisi ya uwakilishi wa kudumu Tanzania kwenye ofisi za Umoja wa Mataifa, New York, Marekani.

Mwaka 2006, alirudi nyumbani kuwa Naibu Katibu wa aliyekuwa Waziri Mkuu, Edward Lowassa, nafasi aliyoitumikia pia chini ya Waziri Mkuu, Mizengo Pinda, kati ya mwaka 2008 na 2012 na baadaye kuteuliwa kuwa Balozi na Mkurugenzi katika Wizaya ya mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mwaka 2018 hadi 2021 aliteuliwa kuwa Katibu Tawala Msaidizi kwenye masuala ya uchumi na uzalishaji ya mkoa wa Mtwara. Desemba 2021 aliteuliwa kuwa Balozi wa Tanzania nchini Australia na mwakilishi wa kudumu wa Tanzania wa Ofisi za Umoja wa Mataifa, Viena.

## TANGAZO




**Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan**

**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

**Zoezi la kuanza ujazaji wa maji kwenye Bwawa la Julius Nyerere**

# 22/12/2022

**BWAWA LANGU | BWAWA LAKO | BWAWA LETU**

Tutakuwa Mubashara TBC1 UHAI TV ITV TANZANIA millardayo Clouds MAELEZO TV

www.tanesco.co.tz

#TupoKazini

17201202

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Viongozi wanaohusishwa uharibifu mazingira wanalihujumu taifa

**JUZI** wakati akifungua kongomano la wahariri na wadau wa uhifadhi wa mazingira, lililofanyika mjini Iringa, Makamu wa Rais, Dk. Phillip Mpango, aliambiwa kuwa hali ni mbaya katika vyanzo vya hifadhi za maji na mazingira kwa baadhi ya wawekezaji wakubwa kujenga katika Mto Ruaha na kuziba na haijulikani waliowapatia kibali cha ujenzi huo.

Imedaiwa baadhi ya viongozi kuhujumu hifadhi za mazingira na vyanzo vya maji kwa maslahi binafsi.

Akiwasilisha taarifa ya hali ilivyo katika vyanzo vya hifadhi ya maji na mazingira kwenye kongamano hilo, Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi, Mkuu wa Hifadhi ya Taifa Ruaha, Godwell Ole Meing'ataki, alitaja hali kuwa mbaya na baadhi wanaofanya uharibifu huo wanapokamatwa, wako tayari kutoa fedha nyingi kwa wakati mmoja kwa ajili ya faini na kuendeleza vitendo hivyo bila kujali athari itakayotokea kutokana na uharibifu huo.

Licha ya kupata fedha nyingi zitokanazo na faini wanazolipa waharibifu hao, lakini wako tayari kulipa fedha kwa mara moja na kurudia kosa kwa kuendelea kuyaharibu mazingira.

Waharibifu hao wanadaiwa kuingiza mifugo kwenye hifadhi kwa ajili ya malisho na mmoja wao alipokamatwa alitozwa faini ya Sh. milioni 80, lakini alizilipa ndani ya muda mfupi tena siku hiyo hiyo.

Meing'ataki alitahadharisha kuwa suluhisho sio faini kwa sababu ni sawa wanakusanya fedha, lakini hifadhi za taifa zinaharibiwa vibaya.

Kwa hakika uharibifu wa mazingira una madhara makubwa ambayo leo hii tunashuhudia dunia inavyokabiliana na mabadiliko ya tabianchi kutokana na uharibifu huo.

Kama hifadhi zimeanza kuvamiwa, maana yake wanyama ambao ndiyo tegemeo la taifa katika vivutio vya utalii watatoweka kwenye hifadhi hizo kwenda kutafuta malisho sehemu nyingine.

Kama viongozi walioaminiwa na serikali katika kulinda na kuhifadhi mazingira wamekuwa chanzo cha uharibifu huo, hao ni wahujumu uchumi na wanapaswa kuwajibishwa.

Makamu wa Rais, Dk. Mpango baada ya kupata taarifa ya kuwapo kwa viongozi wa aina hiyo, ameahidi kuwa serikali itazifanyia kazi taarifa hizo ili watakaohusika waweze kuchukuliwa hatua stahiki.

Pia, Dk. Mpango amewaagiza viongozi wote wa mamlaka za mabonde nchini, kuwabomolea wote waliojenga na kuziba mto Ruaha Mkuu bila kibali kwa gharama zao wenyewe na kuagiza kupatiwa majina ya wote waliopewa vibali vya kujenga katika hifadhi hiyo.

Mwenyekiti wa Kituo cha Wanahabari Watetezi wa Rasilimali na Taarifa (MECIRA), Habibu Mchange, alibainisha kuwa tayari baadhi ya timu ya waandishi wa habari waliotembelea baadhi ya vyanzo vya maji ikiwano Mto Ruaha Mkuu, wamefanya uchunguzi na kubaini namna watu wanavyoharibu vyanzo hivyo katika sekta za kilimo, uvuvi na ukataji miti.

Anasema waandishi hao watashirikiana na serikali kufichua hujuma zote zinazofanywa na baadhi ya watu kwa maslahi yao binafsi kuharibu hifadhi za mazingira na vyanzo vya maji kwa kuwa athari zake zinamgusa kila Mtanzania.

Ni matumaini yetu kuwa ahadi aliyoitoa Makamu wa Rais itatekelezwa ili vitendo hivyo vya uharibifu wa mazingira vikomeshwe nchini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Halfani Chusi

## Muungwana Lazima Nilonge

# Serikali idhibiti kupanda nauli

**KWA** muda mrefu kumekuwapo na tabia ya wamiliki wa mabasi yaendayo mikoani kupandisha nauli hasa msimu huu wa sikukuu za mwisho wa mwaka ikiwamo Noeli kutokana na uwapo wa abiria wengi wanaohitaji kusafiri.

Ni jambo linalotokea kwa miongo kadhaa, na limekuwa kama kitu cha kawaida kwa kila mwaka, lakini upande wa pili wa sarafu mchezo huo unawaumiza wasafiri na kuwavurugia bajeti zao, na umma ukijiuliza hivi tatizo hili halikomeshwi?.

Wenye mabasi wanafanya hivyo wakitambua kuwa kupandisha nauli kiholela ni kosa kisheria, lakini inapofikia wakati kama huu huwa wanapuuza na kuendeleza mchezo ambao ni kinyume na utaratibu.

Kwenye kituo cha usafiri wa mikoani na nje ya nchi, Stendi ya Magufuli, Mbezi Dar es Salaam, nyakati hizi unakutana na kundi kubwa la abiria wanaosubiri usafiri wa kwenda sehemu mbalimbali, ambao kilio chao kikubwa ni kupanda kwa nauli.

Hii ni changamoto kubwa kwenye kuvuruga bajeti kwa mfano nauli ya kwenda mkoani Iringa, imefikia Shilingi 30,000 kutoka 22,000 iliyowekwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Usafiri Ardhini (LATRA) kwa hiyo hapo kimahesabu kuna ongezeko la Shilingi 8,000 ambazo hazikutarajiwa na wanafamilia au msafiri kwenye mipango ya wakati huo.

Mambo hayaishii hapo usafiri wa Arusha unafikia hata Shilingi 50,000 na magari hayafiki kituoni Mbezi yakidaiwa kuwa yapo yanayopiga debe njiani na kuitia abiria na kutoza Shilingi 40,000 au zaidi kutoka Dar hadi Arusha. Ombi langu kwa mamlaka za kushughulikia usafiri kuanzia polisi, LATRA, Chama cha Kuwatetea Abiria kusimamia haki za abiria kwa kushirikiana na serikali ili kuwasaidia wasafiri ambao wanakwenda likizo kusherehekea sikukuu za Krismas na mwaka mpya.

Wamiliki wa magari wanapaswa kutambua kuwa, kusafiri kwa watu wengi msimu wa sikukuu sio sababu ya kupandisha nauli kwa sababu hupanda kwa sababu maalum kama kuongezeka bei ya mafuta, lakini sio wingi wa abiria, kwa sasa hakuna kisingizio chochote kwa sababu hata mafuta hayana mabadiliko kwenye bei.

**Utaratibu wa kuongeza magari ili kumudu wingi wa abiria uende sambamba na kuongeza mabehewa ya treni na hata safari za kwenda na kurudi kwenye mikoa yenye abiria wengi.**

Penginepo ulikuwa ndio muda sahihi wa wamiliki wa vyombo vya usafiri kufurahi kwa kuwa abiria wanapatikana kwa wingi na sio kupandisha bei kutokana na ongezeko la abiria kitu ambacho kinawapatia faida kwa kuumiza wengine.

Mbali na hilo pia serikali iweke utaratibu mwingine wa kuhakikisha kwamba wanaotaka kusafirisha abiria wakati wa sikukuu wanapewa vibali na kuruhusiwa kuanza kazi hiyo mapema zaidi ikibidi hata Novemba ili unapofika mwezi wa 12 kusiwe na kero bali kuipunguza.

Utaratibu wa kuongeza magari ili kumudu wingi wa abiria uende sambamba na kuongeza mabehewa ya treni na hata safari za kwenda na kurudi kwenye mikoa yenye abiria wengi.

Ni vyema pia polisi na LATRA wakawepo kwenye vituo hivyo ili kukomesha wale wenye tabia za kupandisha nauli kwa sababu kunakuwa hakuna sababu ya abiria kukosa usafiri.

Lakini jambo la muhimu ni kuendelea kuwakumbusha madereva kuwa makini wanapo fanya safari zao kwenda kwenye mikoa mbalimbali mara nyingi mwisho wa mwaka ajali zinakuwa nyingi.

Jingine ni umakini kwani wapo watu ambao wao wanasafiri wakiwa na mambo mengine hasa uhalifu ni vyema pia kuacha kula chakula kutoka kwa jirani yako ambaye ana nia ya kukudhuru au kukuibia si vyema kula kuepuka kulishwa dawa za kulevya na kuporwa kila kitu.

Ikumbukwe wahalifu wakishafanya hivyo wanashuka kituo kinachofuata kwa kuwa lengo lao limetimia kwa hiyo ni hatari kwa wakati huu na umakini unahitajika ikibidi dereva na makondakta watoe tahadhari kabla ya kuanza safari na wakati wa kula njiani.

# NAMNA YA KUTAMBUA STEMPU HALALI ZA KODI ZA KIELEKTRONIK (ETS)

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015




Stempu ya kodi ya kielektroniki **(ETS)** ni alama maalum **(label)** inayobandikwa au kuchapishwa katika bidhaa ili kuonesha kuwa bidhaa hiyo imelipa kodi.

Kwa kutumia **App** iitwayo **"Hakiki Stempu"** ambayo inapatikana kwa wenye simu janja (smart phones) aina zote mtumiaji wa bidhaa anaweza kuhakiki.




**HATUA ZA KUFUATA**

**1.** Pakua (download) App yako ya **"HAKIKI STEMPU"** kwa watumiaji wa **Android** kutoka **(Google Play)** na kwa watumiaji wa **iOS** kutoka **(Apple Store)** kwa kuandika neno **"HAKIKI STEMPU"** na kuinstall katika simu yako, kisha ukishakamilisha utaiona App husika katika simu yako.



**2.** Baada ya kuipakua na kuinstall, moja kwa moja fungua App hiyo na kisha ukurasa wa mwanzo (Splash Screen) utatokea ambapo Vigezo na Masharti **(Terms & Conditions)** zitaonekana ambapo utatakiwa kuzikubali **(Accept)** ili kuweza kuendelea mbele zaidi.



**3.** Kisha, App ya **"Hakiki Stempu"** itapenda kupata ruhusa ya kutumia kamera ya simu yako ili iweze kuscan bidhaa husika, hivyo utapaswa kukubali kwa kubonyeza kitufe cha **"OK"** na hapo App itakupeleka katika ukurasa wa **KuScan** bidhaa hiyo, ndipo utaweza kuhakiki alama za usalama kwa kuscan stamp yako iliyobandikwa kwenye bidhaa husika.



**4.** Eneo linalotakiwa kuwa scanned ni eneo **namba 2** kwenye **QR Code** kama inavyoonekana katika picha hapa.




**5.** Mara baada ya kulengesha kibox cha kuscan katika QR Code iliyo kwenye stempu, App itascan yenyewe na kukuuliza iwapo unaona mabadiliko ya rangi katika stempu iwapo ukiiangalia kwenye mwanga, na utabonyeza sehemu ya **"YES"** kama inavyoonekana katika picha.



**6. Hakiki Stempu** itakupatia majibu ya uhalali wa stempu iliyobandikwa katika bidhaa kama ifuatavyo,

**>>** Iwapo Bidhaa ni halali, basi simu yako itaonesha **namba** na **herufi** kama zilivyo kwenye stempu yaani; **jina la bidhaa, aina ya bidhaa, imezalishwa lini, jina la mzalishaji** na **namba ya Barcode.**




217199702

# Kilichojificha machinga wagumu kuondoka masoko ya barabarani

## ● TAKUKURU yajitosa kufuatilia nyendo zao

Na Romana Mallya

**SEHEMU ya kwanza ya ripoti hii jana, ilikuwa na ufafanuzi wa machinga wa Soko la Mwenge wilayani Kinondoni na viongozi wao kuhusu madhila yanayowapata kwa kuendesha biashara kwenye maeneo yasiyo rasmi.**

Pia kulikuwa na ushuhuda wa vikwazo kwa askari wa Jeshi la Akiba (Mgambo) na viongozi wa serikali katika kukabiliana na machinga. Endelea na sehemu ya mwisho kupata undani wa hatua za kitaifa.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Kijitonyama linakopatikana soko hilo, Boniphace Barnabas, anasema wamebaini kuwapo machinga sokoni Mwenge huchangia wenye fremu kupata wateja na ndiyo sababu baadhi ya wafanyabiashara hao wamekuwa wakilisaidia kundi hilo.

Kuhusu meza zilizotengwa kwa ajili ya machinga kubaki wazi kwenye soko jipya la Coca-Cola karibu na Soko la Mwenge, Barnabas anasema: "Tunahangaika nalo, wale ni binadamu, tunavyohangaika na wao wanakuja na akili zaidi, tunaamini kwa kuimarisha ulinzi muda wote itasaidia, huu ndio mpango wetu, tunakusudia tujenge kibanda cha ulinzi eneo lile, tunaomba wadau watusaidie."

Kuhusu madai ya kuwapo viongozi wanaopokea rushwa kutoka kwa machinga, Ofisa Mtendaji huyo anasema wamekubaliana katika kuboresha udhibiti, waweke utaratibu wa kuwa na maofisa ambao watakuwa wakibadilishwa mara kwa mara ili wasizoeane na machinga.

Pia anakiri kukabiliwa na uhaba wa vitendea kazi kama gari na askari polisi, akisisitiza umekuwa ukichangia kuahirishwa operesheni mara kwa mara na ndiyo sababu ya kundi hilo kuendelea kuwapo masoko ya barabarani.

### FAINI ZINAZOTOZWA

Barnabas anasema pindi wanapowakamata, huwatoza faini kati ya Sh. 60,000 na Sh. 10,000 kwa ajili ya kutunza mzigo huku zile za afya na usafi wa mazingira huwa ni kati ya Sh. 50,000 na 300,000 na anayeshindwa kulipa hupelekwa mahakamani.

"Ukimtoza Sh. 50,000 ni kama umemkuna, kule si wanasema kuna biashara, akilipa tu anarudi muda huo huo na kuendelea na biashara, juzi tulikamata gari linauza mananasi eneo la Mwenge, biashara hizo zinatakiwa kufanyika sokoni, alitakiwa kutozwa Sh. 300,000 lakini akalia hapa, akatozwa Sh. 200,000.

"Tulihisi itakuwa ni adhabu kwake na wengine, jioni nimemaliza kazi ninapita pale, ninamkuta kaegesha gari palepale anaendelea na biashara. Na sheria hiyo hiyo unaweza kumtoza faini mtu leo, kesho, keshokutwa," anafafanua.

Anasema mikakati yao pia inajumuisha kukutana na wadau, hasa viongozi wa machinga ili kujua changamoto zinazowakabili, akibainisha kuwa wiki mbili zilizopita walipofanya hivyo, machinga walilalamika ukosefu wa choo kwenye soko jipya la machinga la Coca-Cola, sasa kimejengwa.

Barnabas pia anasema wamekubaliana kuwapo uwezeshaji mdogo kwa walinzi watakaofanya kazi hiyo, hivyo machinga walioko maeneo rasmi ya Coca-Cola wamekubali kuchangia fedha kidogo ili kuwezesha hilo.

### KAULI YA MANISPAA

Mwanasheria wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, Jumanne Mtinangi, katika ufafanuzi wake kwa Nipashe kuhusu suala hilo, anasema:

"Mkakati wa kuwaondoa machinga upo, vikao vinaendelea, jana (Desemba 16 mwaka huu) tumekaa kikao na DC (Mkuu wa Wilaya) wa Kinondoni) ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kuona ni namna gani tunaweza kushirikiana kuhakikisha wanakaa maeneo yanayotengwa.

"Kikao hiki kilishirikisha wasimamizi wa barabara, TANROADS (Wakala wa Barabara Tanzania) na TARURA (Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini) kwa kuwa maeneo mengi biashara zinakofanyika ni kwenye hifadhi za barabara na hawa ndiyo wasimamizi, tumeamua kuunganisha nguvu tulishughulikie kwa pamoja."

Mwanasheria huyo anasema kitendo cha machinga kuondolewa na kurejea kwenye maeneo yasiyoruhusiwa kinatokana na mitazamo yao, wakiamini wakienda maeneo ambayo yametengwa wateja hawatayafikia.

"Ukweli ni kwamba kama watatulia maeneo walikopangiwa, wateja watafika kwa sababu mahitaji yote waliyoyataka yametimizwa, mfano Mwenge (soko jipya la machinga la Coca-Cola) walitaka kituo cha daladala, tumekipeleka, walitaka miundombinu ya maji, kutengenezewa vibanda lakini bado wanarudi barabarani.

"Jambo lingine tunaloliona linasababishwa na imani ya kupoteza wateja wao, hawajakubaliana na mabadiliko, wanaona waliko sasa ndiko wanauza zaidi."

Mwanasheria huyo pia anakiri manispaa hiyo kutowalipa mgambo waliotekeleza opereseheni za kuwaondoa machinga hivi karibuni, akijitetea kuwa dosari hiyo imechangiwa na changamoto katika mfumo wa malipo.

Kuhusu mgambo aliyejeruhiwa akiwa kazini na mwathirika huyo kugharamia mwenyewe, mwanasheria huyo anasema alipata taarifa za kupigwa kwake lakini hana taarifa kuhusu suala la matibabu yake.

"Tunapofanya operesheni tunakuwa na usaidizi wa Jeshi la Polisi. Siku hiyo walifanya operesheni, wakakamatwa baadhi ya machinga, timu ikaondoka eneo la tukio kuwapeleka kituo cha polisi.

"Hawa mgambo waliokuwa wakifanya kazi ile, wakarudi eneo la tukio, huo haukuwa mpangilio wetu wa kazi kwa kuwa pale tayari kulikuwa na taharuki.

"Kwenye operesheni kama hizi ukishasababisha taharuki, unaporudi inabidi urudi kwa tahadhari kubwa, hili ndilo kosa walilolifanya, likatokea lililotokea," anasema.

Kuhusu hoja ya uhaba wa vitendea kazi, mwanasheria huyo anasema moja ya yanayojadiliwa katika vikao vyao ni namna ya kukabiliana na changamoto zilizojitokeza, ikiwamo hiyo ya ukosefu wa vitendea kazi.

"Tumekubaliana namna gani tutakwenda na hizi changamoto na tuone kwanini machinga wanaendelea kurudi? Mambo mengi bado yapo kwenye majadiliano.

"Kwa kuwa tulishawaondoa lakini bado wanarejea na hili si kwa Kinondoni peke yake, ukienda Posta maeneo ya Kisutu utawakuta wale wauzaji wa mboga wamerejea, karibu maeneo yote Dar es Salaam walikoondolewa wamerejea, kwa hiyo kuna kitu cha ziada cha kufanya ili watuelewe," anasema.

### TAKUKURU

Kaimu Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Kinondoni, Ismail Seleman anasema ofisi yao inapokea taarifa vitendo vya rushwa, lakini hawajapata taarifa za viongozi kupokea rushwa kutoka kwa machinga.

"Taarifa kutoka kwa machinga kwamba wanatoa rushwa ili wasihame hatujazipokea, ofisi zetu zipo wazi saa 24, tuna namba 113 na namba ya ofisi ni 0652409165, wanachokifanya inaitwa hongo ambayo inakuwa ni makubaliano ya watu wawili, mtoaji na mpokeaji.

"Ni vigumu sisi moja kwa moja kubaini mpaka mmoja wao akubali kutoa taarifa, kwa hao wanaoshawishiwa, ofisi zetu zipo wazi au wapige simu hizo, tuna magari ya kutosha na rasilimali watu, hata leo wakitupa taarifa tutaichangamkia leo," anasema.

### JESHI LA POLISI

Kamanda wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, anakumbusha jukumu la msingi Jeshi la Polisi ni kulinda usalama wa raia na mali zao, akifafanua kuwa suala la kuondoa machinga au kutowaondoa hawezi kulizungumzia kwa kuwa lina wasemaji wake.

Kuhusu tuhuma za uuzaji bangi kwenye Soko la Coca-Cola, Kamanda Muliro alisema watazifuatilia kulingana na taarifa zilizoko.

Oktoba 30, mwaka jana, ilikuwa siku ya mwisho kwa machinga walioko maeneo yasiyo rasmi kuhama baada ya awali Ofisi ya Mkoa wa Dar es Salaam kutangaza ingekuwa Oktoba 18, mwaka jana na baadaye ikatangaza kuongeza siku 12.

Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Makundi Maalum katika bajeti ya mwaka wa fedha 2022/23 imetenga Sh. bilioni 45 kwa ajili ya machinga ili kuendeleza ujenzi wa miundombinu kwenye masoko na kuwawezesha kupata mitaji na Sh. milioni 107.1 kwa ajili ya kuandaa mwongozo na kuwajengea uwezo viongozi wa machinga.

TANGAZO

MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI YA WILAYA YA MONDULI ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE KUWA, KUNA ZOEZI LA UKUSANYAJI WA MADENI YA VIWANJA NA UHAKIKI WA TAARIFA ZA UMILIKI WA VIWANJA ENEO LA BENETI KITALU 'L', 'M' & 'N' NA MAKUYUNI KITALU 'D','E' 'F' & 'G'.
HIVYO WAHUSIKA/ WAMILIKI WA VIWANJA MAENEO HAYO WANATAKIWA KUFIKA NA NYARAKA ZA UMILIKI IKIWA NI PAMOJA NA RISITI ZA MALIPO YA MANUNUZI YA KIWANJA/VIWANJA.
PIA KILA MMILIKI ANAPASWA KUHAKIKI JINA LAKE KUPITIA MFUMO WA UTUNZAJI MILKI ZA VIWANJA(KANZI DATA) WA HALMASHAURI.
NA WALE AMBAO HAWAJALIPA KABISA/HAWAJAKAMILISHA MALIPO YA VIWANJA WANAPASWA KUKAMILISHA NDANI YA MUDA WA MWEZI MMOJA TANGIA TAREHE YA TANGAZO HILI.

HALMASHAURI HAITAWATAMBUA WANANCHI AMBAO WAMELIPA KIASI, WASIOLIPA KABISA NA AMBAO TAARIFA ZAO HAZIPO KATIKA MFUMO WA HALMASHAURI WA UMILIKI WA VIWANJA(KANZI DATA) BAADA YA MUDA WA TANGAZO HILI KUISHA.

VILEVILE HALMASHAURI ITAUZA NA KUMILIKISHA KWA WANANCHI WENGINE VIWANJA AMBAVYO HAVIJALIPIWA AU VIMELIPIWA KIASI NA VISIVYOENDELEZWA KWA MUDA WA MIEZI 36 TANGIA KUMILIKISHWA NA AMBAVYO HAVIKO KATIKA MFUMO WA UTUNZAJI MILKI YA VIWANJA(KANZI DATA).

HALMASHAURI HAITAREJESHA KIASI CHOCHOTE CHA PESA KWA WANANCHI AMBAO HAWAJAKAMILISHA(WAMELIPA KIASI) MALIPO YA VIWANJA.

LIMETOLEWA LEO TAREHE 13.12.2022.

RAPHAEL J SIUMBU

MKURUGENZI MTENDAJI Halmashauri ya Wilaya ya Monduli

MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI YA WILAYA YA MONDULI.

17202402

# Waziri ataka wafugaji kutunza vyanzo vya maji

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Khamis Hamza Khamis, ametoa rai kwa wafugaji nchini kuzingatia hifadhi ya mazingira kwa kutoharibu vyanzo vya maji.

Alitoa rai hiyo juzi wakati wakati wa Kongamano la Wadau Sekta ya Mifugo lililofanyika jijini Dodoma na kufunguliwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Khamis alisema kwa mujibu wa utafiti wa kimazingira, sehemu kubwa ya uchafuzi wa mazingira inatokana na shughuli za kibinadamu zikiwamo kilimo kisicho endelevu, ufugaji usio endelevu na uchimbaji wa madini usiofuata sheria za mazingira.

Alisema pamoja na kuwa ufugaji ni sekta kubwa inayokuza uchumi na kutangaza nchi, wafugaji wanao wajibu wa kuhakikisha wanafuata sheria za mazingira.

"Niwaombe ndugu zangu wafugaji tuhakikishe hatuchungi wala hatunyweshi maji mifugo yetu kwenye vyanzo vya maji kwani kwa kiufanya hivyo, tutasababisha uharibifu wa mazingira na kuua viumbe waishio humo," alisema.

Pia aliwasisitiza wafugaji na wananchi kwa ujumla kupanda miti na kuitunza ili kusaidia kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi yanayoikumba nchi yetu.

Alisema hali ni mbaya kwa sababu maeneo mengi wananchi wamekata miti ovyo, hivyo kusababisha ukosefu wa mvua na ukame kukithiri katika maeneo mbalimbali ya nchi.

Naibu Waziri Khamis alisema mifugo inahama kutafuta malisho kwa sababu ukame unaosababishwa na ukosefu wa mvua uliochangiwa na ukataji miti.

"Wakati tunapita na Kamati ya Mawaziri tumeona baadhi ya maeneo yamekauka sana kwa sababu za kibinadamu zikiwamo kilimo, ufugaji au uchomaji moto ovyo kwa ajili ya kuni na mkaa, niwashauri ndugu zangu pamoja twendeni tukapande miti na kuitunza," alisisitiza.

# Waziri aonya uombaji holela vibali

**Na Munir Shemweta**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameonya watu wanaoomba vibali vya ujenzi kwa ajili ya ukarabati majengo na badala yake wanafanya ujenzi bila kuzingatia mipango kabambe ya uendelezaji miji katika maeneo husika.

Dk. Mabula alitoa onyo hilo jana Kigamboni, Dar es Salaam wakati wa utoaji hati kwa wananchi wa wilaya hiyo waliorasimishiwa makazi yao, akiwa katika ziara yake ya siku nne mkoani Dar es Salaam.

Akitolea mfano wa Mkoa wa Mwanza na Kigamboni, Dk. Mabula alisema baadhi ya wananchi wameomba vibali kwa ajili ya ukarabati wa majengo na badala yake usiku wanabomoa jengo zima na kujenga usiku na mchana nyumba za kawaida au maduka.

Waziri alisema ambalo ni kinyume cha utaratibu mzima wa mpango kabambe wa uendelezaji miji.

Aliyataja maeneo yenye mchezo huo katika Mkoa wa Mwanza kuwa ni Nyamagana, Pamba na Mabatini. Alisisitiza waliopewa vibali kinyume cha utaratibu wa mipango ya uendelezaji miji, kusimamisha ujenzi mara moja kwa sababu ni lazima wajenge kwa mujibu wa mpango kabambe wa halmashauri husika.

Waziri Mabula aliagiza wakurugenzi na makamishna wa ardhi wasaidizi wa mikoa kuhakikisha wanapita na kukagua kama kuna vibali vipya vilivyotolewa na ujenzi kufanyika kinyume cha mipango kabambe ya uendelezaji miji kusitishwa mara moja.

"Tunahitaji kutengeneza miji yetu. Hatuhitaji kurudi nyuma. Gharama iliyotumika kwenye uandaaji 'master plan' ni kubwa sana. Sasa haiwezekani kujengwa nyumba mpya katika eneo lenye 'mastaer plan', " alisema.

Sambamba na onyo hilo, Dk. Mabula pia ameagiza kampuni nne zilizokuwa zikifanya kazi ya urasimishaji makazi nchini, kutopewa kazi kwenye halmashauri za mkoa wa Dar es Salaam na nje ya mkoa huo mpaka hapo Bodi ya Usajili wa Wataalamu wa Mipango Miji itakapojiridhisha na adhabu iliyotolewa kwa kampuni hizo.

Kwa mujibu wa waziri, kampuni hizo zilikuwa na upungufu mbalimbali uliojitokeza wakati wa utekelezaji miradi ya urasimishaji makazi holela. Alizitaja kampuni hizo kuwa ni Hosea Co.Ltd, Makazi Consult Ltd, Visible Planners na ERECO Development Estate Ltd.

"Tunataka tutoe fundisho maana kazi ya urasimishaji imekuwa na kelele sana na lawama hizo zimeelekezwa au kuishia Wizara ya Ardhi wakati maelekezo ya Rais (Samia Suluhu Hassan) katika kutekeleza urasimishaji ni kushirikisha kampuni binafsi kwa lengo la kuleta ufanisi," alisema Dk. Mabula.

Aidha, Waziri aliwataka wananchi wanaovamia maeneo ya ardhi kuchukuliwa kama wamefanya kosa la jinai na si wavamizi wa kawaida.

Dk. Mabula alisema kumekuwa na tabia inayoonesha kuwa wananchi wanaochukua ardhi za watu kama wavamizi wakati watu hao wanatenda kosa la jinai na kusisitiza kuwa watu hao wanatakiwa kuchukuliwa hatua kama wakosaji wengine wa jinai.

Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Fatma Nyangasa, alimweleza Waziri Mabula kuwa wilaya inaendelea kujipanga katika masuala ya ardhi na kuhakikisha maeneo yanapangwa na kupimwa kwa maelekezo ya mipango miji.

Hata hivyo, alisema wilaya inakabiliwa na vitendo vya uvamizi vinavyofanywa na baadhi ya watu wasio waadilifu na kubainisha kuwa tatizo hilo wanaendelea kupambana nalo.

Kamishna wa Ardhi Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Dar es Salaam, Shukran Kyando, alisema ofisi yake imekuwa ikishirikiana vyema na Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni katika masuala ya ardhi. Alibainisha kuwa kuanzia Julai, mwaka huu, Idara ya Ardhi katika halmashauri hiyo imeandaa hati 4,722.



Mkurugenzi wa Mtandao wa Wafugaji Tanzania-PINGO'S FORUM (wa pili kulia), Edward Porokwa, akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana kuhusu migogoro ya ardhi na ukiukwaji wa haki za binadamu kwenye maeneo mbalimbali hususani kwa wafugaji. Kulia ni Mratibu Jukwaa la Ardhi, Bernard Baha, Mkurugenzi wa Taasisi ya Civic and Legal Aid-CILAO, Odelo Odelo (wa pili kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya HAKI ARDHI, Cathbert Tomitho. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# CCM yawashukuru Watanzania kwa ushindi

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimewashukuru Watanzania kwa kuendelea kukiamini na kukipatia ushindi wa kishindo katika uchaguzi mdogo uliofanyika Desemba 17, mwaka huu.

Uchaguzi huo ulifanyika kujaza nafasi ya ubunge katika Jimbo la Amani, wilaya ya Mjini mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar na udiwani uliofanyika katika kata saba kati ya 12.

Katika uchaguzi mdogo wa ubunge Jimbo la Amani, Msimamizi wa Uchaguzi, Safia Idd Muhammed, alimtangaza mgombea wa CCM, Abdul Yussuf Maalim, kuwa mshindi.

Alisema katika kinyang'anyiro hicho, Maalim alishinda baada ya kupata kura 4, 242 sawa na asilimia 84.1, akifuatiwa na mgombea wa ACT Wazalendo, Mohamed Khamis Mohamed, aliyepata kura 728, sawa na asilimia 14.4.

Licha ya ushindi katika jimbo hilo, CCM iliibuka kidedea katika uchaguzi wa udiwani kata za Majohe (Dar es Salaam), Mwamalili (Shinyanga), Njombe (Njombe), Vibaoni na Mnyanjani (Tanga), Mndubwe (Mtwara) na Dunda (Pwani).

Mbali na kushinda katika kata hizo zilizoshirikisha vyema mbalimbali vya siasa, CCM ilipata ushindi bila kupingwa katika kata tano ambazo ni Dabalo (Dodoma), Ibanda (Mbeya), Misugusugu (Pwani), Kalumbeleza (Rukwa) na Lukozi (Tanga).

Kutokana na ushindi huo, katika taarifa yake iliyotolewa juzi na Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC), Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, CCM imesema siri ya kuibuka kiddedea ni umoja na mshikamano ulioko ndani ya chama.

Shaka pia alisema siri zingine ni uteuzi wa wagombea bora, kampeni za kisasa zilizowafikia wapigakura, uadilifu na uaminifu katika kuwatumikia wananchi hususani katika kukidhi mahitaji na matarajio yao katika kuwaletea maendeleo.

Alisema kazi hiyo inafanywa kwa weledi na ustadi mkubwa na serikali zake zikiongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na Dk. Hussein Ali Mwinyi kupitia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025.

Kushindwa kwa vyama vya upinzani, alisema ni mwendelezo wa ushahidi kwamba havikubaliki na Watanzania wameendelea kuvithibitishia kwamba hawajazoea siasa za vurugu, ulaghai, ubinafsi na migawanyiko ambazo hazina tija katika ustawi wa maisha na maendeleo yao.

"CCM inaahidi kuendelea kuwatumikia Watanzania kwa amani na utulivu kwa kuwa ina uzoefu wa kufanya siasa za kistaarabu na maendeleo kwa ustawi wa Watanzania wote ndiyo maana imeendelea kukubalika kwa wananchi," alisema Shaka katika taarifa hiyo.

# Utafiti: Asilimia 75 magonjwa ya mlipuko yanachangiwa na wanyama

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

UTAFITI uliofanyika ukiwamo wa Shirika la Afya Duniani (WHO), unaonyesha kuwa asilimia 65 hadi 75 ya magonjwa ya mlipuko kwa binadamu yanachangiwa na wanyamapori na wanyama wanaofugwa.

Hayo alibainishwa na Mkurugenzi wa Uzamili, Utafiti, Uhaulishaji wa Teknolojia na Ushauri wa Kitaalamu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Prof. Esron Karimuribo, kwenye kikao cha wataalamu na maofisa viungo wa mradi wa Afya Moja.

Alisema kutokana na ukubwa wa tatizo hilo, Ofisi ya Waziri Mkuu yenye dhamana ya kuratibu maafa yakiwamo magonjwa mbalimbali, imeanzisha jukwaa linaloendana na teknolojia ya sasa ya kidigitali.

Prof. Karimuribo alisema lengo ni kuratibu, kutambua na kushughulikia maafa yote yanayoendana na dhana ya Mradi wa Afya Moja ( One Health Detect - TZ Project).

Alisema dhana ya afya moja inajumuisha watafiti, wataalamu na maofisa viungo kutoka sekta mbalimbali zikiwamo za afya, mifugo, wanyamapori, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na mazingira.

Prof. Karimuribo ambaye ni Mtafiti Kiongozi wa kuratibu mpango kazi ulioko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Idara ya Maafa, alisema wameamua kushirikiana na SUA kuratibu magonjwa yanayoendana na dhana ya Afya Moja.

Alitaja mifano mbalimbali ya matukio yanayofanana ya magonjwa ya milipuko ikiwamo miaka mitatu iliyopita mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19 na homa ya Bonde la Ufa ambayo yanajitokeza kwa njia ya milipuko.

Mtaalamu huyo alisema kuanzishwa kwa mfumo huo ni kukinga, kuwalinda na kupunguza madhara yanayoweza kutokana na milipuko ya magonjwa kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu au kutoka kwa binadamu kwenda kwa wanyama.

Alisema mfumo huo utaleta mafanikio pale jamii husika ambayo imeathirika na tukio lolote la maafa itakapotoa taarifa kwa sekta husika na kuifikia serikali kwa haraka zaidi na hata msaada utatolewa kwa haraka zaidi.

Prof. Karimuribo alisema taarifa zitakapofikishwa wa haraka zaidi serikalini itasaidia kuepusha madhara makubwa yanayoweza kutokea kwa taifa, kupoteza watu (vifo) , vifo vya mifugo na kuathiri uchumi wa taifa.

Naye Mkurugenzi Msaidizi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) Kituo cha Operesheni na Mawasiliano ya Dharura, Prudence Constantine, alisema mradi wa Afya Moja unaangalia namna wataalamu watakavyounganisha nguvu zao kupata suluhisho la matatizo ya magonjwa mengi yanayowakumba binadamu zaidi ya asilimia 70 yanayotokana na wanyama.

Alisema jukwaa lililoundwa na wataalamu kutoka mradi wa Afya Moja litaimarisha uwezo wa kitaifa wa kubaini uwepo wa viashiria vya milipuko ya magonjwa na matukio mengine yanayoweza kuathiri afya ya binadamu, wanyama na mazingira.




Muuza kahawa, Hassan Hassan kutoka Magomeni, wilayani Bagamoyo, akionesha mfano wa hundi ya Sh. milioni moja jijini Dar es Salaam juzi, aliyoshinda katika promosheni inayoendelea ya Shinda Ndinga na Mamilioni ya Pesa inayoratibiwa na Tigo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## TARURA Chalinze yawasilisha bajeti

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

MENEJA wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) Wilaya ya Bagamoyo, Mhandisi Emmanuel Ndyamukama, amewasilisha Mpango na Bajeti wa Matengenezo ya Barabara kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kwa Halmashauri ya Chalinze ambayo imepitishwa na Baraza la Madiwani.

Akiwasilisha kwenye kikao cha Baraza Maalumu la Madiwani wa Halmashauri ya Chalinze kilichofanyika jana, Ndamukama alisema bajeti hiyo inalenga kuhakikisha maeneo yenye huduma za kijamii na uzalishaji yanafikika kwa urahisi, kata zote zinaunganishwa na pia Halmashauri ya Chalinze inaunganishwa na wilaya jirani.

Pia alisema bajeti hiyo pia itajikita na kuhakikisha takataka na magugu kwenye mifereji hasa barabara za mitaa vinaondolewa na mvua zinaponyesha na maji kupita bila shida.

Mhandisi Ndyamukama alisema mpango huo wa bajeti utatekelezwa kupitia Sh. milion 695 kutoka Mfuko wa Barabara ambazo zitafanya matengenezo ya barabara kilomita 82.1, fedha za tozo Sh. bilioni moja ambazo zitafanya matengenezo ya kilomita 82.

Pia alisema Sh. milioni 500 kutoka Mfuko wa Jimbo, zitafanya matengenezo ya kilomita 18 na Mpango wa Matengenezo wa Fedha za Maendeleo, Sh. bilioni 7.3 zitatumika katika matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilomita 97.7 katika viwango mbalimbali kwa maana ya changarawe na lami.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Chalinze, Hassan Mwinyikondo, kwa niaba ya madiwani, alipongeza TARURA kwa bajeti hiyo huku akielekeza taasisi zingine kuiga utamaduni unaofanywa na wakala kwa kuweka bayana shughuli zinazofanyika kwa maslahi ya wananchi.

# Sekta binafsi kushirikishwa miradi kimkakati

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema itashirikiana na sekta binafsi, ndani na nje ya nchi ili kuongeza kasi ya ujenzi wa miradi ya kimkakati kwa maendeleo ya taifa, kiuchumi na kijamii.

Hayo yalisema juzi jijini Arusha na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi), Ludovick Nduhiye, wakati akifungua semina ya siku mbili (2) iliyoandaliwa na wizara hiyo kwa kushirikiana na Chama cha Barabara Tanzania (TARA) katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano Arusha (AICC).

"Kama nchi tuna miradi mingi inayoendelea kutekelezwa, hivyo nia yetu ni kuharakisha miradi hiyo kwa kuhusisha sekta binafsi hususani kwa miradi ya barabara, madaraja, viwanja vya ndege na miradi mingineyo", alisema. Nduhiye alisema serikali imetangaza kuanza ujenzi wa barabara kupitia ubia na sekta binafsi katika mradi wa barabara ya Kibaha - Morogoro (highway) na barabara ya Igawa - Tunduma mkoani Mbeya.

Alisema semina hiyo ina lengo la kuwajengea uelewa na uwezo wa mambo muhimu kuanzia kuandaa makabrasha ya mradi mpaka utekelezaji wake. Wadau muhimu waliohusishwa ni sekta za ujenzi na uchukuzi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Wizara ya Fedha na Mipango ili miradi hiyo inapoanza kutekelezwa isikwame kwa namna yoyote.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Hadija Hamisi Rajabu, alisema miongoni mwa tija za ushiriki wa serikali ya Zanzibar ni pamoja na kutatua changamoto ya kukwama kwa miradi kwa kukosa utaalamu.

"Katika utekelezaji wa miradi kama hii kwa upande wa sera na sheria ziko vizuri lakini wakati wa utekelezaji ndipo kunapotokea sintofahamu kwa kuwa hili jambo hatujalielewa vizuri sana na ndiyo maana tupo hapa ili kuona wapi tulikuwa tunakosea na namna sahihi ya kuepuka changamoto pindi zinapojitokeza," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Barabara Tanzania (TARA), Joseph Haule, alisema mafunzo hayo yameandaliwa kwa kushirikiana na wizara ili wataalam wajifunza kutoka katika nchi ambazo zimetekeleza miradi kama hii na kupata njia sahihi ya kuepuka makosa yanayoweza kujirudia katika utekelezaji wa miradi hiyo.

Semina hiyo imewakutanisha wataalamu mbalimbali wa masuala ya miundombinu nchini na baadhi ya wataalamu kutoka nchi za Afrika Kusini na Brazil.



## Huduma mbovu Hospitali Pangani yamchefua kigogo CCM

**Na Oscar Assenga,** PANGANI

HUDUMA mbovu za tiba na uchunguzi zinazotolewa katika Hospitali ya Wilaya ya Pangani, mkoani Tanga 'zimemchefua' Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoani humo, Rajab Abdurhaman ambaye ameahidi kutafuta haraka mwarobaini wake ili wananchi wapate huduma stahiki na kwa wakati.

Akizungumza jana wilayani humo, Rajab alisema haileti afya kuona bado kuna watu wanachezea kazi na kukiuka maadili ya taaluma zao, wakati kuna wagonjwa wanahitaji huduma.

Akieleza namna asivyoridhishwa na huduma hizo, Rajab alisema: "Hospitali ya Wilaya ya Pangani imeoza. Mgonjwa anakwenda kupata huduma anakaa saa mbili, daktari hajatokea.

"Hatuwezi kukubali hili ndugu zangu. Mgonjwa anapelekwa anakosa huduma, maumivu yamemjaa, nesi (muuguzi) anachukua simu yake anachati, hatuwezi kukubali na haya ndio yaliyonifanya niombe nafasi hii," alisema.

Aidha alisema CCM haifurahishwi na thamani halisi ya fedha zilizotumika katika ujenzi wa Jengo la Wagonjwa Mahututi (ICU) la hospitali hiyo.

Alisema: "Haiingii akilini kwamba serikali imepeleka mamilioni ya fedha kwa ajili ya kujenga ICU lakini jengo lilipofikia fedha zimekwisha na jengo halijakamilika.

"Mbona katika maeneo mengine, yako majengo yaliyokamilika kwa kutumia kiwango hicho hicho cha fedha zilizotolewa na serikali? Kama chama kinachosimamia ilani, tunahitaji maelezo ya kutosha ni kwa nini jengo hilo halijakamilika."

Katibu wa CCM wa Mkoa wa Tanga, Suleiman Mzee, alisema watalifikisha suala hilo kwa Mbunge wa Pangani, Jumaa Aweso ili afuatilie maendeleo ya mradi huo na kuipa taarifa CCM.

# Wabunge EALA waapishwa, watoa ahadi lukuki

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WABUNGE wapya wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EALA), wameapishwa ili kuanza rasmi kazi ya kutumikia wadhifa huo kwa kipindi cha miaka mitano.

Kazi ya kuwaapisha wabunge hao kutoka nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki iliongozwa na Katibu wa Bunge hilo, Alex Obarti.

Akizungumza baada ya kuapishwa, Mbunge James Millya (Tanzania), aliwaomba Watanzania kuchangamkia fursa zilizoko ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), hasa zile zinazohusu nyanja za kibiashara.

"Nitakuwa balozi kuhakikisha natembelea vijiji, wilaya na kila mkoa kuhakikisha naisemea Tanzania na fursa zilizoko katika EAC ili kila mtu achangamkie fursa hii," alisema.

Kwa mujibu wa Ole Millya yupo tayari pia kutembelea vyuo vikuu na mahali pengine kwa ajili ya kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji, kwani ndani ya EAC kuna fursa mbalimbali ikiwamo kilimo.

Aidha, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan na Watanzania kwa kumwamini na kumchagua kuwa miongoni mwa wabunge kutoka Tanzania.

Baada ya uapisho huo, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Stergomena Tax, aliwasihi wabunge wa EALA kuendeleza mambo mazuri yanayotakiwa kufanywa kwa ajili ya kuimarisha utangamano wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Pia aliwahimiza wajikite katika kupigia kelele kwenye masuala ya kukuza biashara, kwenda pamoja kama jumuiya pamoja na masuala mengine ili kutoa fursa mbalimbali za kiuchumi.

Aidha, aliwahimiza kugusia umuhimu wa kila nchi kutoa michango kwa wakati ili EAC itimize majukumu na malengo waliyojiwekea.

Shughuli ya kuapishwa kwa wabunge hao ilihudhuriwa pia na spika wastaafu akiwamo Abdulrahaman Kinana, Martine Ngoga na Margareth Ziwa.

Wengine walioshuhudia uapisho huo ni mawaziri kutoka nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Wabunge walioapishwa kutoka Tanzania ni Angela Kizigha, Nadra Mohamed, Dk. Shogo Mlozi, Dk. Abdullah Makame, Machano Ali Machano, Mashaka Ngole, Ansar Abubakari Kachwamba, James Millya na Dk. Ng'waru Maghembe.



Mwenyekiti wa Nyanza Group Mji Mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, Malimi Kija (kushoto), akikabidhiwa fulana na Ofisa Maendeleo ya Jamii Mirerani, Isack Mgaya, kwenye uzinduzi wa fulana na kalenda, Sh. milioni 4.8 zilipatikana kutunisha mfuko wao juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Aweso atoa mil.10/- ukarabati wa miundombinu ya soko

**Na Hamida Kamchalla,** PANGANI

WAZIRI wa Maji, Juma Aweso, amesema havutiwi na uchakavu wa miundombinu ya Soko la Pangani lililoko mkoani Tanga, kwa kuwa linahatarisha maisha ya wakazi wa wilaya hiyo na walaji wa bidhaa zinazouzwa sokoni hapo.

Kutokana na taswira mbaya ya soko hilo kwa sasa, Aweso alitoa mchango wa Sh. milioni 10 kwa Halmashauri ya Pangani ili zitumike katika kuweka bati mpya.

Aweso ambaye ni Mbunge wa Pangani (CCM), alikabidhi fedha hizo jana kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo.

"Nimetoa fedha hizi kwa ajili ya kuanza ujenzi wa soko, nataka mtoe mabati yote chakavu haraka ili kuepuka uharibifu wa bidhaa za vyakula, athari za kiuchumi kwa wafanyabiashara na matatizo kwa walaji wa bidhaa zinazopatikana kwenye soko hili.

"Nimefanya hivi baada ya kupokea malalamiko ya muda mrefu ya wafanyabiashara kuhusu ubovu wa soko letu. Kwanza ninyi mnajua hakuna hata miundombinu muhimu na kuna mahitaji ya kibinadamu yanakosekana hapa."


"Nitamwelekeza Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji, maji yaletwe hapa, lakini jambo moja niwasihi. Hili ni eneo lenu la kazi, kwa hiyo ndugu zangu wafanyabiashara, mkilitunza ndipo mtakapofanya kazi zenu vizuri," alisema.

Baada ya makabidhiano hayo, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Tanga, Rajabu Abdallah, alisema yupo kwa ajili ya kutekeleza ilani ya chama hicho na kwamba kero zote zinazowakabili wananchi wa Tanga, zitatatuliwa kulingana na muda lakini katika utengaji wa bajeti.

Alisema: "Nimezaliwa Pangani, nazijua kero nyingi zilizoko katika soko hili. Nalijua sana kwa maana wakati linajengea mimi nilikuwa mdogo sana, mbali ya kero za soko kuanza kufanyiwa kazi, nimewania nafasi hii kuona bado kuna maeneo yanahitaji kufanyiwa kazi, sipo hapa kupiga siasa, niwaahidi ninatoa miezi mitatu kero zote zitatuliwe".

Awali wafanyabiashara wa soko hilo, akiwamo Mariam Said, alilalamikia soko hilo kukosa miundombinu ya maji, choo na umeme, akisema kuwa ni chakavu hali inayowakosesha amani.

Alisema: "Hapa kero kubwa ni maji na umeme hasa hili la umeme linatunyima usingizi kabisa, ikifika usiku hapa ni kiza kinene kwa maana akiingia mtu kuiba huyo mlinzi hajui atamkamata sehemu gani, lakini umeme ukiwaka hapa hata huyo mwizi ataona haya kuja kuiba".





# Wafanyabiashara wa ngozi Moshi walia kukosa mikopo

**Na Mary Mosha,** MOSHI

BAADHI ya wafanyabiashara wadogo wa bidhaa za ngozi (wenye ulemavu) Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro, wameiomba serikali kuwapa vipaumbele kwenye mikopo ya halmashauri pamoja na kusikiliza matatizo yao ili waweze kujikimu kiuchumi.

Wakizungumza na Nipashe katika nyakati tofauti, Edwald Msaki, mkazi wa Msaranga alisema bado upatikanaji wa mikopo hasa kwa halmashauri kuna ushindani mkubwa hasa kwa watu wenye ulemavu.

"Tunajua wote wanahaki sawa ya kupewa mikopo, ila sisi tunaomba watuangalie kwa namna ya pekee, tumeamua kuacha kuombaomba kutokana na ulemavu wetu na badala yake kujikita katika kutengeneza bidhaa za ngozi na kufanya biashara," alisema.

Eliasi Mrutu ni Mkazi wa Mji Mpya alisema uwapo wa tatizo la mikopo ungeweza kutatuliwa kwa kuangalia upya uhitaji hasa kwa watu wenye ulemavu waliojikita katika biashara ndogo.

Zakaria Melkizideck ni Mkazi wa Njoro kwa Dobi, alisema ipo haja ya serikali hasa za halmashauri kuona namna ya kuwatazama watu wenye ulemavu katika upatikanaji wa mitaji na matatizo wanayokabiliana nayo.

Aidha, Meya wa Manispaa ya Moshi, Zubery Kidumo, alisema manispaa hiyo inafuata sheria taratibu na kanuni katika utoaji wa mikopo kwa rika zote zilizoainishwa na sheria.

**Aidha, Meya wa Manispaa ya Moshi, Zubery Kidumo, alisema manispaa hiyo inafuata sheria taratibu na kanuni katika utoaji wa mikopo kwa rika zote zilizoainishwa na sheria.**

"Manispaa ya Moshi inafanya kazi zake kwa mujibu wa sheria taratibu na kanuni, hakuna upendeleo na pesa hutolewa kila baada ya robo mwaka, tumepokea ombi la wenzetu ingawa sheria inawatambua kwa kupewa fedha,"alisema Kidumo.

Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Abbas Kayanda, aliiambia Nipashe kuwa wapo tayari kuwahudumia watu wote kwa mujibu wa sharia, taratibu na kanuni.

Akiwa mkoani Kilimanjaro Julai 30, Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Tixon Zunda, alizitaka halmashauri nchini kuvunja urasimu kwa wadau wa sekta ya ngozi badala yake wakae pamoja na kuondoa vikwazo kwa wadau hao hasa kwa watu wenye ulemavu.



Mbunge wa Moshi Mjini, Priscus Tarimo (wa tatu kulia), akipata kikombe cha kahawa ya asili pamoja wananchi wa jimbo lake katika Kata ya Kiborilonі, Manispaa ya Moshi juzi. **PICHA: JAMES LANKA**

## Walikimbia soko kisa uhaba wateja

**Na Hamida Kamchalla,** KOROGWE

WAFANYABIASHARA katika soko jipya la Halmashauri ya Mji wa Korogwe mkoani Tanga wamesusa kufanya shughuli zao licha ya serikali kutumia zaidi ya Sh. bilioni 1.2 kujenga soko hilo.

Hali hiyo ilifahamika juzi baada ya Ofisa Biashara wa Halmashauri hiyo, Farjala Msangi, kuwasilisha taarifa rasmi kwa Mkuu wa Mkoa huo, Omari Mgumba.

Katika taarifa yake, Msangi, alisema wafanyabiashara wa Mji wa Korogwe wamelitelekeza soko hilo kwa kukataa kufanya biashara zao kwa madai kuwa ni mbali na mji, hivyo hakuna wateja.

Aidha, Msangi alieleza kuwa halmashauri hiyo ilitekeleza mradi huo kwa asilimia 100 lakini wamekutana na kikwazo cha wafanyabiashara kugoma kulitumia.

Akizungumzia juu ya mgomo huo Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omari Mgumba alisema: "Serikali imetupa fedha nyingi kujenga soko hili, lakini halina faida. Nimemwagiza Mkuu wa Wilaya, akisaidiana na kamati yake ya ulinzi na usalama, ndani ya siku 14 kuwe hakuna mfanyabiashara hata mmoja anayeshusha mazao yake shambani nje ya soko hili. Ni lazima magari yote yaingie kushusha bidhaa zao ndani ya soko hilo kuanzia sasa".

Alipoulizwa Mkuu wa Wilaya ya Korogwe, Basila Mwanukuzi, kuhusu taarifa hiyo, alikiri kuwapo kwa tatizo hilo, akisema hivi sasa anatafuta ufumbuzi wa tatizo hilo.

"Soko hilo limekamilika kwa asilimia 100 na halina shida kwenye utekelezaji. Tumeyapokea maelekezo ya kutaka lianze kutumika, kwamba wafanyabiashara washushie mizigo yao hapo.

"Nimepokea maelekezo ya Mkuu wa Mkoa na tutalifanya hili kwa nguvu zetu zote kuhakikisha linatekelezeka. Soko hili lina uwezo wa kuchukua wafanyabiashara zaidi ya 100 kwa wakati mmoja," alisema Mwanukuzi.

# Polisi yaingizwa katika mfumo maalum ukamataji wahalifu

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

JUKWAA la Maendeleo la Mkoa wa Kilimanjaro (KDF), limewaingiza katika mfumo maalum wa closed user group (CUG) maofisa wakaguzi na askari polisi 1,504 ili waweze kufuatilia mienendo na taarifa za kiuhalifu.

KDF na kampuni ya simu za mkononi ya Vodacom wameingia makubaliano ya kuwapa polisi mkoani humo namba mpya za simu ili waweze kuwasiliana bure na hakuna atakayeingia gharama ya kuwasiliana na askari mwenzake wenzake. Akizungumza jana wakati wa uzinduzi wa programu hiyo, Mwenyekiti wa Bodi ya KDF, Mahmood Mringo, alisema mapumziko ya mwisho wa mwaka ya mwaka huu yatasherehekewa kwa staili mpya, ikiwamo kutangazwa siku maalumu ya mapumziko ya Sikukuu ya Krismasi na Mwaka Mpya.

Jukwaa la KDF, limependekeza kuwapo kwa tafrija fupi ambayo itafanyika kila mwaka, kati ya Desemba 15 hadi 19, kutumika kuzindua mapumziko hayo.

"Tunataka kutangaza siku maalumu ili kuongeza hamasa na thamani ya sherehe za Krismasi na Mwaka Mpya. Haitakuwa siku inayotambuliwa na serikali, bali itakuwa ni siku ya ishara tu kwa kuanza rasmi kwa mapumziko ya mwisho wa mwaka.

"Tunataka kutumia kipindi hiki kuleta sura mpya na ya kisasa katika kujenga Kilimanjaro kama kivutio. Watu waje kwa wingi, wafurahi na kustarehe na familia zao kwa amani na wajipange kwa mwaka mpya."

Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo, Kamishna Msaidizi (ACP), Simon Maigwa, licha ya kuishukuru KDF kwa kuja na wazo hilo, alisema Jeshi la Polisi imejipanga kuimarisha ulinzi sehemu za ibada, mikusanyiko ya watu kwa wageni na wakazi wa mkoa huo.

"Tunaelekea mwisho wa mwaka 2022, Mkoa wa Kilimanjaro huwa na ongezeko la wageni wanaofika kwa ajili ya sherehe za mwisho wa mwaka. Tumejipanga kuimarisha ulinzi sehemu za ibada, mikusanyiko ya watu, wananchi wote, wageni na wakazi wa Kilimanjaro.

"Tunawataka waheshimu sheria, kanuni na taratibu. Aidha, tunaendelea na misako ya kuwabaini na kuwakamata wakiukwaji wa sheria za usalama barabarani wakati wote kwa mchana na usiku."

Ukurasa 14




**Mabadiliko ya tabianchi yanavyochochea ukatili**

Ukurasa 15



MABALOZI KIDUCHU
Rais Samia anakumbushwa afanye kitu, uchache wanadiplomasia wanawake

Ukurasa 19



**MLUNGULA KOMBE LA DUNIA ULIVYOBOMOA BUNGE ULAYA**

siasa
JUMATANO DESEMBA 21, 2022
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU

NYOTA YA BIBI TITI HIYO

# UWT yatamani kiwepo kigoda kumuenzi, hakuwa msomi, ila amefanya maajabu

**Na Sabato Kasika**

BIBI TITI Mohamed ni mwanamama shupavu anayeenziwa na wengi Tanzania Bara na Visiwani na katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini kwa kushiriki kwa hali na mali kwenye harakati za ukombozi na kufanikisha kupatikana uhuru.

Kwa mchango wake huo, Bibi Titi anapata heshima kubwa miongoni mwa Watanzania kwa mchango wake mkubwa katika maendeleo ya nchi, kulinda uhuru, amani na haki za wanawake nchini na hata bara zima la Afrika.

Ni baada ya miaka 22 ya kifo chake, akifarika Novemba mwaka 2000, wiki iliyopita linafanyika kongamano la kumuenzi, linaloandika historia wilayani Ikwiriri Rufiji mkoani Pwani, kuibua na kujadili mchango wa mwanasiasa huyo mahiri kwa taifa.

Likiandaliwa na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT), Mary Chatanda anatoa ahadi za kumuenzi,

Anasema UWT itafuata nyayo zakekwa kuondokana na mawazo ya kusubiri kuwezeshwa, badala yake kujiamini na kuonyesha uwezo walionao ili wafike mbali bila msukumo mkubwa kutoka nje.

Anasema Bibi Titi alikuwa ni jasiri, anayejiamini na mwenye kuonyesha uwezo wake na kwamba wana UWT hawana budi kufuata nyayo hizo, ili kusaidia nchi kusonga mbele kimaendeleo.

"Katika miaka ya 1950, alikuwa miongoni mwa wale waliopigania uhuru wa Tanganyika kutoka kwa Muingereza akiwa na Baba wa Taifa Mwalimu Juliu Nyerere,



Mary Chatanda Mwenyekiti wa UWT Taifa; akizungumza kwenye Kongamano la Bibi Titi Mohamed. **PICHA: CCM**

Waziri Mkuu Rashid Kawawa na viongozi wengine wa TANU," anakumbusha Mary.

Anaongeza:"Bibi Titi alikuwa mwanamke wa kwanza kujiunga na harakati mbalimbali za kupigania uhuru wa Tanganyika, na kwamba mwanzoni mwa harakati zake za kisiasa alishawishi wanawake kujiunga pamoja naye kudai uhuru."

"Kama kiongozi wa tawi la wanawake wa TANU, alikuwa na jukumu la kushawishi wanawake kuunga mkono sera na maoni ya chama, nasi hatuna budi kufanya hayo ili kushawishi wengine kujiunga na CCM," anasema Mary.

**KUANZISHIWA KIGODA**

Mwenyekiti wa UWT anasema ipo haja ya kuanzisha taasisi ambayo itajihusisha na Bibi Titi kama ilivyo Kigoda cha Mwalimu Nyerere, lakini pia kuwa na siku maalum la kuadhimisha siku ya mwanasiasa huyo.

"Ikiwezekana, kiandikwe kitabu cha kumwelezea kiongozi huyo shupavu, mwanaharakati na mpigania uhuru wa Tanganyika na ninaipongeza wizara kwa kuandaa kongamano na tamasha hili," anasema.

Kufanyika kwa kongamano hilo, ni ishara kwamba wizara hiyo ina mchango mkubwa, katika historia ya kuwaenzi wapigania uhuru na kuendeleza masuala ya maendeleo, hasa ya wanawake.

"UWT inaamini katika kaulimbiu ya kongamano hili ya mwanamke ni jeshi imara katika kuleta mabadiliko, tumuenzi. Huo ndio ukweli, kwani chini ya Rais Samia Suluhu Hassan tumeona mambo makubwa anayofanya," anasema.

Anamtaja kuwa tangu nchi kupata uhuru, na Rais Samia ndiye anapaswa kuitwa Bibi Titi wa leo.

"Tunaweza kumwita Bibi Titi wa leo, kwa sababu katika uongozi wake wa miaka miwili tumeona namna ambavyo ameleta mageuzi ya kihistoria katika kuendesha nchi," anasema.

Anasema serikali yake imejenga miundombinu ya huduma za afya, elimu ikiwamo vyuo vya VETA na shule ya wasichana ya Mkoa wa Pwani iliyopewa jina la Bibi Titi Mohamed.

"Mambo yote hayo na mengine yanaonyesha kweli kwamba Rais Samia ni Bibi Titi wa sasa anaeyaishi maono ya waasisi wa taifa hili na kuwa jasiri katika

INAENDELEA UK. 20

# Mabadiliko ya tabianchi yanavyochochea ukatili

**Na Mwandishi Wetu**

MABADILIKO ya tabianchi ni kilio cha dunia kwa sasa kwa sababu athari zake zinawaumiza wanadamu na viumbe hai karibu wote, lakini kwa wanawake na mabinti ni maumivu mara mbili, hasa kwa mataifa maskini ya Afrika Kusini ya Jangwa la Sahara ikiwamo Tanzania.

Haya yanaonekana kutokana na majukumu mengi kuachwa kwenye utendaji na usimamizi wa kinamama, kuanzia kusaka chakula, maji, kutafuta nishati na kutunza nyumba au makazi ya familia zao.

Itakumbukwa kuwa athari za mabadiliko ya tabianchi ni pamoja na uhaba wa chakula, kuni za kupikia, kuwapo joto kali, ukosefu wa maji, malisho ya wanyama, mafuriko na vimbunga vinavyoharibu makazi na maisha.

Kiafrika mwanamke ndiye mlezi wa watoto, mtafutaji wa maji, kuandaa chakula na usafi wa makazi ya familia, hivyo kama hakuna chakula , maji anawajibika kuvitafuta kokote ili familia istawi, ndiyo maana wamekuwa wahanga wakubwa.

Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), umeona jambo hilo na sasa unaiomba jamii kutumia mbinu za kuhifadhi maji ili wanawake wasitendewe ukatili na kushindwa kutoa mchango kwenye maendeleo ya nchi.

Ni moja ya ajenda kwenye mjadala muhimu wa kongamano la wanawake na uongozi linalowaleta pamoja wanawake zaidi ya 200 kutoka mikoa mbalimbali.

Ni ndani ya siku 16 za kupinga ukatili dhidi ya makundi yote kwenye jamii kwa kauli mbiu ya 'kila uhai una thamani, tokomeza mauaji na ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

Na TGNP imewaleta pamoja ili kujadili na kutathimini suala zima la uwekezaji na utumiaji wa rasilimali na kuongeza ushiriki wa wanawake katika uongozi ili kutokomeza ukatili wa kijinsia nchini.

Mwenyekiti wa TGNP, Gemma Akilimali, anasema kongamano hilo pia limekuja wakati ambapo masuala ya mabadiliko ya tabianchi yameshika kasi na changamoto zake zimekuwa zikiongeza ukatili wa kijinsia hususani suala la ukosefu wa maji na nishati.

"Ninawaasa viongozi wa mashirika katika maeneo yenu ya kazi mtumie nafasi zenu kuelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kutunza mazingira na hususani vyanzo vya maji, kuhakikisha kuwa hawapeleki mifugo kwenye vyanzo hivyo ili kusaidia upatikanaji wa maji safi na salama.

"Elimisheni vilevile kuvuna maji ya mvua kwa matumizi mbalimbali.Tukumbuke kuwa maji ni uhai, na bila maji maisha yanakuwa magumu hususani kwa wanawake ambao hutumia muda mwingi kutafuta maji badala ya kufanya kazi za kuongeza kipato."

Aidha, anawaomba wataalamu kutayarisha nishati mbadala nafuu kwa wananchi wa kipato cha chini ili kupunguza matumizi ya kuni.

"Ikilazimu watu kukata miti, basi utaratibu wa panda mti, kata miti utumike ili kuboresha mazingira. Ni kwa kufanya hivyo tu, ndipo tutaweza kukabiliana na ukame unaotishia usalama wa chakula katika nchi yetu. Ninawaomba pia kila mtu ajitahidi kuipanda anapopata fursa ya kufanya hivyo," anahimiza.




Mwenyekiti wa Bodi ya TGNP, Gemma Akilimali (kushoto), akimkabidhi zawadi Waziri Dorothy Gwajima, kwa jitihada za kupambana na ukatili **PICHA:MWANDISHI WETU**

Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, Lilian Liundi, anasema uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi hayataacha watu salama katika suala la ukatili wa jinsia, wanawake na wasichana wanapitia magumu wakati wa kutafuta nishati za kupikia, maji, chakula cha mifugo na maeneo ya kulima.

"Wanawake wanabakwa na kupigwa huko msituni wakati wanasaka kuni. Pia wanaporejea nyumbani hawako salama wanapata vipigo kwa wenzi wao huku wengine wakikaguliwa kama waligawa ngono wakiwa kwenye zoezi la kusaka kuni,"anasema na kuongeza:

"Kwa nishati hii adhimu kusogea mbali kutokana na mabadiliko ya tabia nchi wanawake hutumia saa nyingi kutafuta kuni huku majukumu ya kutoa huduma za kifamilia na kijamii yakiwa bado yanawaelemea. Ni muhimu sana kujadili na kuwekeza katika teknolojia na ubunifu ili kupata nishati mbadala ya bei nafuu kuwanusuru wanawake na wasichana na ukatili wa jinsia."

Aidha, Lilian anasema maji ni changamoto inayochangiwa na mabadiliko ya tabia nchi kutokana na wanawake wanatumia muda mrefu, wanapigwa, wanaombwa rushwa ya ngono, saa nyingi ya kutafuta maji yanawaongezea mzigo wa majukumu, na kwamba ni muhimu kutafuta ufumbuzi wa changamoto hizo ili kupunguza ukatili wa kijinsia.

**UNYANYASAJI KITEKNOLOJIA**

Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP , anasema maendeleo ya sayansi na teknolojia hayatawaacha watu salama kwa kuwa yamekuja na aina mpya za ukatili wa jinsia hayajatuacha salama, yamekuja na aina mpya za ukatili wa jinsia hususan wa kwenye mitandao, na kwamba ni muhimu kuchukua hatua za haraka kutafuta ufumbuzi changamoto hiyo inayokua kwa kasi.

Liliana anasema ukatili dhidi ya wenza na mauaji ya wanawake yamekuwa tishio dhidi ya wanawake nchini na kwamba mwaka 2021, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kilikusanya jumla ya matukio 35 ya mauaji yaliyosababishwa na ukatili dhidi ya wenza ambazo zilionyesha wahanga asilimia 86 ni wanawake.

Anasema: «Kuli mbiu ya mwaka huu, kila uhai una thamani, tutokomeze mauaji na ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Inaitaka jamii kuthamini uhai wa mwenzake kwa kuwa kila mtu ana haki ya kuishi na hakuna mtu kwa sababu zozote anahaki ya kuondoa uhai wa mwenzake. Kila mtu ana wajibu wa kufanya.'

**HISTORIA SIKU16**

Mwenyekiti wa TGNP, Gema Akilimali akikumbusha historia ya siku 16 kijinsia ni kampeni ya kimataifa iliyoanzia kwenyemkutano wa kwanza wa Taasisi ya Uongozi wa Wanawake Duniani (Women's Global Leadership Institute) mwaka 1991.

Washiriki walichagua tarehe 25 Novemba, siku ya kimataifa ya kupinga ukatili dhidi ya wanawake, na Desemba 10, siku ya haki za binadamu duniani, ili kuhusianisha ukatili dhidi ya wanawake na haki za binadamu kuhamasisha na kusisitiza kuwa ukatili kama huo ni ukiukaji wa haki za binadamu.

**MIJADALA JINSIA**

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, anasema kukabili matukio ya ukatili kunahitaji ushiriki wa jamii yote huku akitaka kamati kutekeleza wajibu wake ipasavyo. "Ni aibu kunakuwa na mkutano au baraza la madiwani halafu hakuna ajenda ya ukatili wa kijinsia, lazima tujadiliane kuanzia ngazi ya mtaa ili tukabili matukio haya ambayo yanashamiri. Hata kama muhusika atakamatwa na kufikishwa mahakamani na kufungwa lakini tayari aliyetendewa ameathirika kisaikolojia,"anasema.

Anasema ukatili unaanzia ndani ya familia na wakati mwingine matukio hayaripotiwi kwasababu waliotenda ni wanafamilia wenyewe ambao hukaa kikao kumaliza, jambo ambalo linabaki kuwa maumivu kwa waliyetendewa na hudnda naye akiwa mkubwa atatenda kwa mwingine.

"Tusisahau kuwa usawa wa kijinsia ni msingi katika kujenga dunia tuipendayo; isiyo na ukatili kwa wanawake, wasichana na hata wavulana na wanaume na watoto. Hilo linawezekana ikiwa kila mmoja wetu katika nafasi yake atachukua hatua sasa kukomesha vitendo vya ukatili wa kijinsia," anasema Waziri Gwajima.

MABALOZI KIDUCHU

# Rais Samia anakumbushwa afanye kitu, uchache wanadiplomasia wanawake

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**



Balozi wa Tanzania Burundi Dk.Jilly Maleko , akizungumza katika kongamano la Kiswahili kinavyounganisha diplomasia na uchumi nchini Burundi .**PICHA :UBALOZI BURUNDI**

WAKATI dunia inapigania usawa wa jinsia katika nafasi za uongozi kada ya diplomasia na uwakilishi wa kimataifa, imeachwa mbali kwenye kuufikia usawa huo, na kwamba kati ya mabalozi 49 wanaoliwakilisha taifa ughaibuni wanawake ni 13 pekee.

Kati ya mabalozi 49 wanaoiwakilisha nchi sehemu mbalimbali duniani wanawake ni asilimia 26.5 na idadi yao ni 13 pekee.

Na kama haitoshi kati ya hao 13 wanane ndiyo mabalozi kamili waliopangiwa vituo vya kazi na watano ni makonsela (mabalozi wadogo) ambao hawajapangiwa vituo bado.

Licha ya uwepo mdogo wa wanawake katika nafasi hizo lakini hao wachache wanaelezwa kuwa wanafanya kazi nzuri kwenye diplomasia ya uchumi.

Balozi wa Tanzania nchini Burundi,Dk Jilly Maleko, ni miongoni mwa mabalozi wanawake wanane wenye vituo vya kazi kati ya 13. Akizungumza na Nipashe visiwani Zanzibar, anasema:

"Kutokana na idadi kubwa ya wanawake wa Tanzania ambao ni asilimia 52 kwa mujibu wa sensa ya mwaka huu ipo haja ya kuangaliwa upya namna ya ushiriki wao kwenye masuala ya kibalozi na diplomasia ya kimataifa ".

Anatoa mfano kuwa Burundi ni nchi inayoheshimu wanawake na katika masuala ya jinsia ipo vizuri na bunge lao limevuka asilimia 40 ya usawa wa kijinsia katika uongozi hapa Afrika Mashariki.

"Nikiwa huko nimeona namna wanawake wanavyoweza kufanya kazi mbalimbali . Hii ni kuonyesha jinsi gani wanawake wanapewa kipaumbele kwenye nyanja tofauti za kiuchumi, jamii na hata siasa", anaongeza.

Akizungumzia hali ya Tanzania anasema wapo wasomi wengi wanawake na ana imani na Rais Samia Suluhu Hassan kuwa ataliona hilo na kulifanyia kazi.

Mkurugenzi Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali Balozi Mindi Kasiga, anasema licha ya idadi ndogo ya wanawake katika nafasi ya ubalozi lakini wachache waliopo wanafanya kazi vizuri sawa na wanaume.

"Mabadiliko hayahitaji haraka hivyo imani yangu ni kwamba idadi hiyo itazidi kuongezeka hasa ikizingatiwa kuwa nafasi ya Urais wa Tanzania inashikiliwa na mwanamama Rais Samia"

Anasema jamii imeanza kubadilika na kumuona mwanamke ni imara na anapopewa majukumu ya kazi anayatekeleza kikamilifu bila ya kujali maumbile yake ya kijinsia.

"Tunapotoka Watanzania na sasa tulipo mambo yanabadilika kidogokidogo kuhusu nafasi za wanawake katika uongozi na idadi ya mabalozi wanawake kufikia 13 tunatoka mbali zamani walikuwa wachache zaidi," anasema Jilly.

Chuo kinachotoa Kozi ya Diplomasia Zanzibar cha Utawala wa Umma (IPA) ndicho chuo pekee kwa Zanzibar kinafundisha elimu ya uhusiano wa kimataifa na diplomasia na kinasema ushiriki wa wanawake kusomea fani hiyo ni mzuri.

Mkuu wa Utawala wa IPA Muhammed Khamis Mtumwa, anasema kwa mwaka 2020/2021 wanafunzi wa kada hiyo ni 28 kwa ngazi ya shahada ya kwanza wanawake ni 14 na wanaume 14, mwaka 2021/2022 ni 54 wanawake 29 na wanaume 24 na kwa mwaka 2022/2023 wanafunzi wote ni 87, wanawake 47 na wanaume 40.

Anaongeza kuwa ipo haja ya wanawake kujengewa uwezo tangu wakiwa katika ngazi ya chini kielimu ili wanapomaliza masomo wawe na sifa, ujasiri na uwezo wa kupata nafasi za uongozi.

Naibu Katibu Mkuu, Fatma Rajab Naibu, anayeongoza Wizara ya Mambo ya Ndani anasema, mabalozi ni nyenzo muhimu katika kuimarisha deplomasia ya uchumi na sera ya mambo ya nje hivyo ni vyema kuendelea kutafuta ufumbuzi wa changamoto mbalimbali zilizopo.

Balozi Fatma ambaye ni miongoni mwa mabalozi wanawake wanaotoka visiwani Zanzibar, anasema mkutano wa mabalozi wa Tanzania uliofanyika mwishoni mwa mwaka huu visiwani hapa, umetoa nafasi wa kujadili utendaji wa kazi za mabalozi wote katika balozi zao, mwenendo wa dunia na taathira yake katika diplomasia ya uchumi, nafasi ya itelejensia katika utekelezaji wa diplomasia ya uchumi na fursa na mikakati ya kuiwezesha Tanzania kunufaika na eneo huru la biashara.

> "Mabadiliko hayahitaji haraka hivyo imani yangu ni kwamba idadi hiyo itazidi kuongezeka hasa ikizingatiwa kuwa nafasi ya Urais wa Tanzania inashikiliwa na mwanamama Rais Samia"

Akizungumza kuhusiana na nafasi yake hiyo, anasema kuwa Rais amemwamini na kumteua tena baada ya kuridhika na utendaji wake akiwa balozi kabla ya jukumu hilo la sasa.

"Naamini kuwa mabadiliko hayaji siku moja lakini kabla hatujafikia hatua tuliyopo leo ya idadi ya mabalozi wanawake inahitaji kuongezwa kwani inaonekana dhahiri utendaji wa mabalozi wanaume ni mzuri lakini wanawake tunawazidi", anasema Balozi Fatma.

Dokta Asha Rose Migiro, mkuu wa mabalozi 49 wa Tanzania, anasema katika nchi wanazofanyia kazi kuna fursa mbalimbali za kuisaidia Tanzania kuinuka kiuchumi.

Anasema kinamama hivi sasa wanaweza na wakipewa nafasi wanafanya vyema kiasi kwamba mafanikio yake ni makubwa.

Dk. Asha Rose, aliyewahi kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, aliweka historia si kwa Tanzania tu bali hata Afrika na dunia kwa kuwa ni cheo cha mwanzo kupewa mwanamke katika historia ya UN.

Sambamba na nafasi hiyo, lakini Balozi Asha-Rose alikuwa ni miongoni mwa wanawake waliloweka rikodi ya kugombea urais wa Tanzania mwaka 2015.

Balozi mwingine ni Amina Salum Ali, aliyewahi kuwa Balozi wa Umoja wa Afrika (AU) nchini Marekani, anasema wanawake ni lazima wakazane, wasome ili kupata nyadhifa za uongozi.

Aidha Amina na Asha Rose waliwahi kugombea urais wa Tanzania, aidha Amina ameshika nyadhifa mbalimbali za kiserikali ya Zanzibar na ya Muungano na kichama ikiwa ni pamoja na uwaziri kwa vipindi tofauti.

Ni mmoja ya wanawake waliovunja rekodi hapa Zanzibar na Tanzania kwa kuzingatia kuwa ni mwanamama wa mwanzo Zanzibar kuingia jimboni na kugombea nafasi ya uwakilishi katika jimbo la Kwahani na kuchaguliwa kwa kura nyingi kupitia tiketi ya CCM.

Linapotajwa jina la Getrude Mongella, ni mwanawake aliyefanya makubwa kwa Tanzania na kutambulika kimataifa kwenye kuandaa mkutano wa Wanawake wa DUnia huko Beijing China mwaka 1995.

Mama Mongella ni miongoni mwa wanawake wa Tanzania walioionyesha dunia kwamba taifa hili lina wanawake wa shoka.Mongella ni mwanasiasa, mwalimu, mwanaharakati mke, mama na bibi aliyeitangaza vyema Tanzania kimataifa.

Pia Balozi Getrude Mongella ambaye aliwahi kuzungumza na Nipashe anasema kuwa aliiwakilisha vyema nchi katika mkutano wa Beijing na kupata sifa kem kem mwaka 1995.

Mongella aliwahi kuwa Rais wa Kwanza wa Bunge la Afrika (PAP) na anasema alifanya vyema kazi zake. "Miongoni mwa nafasi ambazo sitazisahau katika maisha yangu ni pamoja na kuteuliwa Rais wa PAP ndipo nilipoanza kupata uelewa mkubwa wa shughuli za kimataifa", anakumbuka.

Takwimu zinaonyesha Canada na Uswizi zinaongoza kwa kuteua mabalozi wanawake na wawakilishi wa kudumu mwaka 2022, huku asilimia 50 ya nyadhifa za mabalozi wa nchi zote mbili zikishikiliwa na wanawake.

# Congo inapoteketea M23, waasi kadhaa waibuka upya

•Watu wachinjwa kama nyama, nyumba zikichomwa moto




Vita inaiweka DRC mashakani. Vikosi vya kulinda amani vya Umoja wa Mataifa vikishika doria mashariki mwa nchi hiyo. **PICHA: AFP**

**Na Mwandishi Wetu**

CONGO hakukaliki ni baada ya mapigano mapya, yakihama kutoka kwa waasi wa M23 wanaoshambuliana na majeshi ya serikali, lakini sasa makabila kama Walendu, Wazaire na vikundi vidogo vyenye silaha vinavyodaiwa kushambuliana navyo vinaanzisha mapigano na kuzusha hofu upya.

Hali ilivyo sasa DRC ni kama sikio la kufa ambalo halisikii dawa. Hofu hiyo inatokana na vita vya kila uchao licha ya juhudi za kitaifa na kimataifa kufanyika kuleta amani na uelewano nchini humo.

Wiki iliyopita ilimalizika kwa mapigano makali yaliyoanza Ijumaa mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kati ya waasi wa M23 na makundi hasimu yenye silaha baada ya siku 10 za utulivu, raia na vyanzo vya usalama vinasema.

Makabiliano hayo yanaripotiwa karibu na Bwiza, kilomita 40 au maili 25, kaskazini mwa mji mkuu wa mkoa wa Goma kwenye ngome ya M23 magharibi mwa mji wa Masisi.

Mapigano kama hayo yaliripotiwa kutokea eneo Desemba 6 wakati M23 ilipokubali kusitisha mapigano na jeshi la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na kutangaza kuwa wako tayari kujiondoa katika maeneo ambayo waliyateka hivi karibuni.

> Makabiliano hayo yanaripotiwa karibu na Bwiza, kilomita 40 au maili 25, kaskazini mwa mji mkuu wa mkoa wa Goma kwenye ngome ya M23 magharibi mwa mji wa Masisi.

Hakuna juhudi zozote zilizofanyika za kuacha na kusitisha mapigano na hata kama zipo zimefanyika ni kiasi kidogo, lakini haijumuishi makundi mengine yenye silaha katika eneo hilo, ambayo baadhi yao yanajaribu kusimamisha harakati za M23.

Mapigano yameanza tena karibu huko Bwiza, katika vijiji vya Swagara, Mudugudu na Kabarozi, mkazi wa Bizwa anaiambia AFP kwa njia ya simu. Wanamgambo wa M23 walianzisha mashambulizi kwa nguvu zaidi anaongeza.

Kundi hilo lilitoa taarifa likishutumu muungano wa serikali kwa kukiuka makubaliano ya kusitisha mapigano na kuanza tena kuingia msituni, lakini chanzo cha usalama kilisema kuwa vikosi vya jeshi havihusiki na mapigano kati ya M23 na vikundi vingine vyenye silaha.

Makundi hayo yanajumuisha wafuasi wa Wahutu na Wanyatura na Muungano wa Nyatura and the Patriotic Alliance for a Free and Independent Congo (APCLS), wengi wao wakiwa wapiganaji kutoka kabila la Wahunde wapo katika muungano unaoojitolea kuwazuia na kukabiliana na waasi wa M23.

"Tumewaondoa maadui huko Swagara," msemaji wa APCLS Heritier Ndangendange anasema.

> Mapigano yameanza tena karibu huko Bwiza, katika vijiji vya Swagara, Mudugudu na Kabarozi, mkazi wa Bizwa anaiambia AFP kwa njia ya simu. Wanamgambo wa M23 walianzisha mashambulizi kwa nguvu zaidi anaongeza.

Waasi wa M23, kundi kubwa la Watutsi wa Kongo, walianza tena mapigano mwishoni mwa 2021 baada ya kuishutumu DRC kwa kushindwa kuheshimu makubaliano ya kuwajumuisha wapiganaji wake katika jeshi.

Kundi hilo katika miezi ya hivi karibuni limeteka sehemu ya eneo la Rutshuru karibu na mpaka wa Uganda na Rwanda na kuingia ndani ya kilomita 20 takribani maili 12 kaskazini mwa Goma.

Ujumbe wa Umoja wa Mataifa nchini DRC uligundua kuwa wanaume, wanawake na watoto 131 walipigwa risasi na kufa au kukatwakatwa hadi kufa mwishoni mwa mwezi uliopita kama sehemu ya kulipiza kisasi dhidi ya raia na M23.

DRC inaishutumu nchi jirani ya Rwanda kwa kuwaunga mkono waasi, lakini Rais Paul Kagame anakanusha shutuma hizo.

**VITA VYA KIKABILA**

Wakati huo huo, vikosi visivyoeleweka vimeibuka na kuanza kushambulia, raia na kuanzisha mapigano ya kikabila na kuzusha tena hofu miongoni mwa Wakongo.

Hivi karibuni watoto watano wameripotiwa kuwa miongoni mwa watu 12 walikatiliwa maisha katika kijiji kimoja kaskazini mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Mauaji hayo yanasadikiwa kufanywa na wanamgambo ambao hawakuhudhuria mazungumzo ya hivi karibuni ya amani na kutafuta suluhu ya DRC yaliyofanyika Nairobi na Luanda, ni kwa mujibu wa duru za ndani.

"Wananchi wamechomwa moto wakiwa hai katika nyumba zao, wengine walikatwakatwa kwa mapanga hadi kufa," Joseph Lotoma, kiongozi wa Kijiji cha Walendu Watsi, anasema kufuatia mauaji hayo ya usiku kucha.

Miili ya watoto watano, wanawake watatu na wanaume wanne ilipatikana asubuhi, anasema na kuongeza kuwa mauaji hayo yalifanyika mwishoni mwa wiki iliyopita..

Wengi wa waathiriwa walikuwa kutoka kabila la Lendu, anasema Jean-Marie Ndjaza, msemaji wa jamii za wa Lendu. Wakati huo Lotoma anaeleza kuwa wahusika wa uhalifu huu sio CODECO wanamgambo wanaodai kuwakilisha kabila la Lendu na wanaoshutumiwa kuua raia wengi katika jimbo hilo katika miaka ya hivi karibuni.

Uchunguzi unaendelea, anaongeza lakini inaaminika waliohusika wanaweza kuwa ni "Wazaire", wanamgambo hasimu ambao wanajitambulisha kama kundi la kabila la Wahema la kujilinda na kujihami.

Anasema CODECO iliwakilishwa katika duru ya hivi karibuni ya mazungumzo ya amani mjini Nairobi na makundi kadhaa ya watu wenye silaha yanayofanya kazi mashariki mwa DRC, lakini kundi la Zaire lilikataa mwaliko huo.

Jumuiya ya Walendu iliibua hofu ya kulipizwa kisasi na CODECO.

"Tunatoa wito kwa viongozi wa CODECO kutoingia katika mtego wa maadui zao, kutojibu chokochoko hii," Ndjaza anasema.

***KUTOKA RFI***

UFISADI KATAVI

# Waziri Mkuu anapofichua wizi mabilioni, unyeti habari za uchunguzi unapojitokeza

**Na Michael Eneza**

WATANZANIA wanafahamu kuwa fedha za umma zinaliwa, lakini wanapata uchungu na kunyong'onyezwa zaidi kila mara ufisadi huo unapotangazwa hadharani, ni hivi karibu huko mkoani Katavi Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, anatangaza hadharani tuhuma za wizi wa takriban bilioni tatu za ujenzi wa chuo cha ualimu.

Ni suala linaloibuliwa ndani ya kongamano la hali ya tasnia ya habari nchini ikihojiwa hivi isingewezekana kwa vyombo vya habari kugundua jambo hilo kwenye taarifa za uchunguzi, badala ya kungoja Waziri Mkuu afike huko atangaze ufisadi huo. Haikuwa rahisi kulijibu.

Kwa upande mwingine, kongamano hilo lilichambua mabadiliko katika tasnia hiyo tangu kuanza kwa awamu ya sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, ambako washiriki wanakubali kuna upana wa uhuru wa kukusanya na kutoa habari.

Ila yako maeneo ya dosari ambayo yamebaki, mojawapo likiwa ni kutotaka kutoa habari kwa wale wenye wajibu wa kufanya hivyo.

Halafu kuna vitisho kuashiria hatua za kuchukuliwa kwa chombo cha habari endapo kinachapisha au kutangaza habari ambazo hazifurahishi serikali, idara mojawapo au mamlaka nyingine za umma kuanzia mkoa hata wilaya.

Mazingira ya mabadiliko katika tasnia yalichukua picha ya uhuru uliotolewa bayana na kila mtu anajua hilo, ila kama alivyoeleza Dk. Ayubu Rioba, Mkurugenzi wa Shirika la Utangazaji TBC na mhadhiri mzoefu wa vyuo vya uandishi, kuna tofauti (katika fikra ya uhuru wa kuandika habari). Tena tofauti ipo bayana kati ya kuwa na uhuru na kuutumia.

Anamnukuu mnadharia Isaiah Berlin aliyemulika kwa kina tofauti hiyo, na kuitaja kama hali inayoonekana katika tasnia ya habari hapa nchini hivi sasa. Anaacha maswali katika mkanganyiko huo wa kutumia uhuru wa kuandika ambao umeainishwa katika awamu ya sita ila unalegalega kiuhalisia.

Udhaifu wa mazingira ya uhuru wa kukusanya na kutoa habari yalijadiliwa kwa kina ila yako maeneo ambayo bado hayajaguswa.

Ukiangalia serikali inachosema -na kuainisha katika kongamano hilo hasa kuhusiana na uendeshaji wa tasnia ndogo ya habari za mitandaoni, kinachoonekana zaidi ni mabadiliko ya kanuni au maelekezo ya kuanzisha, kusajili na kuendesha huduma ya habari mtandaoni. Uhuru upo kama inavyosemwa ila inavyoelekea watu hawathubutu kuutumia, au inaonekana kama hawana ari ya kuutumia kikamilifu, hilo likawa likaibuliwa na wanataaluma katika kongamano hilo.

Ukiangalia kwa karibu unakuta kuwa yako maeneo ambayo wachangiaji ni kama hawakutaka kuyagusa, au labda kwa mbali kwa mfano nini kinazuia wengi kati ya wanahabari kutoingia maeneo hayo. Kwa upande mmoja watawala wa tasnia ya habari walijitahidi kuonyesha kuwa utashi unahitajika katika eneo hilo, kwa mfano mkurugenzi huyo wa TBC akisema kuwa taasisi hiyo inaanzisha kitengo cha habari za uchunguzi na kwamba yajayo yanafurahisha

Labda alikuwa na maana ya habari za utafiti kwani unaweza kufanya utafiti na kuja na hoja, majibu au maswali ukakwepa kukiuka kanuni zozote zinazoweza kuleta mgogoro na mamlaka inayoendesha chombo hicho.

Labda kielelezo kinachofaa ni tukio lenyewe la wizi katika ujenzi wa chuo cha ualimu, ambako Waziri Mkuu anasema vitasa viwili vipya vilionekana katika vyumba vya jengo (ambalo ina maana bado linajengwa hivyo hata kuwepo vitasa visivyofanana na hawajavizoea hapo, kulitangulia kuungua kwa vyumba hivyo. Kimojawapo kinasemekana kilitumiwa kuhifadhi nyaraka za ununuzi wa vifaa katika ujenzi huo, na kiongozi huyo wa ngazi ya juu anasema ilikuwepo shaka kuhusu bei za kununua vifaa na kwaba ilikuwa mara tatu ya bei halisi.

Hapo unaona kuwa tatizo halipo katika tasnia ya habari ila utendaji wake unaendana na mazingira ya kijamii yaliyopo, yakitafsiriwa kama 'civic environment' na siyo 'social environment.' Udhaifu wa kina katika mantiki ya jumla ya uraia ndiyo inaleta tatizo la kina la mshikamano, kwani taarifa ya uchunguzi inajikita katika hitaji la kijamii la kusimamia uadilifu katika miradi ya maendeleo.

Mfano hai ni huo ujenzi wa chuo, kuhakikisha gharama ni sahihi kwa kazi inayookenana, jambo ambalo halikuwa sahihi mwanzo na mwisho.

Kabla ya kutafuta kwanini wanahabari wa eneo hilo hawakuandika habari hizo na ikahitajika Waziri Mkuu afike eneo hilo ataje jambo hilo katika mamlaka yake ya kiutendaji, lazima kuanzia hapo mradi ulipo.

Ni ule usemi kwamba 'fadhila huanzia nyumbani,' kwani bado kuna maswali kwanini tatizo lisianze na mkuu wa mkoa, wilaya na TAKUKURU kwa kusimamia na kuondolewa wajenzi siyo mpaka kufika kwa Waziri Mkuu na kuvunja bodi inayosimamia ujenzi na kuagiza watu wakamatwe.

Iweje mkuu wa wilaya asifanye kazi hiyo, au hata mkuu wa mkoa, ashindwe pia? Kinachoonekana ni kuwa tatizo hilo lilikuwa linajulikana ila likaunganishwa na ziara ya Waziri Mkuu katika mkoa huo, na kwa maana hiyo shangwe au sifa inarudi serikalini kwa kupambana na rushwa au wizi wa mali ya umma.

Jitihada hiyo inakuwa halali pale inapofanywa na wakuu wa nchi wenyewe, watendaji wa ngazi za juu na hasa Waziri Mkuu, au wakati wa awamu ya tano kazi ya kutumbua ikifanywa na JPM-John Magufuli, aliyekuwa anahoji kinachotokea kokote anapofika kukagua au hata akiwa ni mpitaji kama kufika uwanja wa ndege na kuhoji kama mitambo ya ukaguzi inafanya kazi ipasavyo.

Mwelekeo huo bado upo, anayeweza kusema ni yule mkuu tu hasa mwenye mamlaka kikamilifu .

Unaweza kujiuliza tumefikaje hapo, na jibu ni hali ya kisiasa ya mwaka 2015 na jinsi ambavyo dhamira hazijabadilika. Walio na madaraka maeneo tofauti wanategeana na serikali katika kufanya masuala yanayowanufaisha na kimsingi ni Rais Samia ambaye anajitahidi kuwazuia kurudi katika mifumo ya awali ya bajeti. JPM akiingia madarakani Desemba 2015 asilimia 74 ya bajeti ilikuwa ya matumizi ya kawaida na asilimia 26 ndiyo ya maendeleo, ubadhirifu ukitawala huko pia. Barabara za mitaani zinajengwa na hakuna pa kupitisha maji ya mvua, au kuna mitaro ya panya.

Alibadili matumizi na kuifikisha kuwa asilimia 61 akiondoa asilimia 13 ya bajeti kutoka matumizi ya kawaida kuja kwenye maendeleo, hali iliyowatesa baadhi ya wakubwa.

Rais Samia alifuata nyayo za JPM na kufuta sherehe za miaka 61 ya Uhuru na kuhamishia Shilingi milioni 960 za Uhuru na kufuta sherehe ili fedha za matumizi zijenge mabweni ya shule za wanafunzi wenye mahtaji maalumu.

JPM alifuta sherehe kama hizo mwaka 2015 akaokoa Shilingi bilioni 4.5 zitumike Dar kupanua barabara ya Morocco hadi Mwenge jijini Dar es Salaam.

Ni kielelezo cha mabadiliko chanya katika matumizi ya fedha za umma kwenye sherehe na watendaji hawafurahishwi na hilo.

Ukichunguza tuhuma wizi hazichapishwi kokote kwa vile ni kuipaka matope serikali au kuleta chuki ya wanachi dhidi ya serikali yao? Uandishi wa kiuchunguzi wa habari hizo utawezekana leo kweli? Ndiyo mshikamano leo.



Baadhi ya wanahabari washiriki wa Kongamano la Habari lililofanyika Dar es Salaam mwishoni mwa wiki . **PICHA: JUMANNE JUMA**

# 2022 mwaka juhudi za kurahisisha uwekezaji sekta nyeti unapochanua




Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Stergomena Tax, (katikati), akishiriki kwenye uzinduzi wa mfumo wa taarifa za uwekezaji. **PICHA: MAULID MBAGA**

**Na Maulid Mmbaga**

TAARIFA za uwekezaji kuanzia kile unachotaka kufanya kwenye sekta za kilimo, nishati, elimu, utalii na miundombinu zimewekwa bayana ili kuvutia wawekeza wa nje na ndani.

Zipo kwenye mfumo mahususi wenye habari za masoko unaolenga kuwanufaisha wawekezaji ili kung'amua na kuamua fursa za uwekezaji na aina za biashara zilizopo Tanzania, anasema Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe.

Ni wakati wa uzinduzi wa mfumo huo, unaofanyika jijini Dar es Salaam, ikibainishwa kuwa mfumo unaandaliwa kwa ushirikiano wa serikali, Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Maendeleo (UNDP), Kituo cha Uwekezaji (TIC) na Mfuko wa Maendeleo ya Mitaji wa Umoja wa Mataifa (UNCDF).

Anakumbusha kuwa moja ya changamoto taifa lililokuwa nazo kwa wawekezaji wa ndani na nje ni namna ya kupata taarifa kwa urahisi na kwa usahihi.

Anasema hayo wakati wa kuzindua mfumo huo akiongeza kuwa utafanikisha upatikanaji wa taarifa kwa mwekezaji kokote alipo kuona fursa zilizopo nchini, na kwamba teknolojia hiyo haina masharti kwa atakayehitaji kuitumia, huku akitoa wito kwa Watanzania kuchangamkia fursa hiyo.

Anaeleza kuwa program ina taarifa za sekta tano zikiwamo za kilimo, afya na miundombinu, anaongeza:"Watanzania chukueni nafasi hii, tunapoendelea kutengeneza mazingira wezeshi ya uwekezaji na kufanya biashara, tunaamini wawekezaji ambao ni endelevu na makini ni wa ndani," anasema.

Kigahe anakanusha madai kuwa Ijuhudi hizo zinafanywa kwa ajili ya wawekezaji wa nje akisema serikali anawalenga Watanzania washiriki ndiyo maana wanapofanya shughuli hizo wadau mbalimbali wapo.

Pia anabainisha kwamba mfumo uliozinduliwa utakuwa na taarifa za sekta tano zenye fursa za uwezaji ikiwemo kilimo, nishati, elimu, utalii na miundombinu, na kwamba tayari wamerekebisha sera na miongozo itakayowezesha wawekezaji kufikia malengo yo.

Anasema ziko sekta nyingi lakini wameamua kuanza na tano ambazo UNDP wanashiriki kupitia mfumo huo, na kwamba vitu muhimu wanavyovifanya ni kuhuisha sera sekta ya uwekezaji.

Anataja sera zote zinazohusika na mfumo huo kuwa ni pamoja na ya biashara, uwekezaji na viwanda na kwamba zinahuishwa ili waziwekee mikakati mipya kuendana na maboresho ya mifumo mbalimbali inayofanywa.

"Katika bunge lililopita tumepitisha sheria mpya ya uwekezaji. Huu ni utekelezaji wa sera mpya tunazozihuisha ili ziendane na hatua au maboresho yanayofanywa na serikali, sheria hiyo tunaamini itatusaidia kwasababu imepunguza masharti magumu," anasema Kigahe.

"Uziduzi wa ramani ya mwekezaji wa malengo ya maendleo endelevu unaweza kusanifisha ushiriki wa sekta binafsi katika kusaidia uwekezaji endelevu nchini, pia maendeleo ya njia hii yatategemea mahusiano imara kati ya serikali, sekta ya fedha, masoko ya mitaji na Umoja wa Mtaifa (UN)," anasema Kigahe.

**FAIDA ZA MFUMO**

Mwakilishi Mkazi wa UNDP Christine Musisi, anasema kutoa na kuonyesha fursa za masoko kupitia mfumo huo kwa wawekezaji wanaotaka si tu kupata faida, lakini pia ni kubainisha mahitaji ya wawekezaji na kutoa taarifa za masoko zinazoendana na uwekezaji kwa kuunganisha mahitaji ya maendeleo na fursa za uwekezaji.

Mfumo huo utasaidia kuendeleza malengo ya maendeleo endelevu na mafanikio ya mpango wa tatu wa maendeleo ya taifa wa miaka mitano (FYDP III), anasema Christine..

Anaongeza kuwa umeanzisha maeneo 13 ya fursa za uwekezaji pamoja na mifano ya biashara yenye tija na takwimu zinazojitosheleza, ambazo zinaweza kuwaongoza wawekezaji na shughuli za biashara zitakazofanya maisha ya Watanzania na dunia kuwa tofauti.

"Sekta tano za vipaumbele zilizobainishwa zinatoa fursa kwa muungano wa kikanda kwa njia ya fursa za mnyororo wa thamani inayojitokeza kwenye uamuzi wa biashara inayoweza kufanywa katika Eneo la Biashara Huria katika Bara la Afrika (AfCFTA)," anasema Christine.

Anaongeza kuwa UNDP inasaidia na kufanya kazi pamoja na serikali kwa miaka kadhaa sasa katika kutangaza uwekezaji nchini, na kwamba maeneo matano ya uwekezaji yaliyobainishwa yatakuwa na faida kubwa kwa wawekezaji wa ndani na nje na taifa kwa ujumla.

"Tunaona Tanzania inakuwa kwa haraka, tunahitaji kuona wanawake, vijana na watu wazima wote kwa pamoja tukishirikiana katika kuleta maendeleo, hivyo tunashukuru wizara, Kituo cha Uwekezaji na wadau kwenye uwekezaji, tutaendeleza ushirikiano wetu," anaongeza Christine.

**MALENGO YA SERIKALI**

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Stergomena Tax, anasema serikali inalenga kurahisisha uwekezaji, ili wanapotaka kuziona fursa zilizopo nchini wazipate kwa urahisi kupitia mfumo huo.

"Ili tuweze kuzitumia fursa hizi tushirikiane na UNDP ili kuhakikisha kwamba fursa hizi zinawekwa bayana na mwekezaji anaweza kuzitumia, kwa kufanya hivyo tutaongeza uwekezaji ili kujiletea maendeleo na kuondoa umaskini," anasema Stergomena.

**UWEKEZAJI ENDELEVU**

Miongoni mwa uwekezaji mkubwa unaoendelea kufanyika nchini unatekelezwa Kibaha mkoani Pwani, na kampuni ya Sino Tan, inatarajia kujenga zaidi ya viwanda 200, ambavyo vitatoa fursa kwa wadau wa ndani na nje kuwekeza na kuzalisha bidhaa mbalimbali.

Mhandishi na mratibu wa mradi huo Alexander Nchaholil, anasema kazi iko katika eneo lenye ukubwa wa ekari 2,500, na kwamba utatekelezwa kwa awamu mbili, ambapo ya kwanza inachukua miaka miwili na ya pili miaka mitatu, akibainisha kuwa wanategemea utakapokamilika utakuwa na ajira takribani 100,000.

Anasema baada ya viwanda hivyo kukamilika wanategemea pia kutakuwa na kipato cha takribani dola bilioni sita kwa mwaka.

"Tunashirikiana kwa karibu na serikali, kwasababu haya yote kuyakamilisha tunahitaji miundombinu ifike hapa, na Sino Tan tunashukuru kuna umeme, maji, miundombinu kama barabara tayari inaendelea kuja," anasema Nchaholul.

Pia anabainisha kuwa mpaka sasa viwanda ambavyo tayari wameshasaini utekelezaji ni zaidi ya 70, na kwamba mpaka Juni 2023 wanategemea viwanda vitano vitafanya kazi.

Sino Tan itajenga ofisi za serikali makazi na kuzalisha bidhaa mbalimbali na kwamba endapo mfanyabiashara atahitaji kuagiza nje atafanya hivyo akiwa hapa na shehena kutoka nje ikiletwa, itafikia kwao na hakutakuwa na haja ya kwenda bandarini.

**SAUTI ZA WADAU**

Mchumi kutoka Gabon- Afrika ya Kati, Jeff Megola, akizungumzia juu ya uwekezaji huo, anasema ni mkubwa na kuusifia kuwa hawakuutegemea kuukuta Tanzania.

"Sisi Gabon pamoja na serikali pia tunajaribu kupata aina kama hii ya uwekezaji, Sino Tan wamefanya kitu kikubwa na kama Afrika tutachukua mfano wa uwekezaji huu," anasema Megola.

Mwakilishi kutoka Kampuni ya 'Smart Solar' ya Uturuki, Kaan Ozkan, anasema Tanzania ni moja ya maeneo yenye miradi mikubwa ya kuzalisha umeme kwa kutumia sola au umeme jua, akiahidi kwamba watawekeza katika nishati hiyo ili kuwezesha kila mwananchi kufikiwa na huduma hiyo.

Samuel Ndonga, Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Samawat Capital Partners ya Kenya, anasema wanajihusisha na uwekezaji katika sekta ya kilimo, umeme, afya na elimu, na kwamba wako nchini kutimiza lengo hilo.

"Uwekezaji wa Sino Tan utakuwa na 'matokeo makubwa, hivyo tunategemea mradi huu umalizike kwanza maeneo ya viwanda ndiyo tuanze kuongea na kampuni ambazo zitapenda kutumia fursa zilizopo," anasema Ndonga.

# MLUNGULA KOMBE LA DUNIA ULIVYOBOMOA BUNGE ULAYA

## •Kigogo aliyehongwa avuliwa uanachama, atumbuliwa EU

**Na Gaudensia Mngumi**

WAKATI Mabingwa wa Kombe la Dunia 2022 ni Argentina, kwa upande mwingine maandalizi ya kombe hilo yameliachia kilio Bunge la Umoja wa Ulaya (EU).

Kinachoufunga mwaka 2022 EU ni kesi kubwa ya ufisadi inayodaiwa kuwa Qatar iliyoandaa kombe la dunia lililomalizika Jumapili iliyopita , imewahonga wabunge wa Ulaya ili kushawishi kupindisha ukweli wa tuhuma zilizowanga .

Ufisadi unaolitikisa Bunge la Ulaya, umemgusa Makamu Mwenyekiti wake Eva Kaili (44) miongoni mwa wabunge na sasa waendesha mashtaka wa polisi wa shirikisho wa Ubelgiji wanasema waliwakamata na kuwafungulia mashtaka watuhumiwa wanne kufikia wiki iliyopita kwenye kesi ya rushwa, utakatishaji fedha na kushirikiana kula njama na kuhusika katika uhalifu.

Wanadaiwa kufanya hivyo kwa niaba ya "Nchi ya Ghuba," ambayo vyombo vya habari vya Ubelgiji na baadhi ya wajumbe wa Bunge la Ulaya wametambua kuwa ni Qatar, licha ya kwamba, haijatajwa moja kwa moja. Miongoni mwa wanaopandishwa kizimbani ni mbunge wa Ugiriki Eva Kaili .

Baada ya kupanda ngazi na kupata uungwaji mkono alikuwa mmoja kati ya Makamu wa Rais 14 wa Rais wa Bunge la E.U.

Kwa kutikiswa na kashfa hiyo, wabunge wa Ulaya walimvua Eva wadhifa wake kama makamu wa rais , na baadhi ya wafanyakazi wenzake pia walisema anapaswa kujiondoa kama mbunge huku chama cha Kisoshalisti cha Ugiriki cha PASOK anachowakilisha kikimvua uanachama.

Maofisa wa mahakama wanasema Eva ataendelea kukaa rumande kwa siku kadhaa baada ya hakimu kuahirisha kusikiliza kesi yake.

Bunge la Ulaya lilipiga kura 625 kwa moja kumvua Eva jukumu lake kwa madai hayo, akidaiwa kuhusika katika kashfa ya hongo.

Ofisi ya mwendesha mashtaka wa serikali inasema "inashukiwa kuwa vyama na viongozi katika nyadhifa za kisiasa tena kimkakati ndani ya Bunge la Ulaya wamelipwa kiasi kikubwa cha pesa au wamepewa zawadi kubwa ili kubadilisha maamuzi ya Bunge la EU," taarifa inasema.

Hivi karibuni polisi wa Ubelgiji walivamia takribani nyumba 20 na ofisi za bunge, na kukamata Yuro € 1.5 milioni sawa na Dola 1.6 milioni taslimu pamoja na kompyuta na simu. Dola hizo ni sawa na Shilingi 3,736,030,400 (bilioni 3.8).

Vyama vya kisiasa ambavyo Eva alikuwa mwanachama wake vilichukua hatua za haraka kujibu uchunguzi huo; amesimamishwa kazi na chama cha Ugiriki cha PASOK-MOVEMENT FOR CHANGE pamoja na kundi la E.U la Socialists and Democrats. Ugiriki pia imezuia mali ya familia ya Kaili kusaidia kujua ukweli.



Eva Kaili, anayedaiwa 'kushikwa mkono' na Qatar kuzima madai ya serikali yake, kunyanyasa wafanyakazi wahamiaji, kwenye Bunge la EU. **PICHA: RFI**

### EU YAJIBU

Ofisa Mkuu wa E.U, Ursula von der Leyen, anaonyesha "wasiwasi mkubwa" juu ya madai hayo Jumatatu. "Ujasiri na uaminifu katika taasisi zetu unahitaji kutazamwa kwa viwango vya juu zaidi vya uhuru na uadilifu," anasema Ursula, katika mkutano na waandishi wa habari na kutoa wito wa kuundwa kwa chombo huru cha maadili kuchunguza ili kuujua ukweli.

"Hii itaingia katika historia kama moja ya ukiukwaji mkubwa na wa kushangaza zaidi labda kashfa kubwa zaidi katika siasa za Ulaya, ambayo kwa matumaini itazua hisia kutoka kwa viongozi wa kisiasa katika kushinikiza mageuzi," anasema Alberto Alemanno, profesa wa chuo kikuu cha Sheria cha Umoja wa Ulaya jijini Paris na mwanzilishi wa The Good Lobby, shirika lisilo la kiserikali linalojitolea kufuatilia kuwapo kwa mamlaka kiusawa katika kutunga sera za Ulaya.

### BUNGE LAKOSOLEWA

Anasema Umoja wa Ulaya una taasisi tatu kuu zinazounda sheria, ikiwa ni pamoja na Bunge, Baraza la Umoja wa Ulaya, na Tume ya Ulaya. "Kiungo dhaifu zaidi katika mfumo wa uadilifu wa EU ni Bunge la Ulaya,ina ukaguzi na udhibiti mdogo ikilinganishwa na taasisi nyingine," Profesa Alemanno anasema na kuongeza:"Hakuna mtu aliyewajibishwa kwa kutoripoti mambo ya mikutano, mchango au zawadi anazopewa, kwa hivyo huu ni utamaduni wa kutokujali mambo ambao umeenea katika Bunge la Ulaya na hilo linathibitika sasa ."

Alemanno anasema kashfa hiyo ni "kuiamsha E.U na imani inaweza kupotea katika taasisi hiyo, haiwezi kusimama kifuambele tena kwani inaonekana dhaifu kwa ufisadi na nchi ambazo E.U, anaziadhibu hadharani; kuna mashaka 'doble standard' yanayojitokeza."

### HATMA YA QATAR

Uchunguzi wa maofisa wa Ubelgiji unakuja wakati Kombe la Dunia la Qatar limehitimishwa wiki ikiwa ni nchi inayokabiliwa na ukosoaji kuhusu mazoea ya unyanyasaji mbaya wa wafanyikazi wahamiaji.

"Inadhoofisha uaminifu wa watumisha hao na inafanya iwe vigumu kuamini na kuthibitisha kwamba wamefanya jambo ambalo linasonga mbele haki za wafanyakazi," anasema Philip Nichols, profesa katika Chuo Kikuu cha Pennsylvania nchini Marekani na mtaalamu wa rushwa.

Kashfa ya ufisadi inakuja wakati Bunge la E.U lilikuwa linafikiria Qatar kusafiri bila visa kwa Ukanda wa Schengen wa Umoja wa Ulaya."Usafiri bila visa kwenda Ukanda wa Schengen unahusu uaminifu. Kile ambacho Qatar imefanya kimedhoofisha sana juhudi za kuunda usafiri bila visa."

Aidha, Bunge la Ulaya limesitisha kazi yake na Qatar. Kura ya kukaa bila visa katika Ukanda wa Schengen kwa Qatar imeahirishwa.

Qatar anakanusha shutuma za utovu wa nidhamu katika tuhuma hizo kupitia ujumbe wake wa Twitter wa wiki iliyopita kutoka kwa Wizara ya Mambo ya Nje, akisema:"Uhusiano wowote wa serikali ya Qatar na madai yaliyoripotiwa hauna msingi na upotoshaji mkubwa."

Hapo awali mshitakiwa Kaili alielezea kuunga mkono Qatar kabla ya Kombe la Dunia.

"Qatar iko mstari wa mbele katika kulinda haki za wafanyakazi na kupunguza kima cha chini cha mshahara," anasema Eva katika hotuba ya Novemba mbele ya Bunge la Ulaya, wakati wabunge walikuwa wakijadili haki za binadamu katika muktadha wa Kombe la Dunia. Wakati akisema hayo kulikuwa na madai kuwa Qatar inanyanyasa wafanyakazi wahamiaji waliokuwa wanapigia simu kueleza kuwa inawabagua. Wanawaonea na wanamtuhumu kila anayezungumza nao au kujihusisha na ufisadi.

# UWT yatamani kiwepo kigoda kumuenzi, hakuwa msomi, ila amefanya maajabu

INATOKA UK. 13

kuongoza Tanzania," anasema.

Anawaambia washiriki kuwa UWT ianze kuhimiza wanawake kufuata nyayo hizo kwa kuacha kusubiri kuwezeshwa, bali wajiamini, kujituma na kuonyesha uwezo walionao ili wasifike mbali bila msukumo wowote kutoka nje.

"Kama ambavyo Bibi Titi alipigania usawa katika kujenga uzalendo Tanganyika, ndivyo nyakati hizi tunaona Rais akitanguliza ajenda ya usawa ndani ya CCM, tuunge mkono nyayo hizo," anasema.

**USHUJA SI ELIMU**

Profesa Aldin Mutembei kutoka Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, anasema alipofuatilia historia ya maisha ya Bibi Titi, anagundua kuwa mwanasiasa huyo anafundisha jamii jambo moja kubwa, kwamba siyo lazima awe msomi mkubwa ndipo aweze kutenda jambo.

"Elimu ni dhana pana huyo Bibi Titi alikuwa na elimu hata zaidi ya maprofesa, kwa sababu mambo aliyoyatenda yalikuwa ni makubwa, alikuwa mwanaharakati, mwanasiasa lakini pia msanii," Prof. Mutembei anasema.

Aidha, anaeleza kuwa kila mahali ambapo Mwalimu Nyerere alikwenda kuhutubia, Bibi Titi alikuwa nyuma yake na kwamba kabla ya hotuba, Mwalimu alimuita kuimba wimbo wa kuvutia watu kama mtu anayesafisha njia.

"Bibi Titi alitetea umma wa wanyonge miongoni mwa wanajamii, ndio maana Mwalimu Nyerere alimweka katika nafasi mbalimbali ikiwamo uwaziri wa mambo ya jinsia na alifanya mengi kwa ajili ya Watanzania," anasema.



Halima Mzee mtoto wa Bibi Titi. **PICHA: CCM**

> "Kama ambavyo Bibi Titi alipigania usawa katika kujenga uzalendo Tanganyika, ndivyo nyakati hizi tunaona Rais akitanguliza ajenda ya usawa ndani ya CCM, tuunge mkono nyayo hizo," anasema.

Halimza Mzee ambaye ni mtoto pekee wa Bibi Titi, anasema mama yake alikuwa na hofu ya Mungu, na kwamba kwa hatua hiyo alimwezesha kila alilofanya akawa anatanguliza maslahi ya wengi.

"Wengi hamjui Bibi Titi alikuwa wa aina gani. Ukweli ni kwamba alikuwa na hofu ya Mungu kwa yale aliokuwa akifanya, kwani alitanguliza mbele na maendeleo ya wengi katika maisha yake," anasema Halima.

Mwanasiasa Kate Kamba anasema Bibi Titi ataendelea kukumbukwa na kuenziwa kutokana na jinsia ambavyo alikuwa hodari na shupavu katika kupigania taifa wakati wa ukoloni.

NDIYE BIBI TITI

Mwaka 1926, alizaliwa akiwa mmoja wa wanawake wa kwanza wazalendo kushika nafasi za ubunge na uwaziri na pia alikuwa kati ya kinamama wa kwanza kujiunga na harakati za kupigania uhuru wa Tanganyika.

Mwaka wa 1991, wakati Tanzania ikisherekea miaka 30 ya uhuru, jina la Bibi Titi lilionekana kwenye maandishi ya CCM, yakisomeka; 'Shujaa wa Kike Aliyepigania Uhuru'.

Aidha, moja ya barabara za jijini la Dar es Salaam ina jina lake, kutokana na heshima aliyopewa kwa kushiriki katika harakati za kutafuta uhuru wa Tanganyika kwa mafanikio makubwa.

Novemba 5, 2000 Bibi Titi, alifariki dunia katika Hospitali ya Net Care jijini Johannesburg Afrika Kusini.


Ameacha alama za ushujaa, uthubutu, umahiri na ujasiri ambazo UWT inaahidi kuzifuata.

## CHEMSHABONGO NA -00 33 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com


Dondoo: Kulia
1. Fisi
7. mwanadamu wa kwanza
8. ugwe
9. feki
10.kiunganishi katika tungo kinachoashiria majuto
12.neno la kutilia mkazo
13.mmea mkubwa ambao hutoa mbao na kuni
15.bainika
16.chukua bila idhini ya mwenye mali 17.sifuri 18.chombo cha majini

Chini:
1. kifungo cha kufungia mkanda wa nguo
2. karo ya shule
3. mahali unapopumzika msafara
4. fuatana
5. Pesa ya China
6. Kale
11.maisha ya starehe
13.humsaidia mnyama kufukuza wadudu 14.shida




Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

MKATABA
MWANGAZA
AMERIKA
AJENDA
GIDAMU
ALAMA
ALIKWA
MITAA
KAUKIA
ATIA: ADA:
MAANA, WANA
NJAA : UFA
AMI




maoni SMS: 0787 00 97 94

Majibu toleo lililopita








# Polisi yataka wananchi kutoa taarifa matukio ya kihalifu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, limewataka wananchi kutoa taarifa dhidi ya matukio ya uhalifu na likiwaondoa hofu kuwa linazo mbinu za kuwalinda na kutunza siri za watoa taarifa dhidi ya matukio hayo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga, aliyasema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya sikukuu za mwisho wa mwaka.

Kamanda Kuzaga alisema baadhi ya wananchi wanashindwa kuripoti matukio ya uhalifu kwa kuhofia kutambulika na wahalifu hao, hivyo akawahakikishia kuwa taarifa hizo zitakuwa za siri.

"Kwa sasa kuna askari kata, tumewaweka huko kwa makusudi ya kurahisisha utoaji wa taarifa, mwananchi halazimiki kuja kutoa taarifa huku kwetu na badala yake anatoa hukohuko kwenye kata yake," alisema Kamanda Kuzaga.

Aidha, alisema jeshi hilo limeanza maandalizi ya kukabiliana na uhalifu wakati wa sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya ili kukabiliana na matukio ambayo yamekuwa yakijitokeza msimu wa sikukuu za mwishoni mwa mwaka.

Aliwataka wananchi kutokuwa na hofu ya kutendeka uhalifu wa aina yoyote ndani ya mkoa huo kwa maelezo kuwa jeshi lake limejipanga kudhibiti wahalifu wote.

Alisema ili kufanikisha jambo hilo wananchi wanatakiwa kushirikiana kwa kila namna na jeshi hilo kwa kutoa taarifa za mapema dhidi ya matukio ya uhalifu kwa jeshi hilo ama kwa viongozi wa serikali.

"Tumeanza kufanya doria mapema katika maeneo yetu yote ya mkoa tumepeleka askari wa kutosha huko ili kubaini matukio ya uhalifu kabla hayajajitokeza," alisema Kuzaga.

Alisema watakuwapo askari wenye sare na ambao watakuwa wamevalia kiraia ili kudhibiti matukio ya aina yoyote yatakayotokea kwenye makazi ya wananchi.

# TAKUKURU yathibitisha M-NEC kuhusika rushwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Tanzania (TAKUKURU) imethibitisha mmoja wa wagombea wa nafasi ya Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC), Mkoa wa Mbeya, kuhusika na vitendo vya rushwa.

Novemba 21, mwaka huu ilikuwa siku ya uchaguzi wa kumpata mgombea wa nafasi ya Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (MNEC), lakini Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi CCM, Daniel Chongolo, alitangaza kuahirisha uchaguzi huo kwa Mkoa wa Mbeya.

Miongoni mwa sababu alizoziainisha Chongolo ni mchakato wa uchaguzi huo kugubikwa na rushwa na kuwalazimu kuahirisha uchaguzi mpaka uchunguzi utakapofanyika kubaini ukweli wa jambo hilo ambalo lilikabidhiwa kwa vyombo vya sheria.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Mbeya, Maghela Ndimbo, alitoa kauli hiyo juzi alipozungumza na wanahabari kuhusu utekelezaji wa shughuli hizo katika kipindi cha robo tatu ya mwaka.

Alisema TAKUKURU ilishiriki na kufuatilia kwa karibu mchakato wote wa uchaguzi kuanzia ngazi ya kata mpaka mkoa na kubaini baadhi ya dosari.

"Tulibaini mmoja wa wagombea wa nafasi ya NEC kuhusika na vitendo vya rushwa, hivyo tukakishauri chama kumwondoa mgombea huyo kushiriki mchakato wa uchaguzi.

"Kwa kutumia kitengo chetu cha Intelijensia tulibaini alikuwa anakusanya watu nyumbani kwake na kugawa fedha kama nauli kitendo ambacho kilikuwa kinyume cha taratibu za chama," alisema Ndimbo.

Pia walifanikiwa kuzuia baadhi ya fedha ambazo tayari zilikuwa kwa wakala wake ili kuwatumia wajumbe ambao aliwaandaa kwa ajili ya kuwagawia fedha hizo.

"Tumekamilisha kazi yetu na taarifa ya uchunguzi na ushahidi tumepeleka kwa viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria na nidhamu," alisema Ndimbo.



Mkuu wa Wilaya ya Momba, Fakir Luandala na Meneja wa Kanda wa Hifadhi ya Chakula, Eva Kwavava, wakikabidhi mahindi yatakayogawanywa kwa kaya 105 zilizokumbwa na maafa ya kubomolewa nyumba zao baada ya mvua iliyoambatana na upepo mkali katika Kata ya Chilulumo na Ivuna wilayani humo hivi karibuni. **PICHA: IBRAHIM YASINI**

# Jiji la Mbeya ladaiwa kukithiri kwa uchafu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

HALI ya usafi wa mazingira katika Jiji la Mbeya hairidhishi na kutishia kuibuka kwa magonjwa ya mlipuko kwa wakazi wa jiji hilo katika kipindi hiki cha kuelekea msimu wa mvua.

Akizungumza kwenye kikao cha Kamati ya Ushauri ya Wilaya ya Mbeya, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua alisema kwa sasa mitaa ya Jiji Mbeya na baadhi ya maeneo ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya yamekithiri kwa uchafu, hali ambayo inahatarisha afya ya wakazi wa jiji hilo.

"Mitaa yetu ya Jiji la Mbeya na hata baadhi ya maeneo ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kama vile mji wa Mbalizi, hali ya usafi sio ya kuridhisha, kuna taka nyingi mitaani na nyingine zimejazana kwenye madampo haziondolewi kwa wakati, hali inaweza kutusababishia shida kubwa ya magonjwa ya mlipuko katika kipindi cha mvua tunachoelekea," Dk. alisema Chuachua.

Alizielekeza Halmashauri za Wilaya na Jiji kuchukua hatua za haraka za kusafisha mitaa na kuondoa taka hizo ili kuleta mwonekano mzuri wa madhari ya Jiji. Akizungumzia sababu za kukwama kufanya usafi kwa wakati katika halmashauri yake, Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, Triphonia Kisiga, alisema wanakabiliwa na upungufu mkubwa wa watumishi hasa maofisa watendaji wa mitaa ambao ndio wanaosimamia usafi kwenye maeneo yao.

"Sisi Halmashauri ya Jiji tuna changamoto ya uhaba wa watumishi, upungufu mkubwa upo kwenye kada ya watendaji wa mitaa ambao ndio wasimamizi wa kwanza wa suala la usafi," alisema Kisiga.

Hata hivyo, Kisiga alisema kwa kuwatumia watendaji wachache walioko watajitahidi kushughulikia suala la usafi ili kuhakikisha mazingira yanakuwa katika hali nzuri.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Steven Katemba, alisema ukosefu wa rasilimali fedha ni kikwazo katika kufanikisha suala la usafi.

Katemba alisema kwa sasa wanaelekeza nguvu katika kukusanya mapato ya maegesho katika mji mdogo wa Mbalizi ili yatumike kuboresha hali ya usafi katika mji huo.

"Naomba niwakumbushe kuwa suala la ukusanyaji wa mapato ya maegesho limeshatolewa kwa Wakala wa Brabara za Mjini na Vijiji (TARURA) na sasa linasimamiwa na halmashauri, hivyo katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi ushuru huo tunaukusanya sisi na fedha tunazopata tutazitumia kwa ajili ya kufanya usafi," alisema Katemba.

Alisisitiza kwa wananchi wanaopata changamoto ya maegesho katika mji mdogo wa Mbalizi kuwasiliana na maofisa wa Halmashauri badala ya TARURA, huku akidai kuwa ukusanyaji wa ushuru huo unafanyika kistaarabu bila kumwondolea mtu utu wake kama ilivyokuwa siku za nyuma.

Wakichangia mada mbalimbali, baadhi ya wadau walieleza kero zinazowakabili wananchi na kutaka zitafutiwe ufumbuzi.

Mwakilishi wa Vyama vya Siasa, John David Mwambigija, alisema suala la kukatika katika umeme kila wakati na mgawo unaoendelea kwa wakazi wa mkoa wa Mbeya limekuwa ni kero kwa wananchi na baadhi yao linawaingiza hasara kubwa.

Alisema kuna wananchi wanaopata hasara kwa kushindwa kufanya kazi zao zinazotegemea nishati ya umeme na wengine wanapata hasara kwa vitu vyao kuungua kutokana na kukatika katika ovyo kwa umeme.

"TANESCO naamini mpo hapa, angalieni namna mnavyokata umeme ovyo mnawaingizia hasara wananchi, ni vizuri kama kuna upungufu wa umeme mkaandaa ratiba ya mgawo na kuifuata ili wananchi waelewe kinachoendelea kwa lengo la kuwaepusha na hasara wanayoipata," alisema Mwambigija.

Kwa upande wake Mwakilishi wa Viongozi wa Mila, Chifu Rocket Mwashinga, alisema serikali ishirikiane na wananchi katika kukomesha uharibifu wa mazingira ambao umesababisha athari kubwa za mabadiliko ya tabianchi.

Alisema kwa sasa uharibifu wa mazingira umeongezeka hali ambayo inasababisha matatizo mengi kwa wananchi ikiwamo majanga ya asili kama vile ukame wa muda mrefu.



HABARI DODOMA

# Serikali yashauriwa kujumuisha masuala jinsia kwenye bajeti zake

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imeshauriwa kujumuisha masuala ya kijinsia kwenye mipango na bajeti zake ili kuhakikisha hakuna kundi linaloachwa nyuma.

Mchambuzi na mtafiti wa masuala ya kijinsia kutoka Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Dk. Geofrey Chambaua, alitoa ushauri huo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kufungwa kikao cha masuala ya usawa wa kijinsia jijini hapo.

Kikao hicho kilijumuisha wadau kutoka wizara za kisekta kujadili umuhimu wa serikali kujumuisha masuala ya kijinsia kwenye mipango na bajeti zake.

Dk. Chambua, alisema serikali inapaswa kuhakikisha kuwa hakuna kundi linaachwa nyuma katika masuala ya usawa wa kijinsia.

"Watendaji wa serikali wanapoandika mipango ama bajeti zao wanapaswa kuzingatia masuala ya usawa wa kijinsia na mpango elekezi wa taifa kuzingatia usawa wa kijinsia na makundi yote yanaweza kuzingatiwa na kuwajibishwa," alisema.

Aidha, alisema kama serikali itazingatia usawa wa kijinsia kwa kutenga bajeti ya maji kutawezesha kumpunguzia mwanamke kutumia muda mwingi kufuata huduma hiyo umbali mrefu.

"Zikiwamo bajeti za kutosha kwenye ujenzi wa vituo vya afya na ununuzi wa vifaa tiba kutasaidia kupunguza vifo vya wajawazito na watoto chini ya miaka mitano," alisema.

Kwa mtazamo wake anaona hivi sasa kumekuwapo uelewa wa masuala ya kijinsia katika jamii na kutoa wito kwa serikali kuendelea kusaidia kukua kwa mwelekeo huo.

"Wizara zimekuwa na mipango mingi mizuri kuhusu masuala haya ya usawa wa kijinsia, lakini tatizo tulilonalo kama taifa ni utekelezaji," alisema.

Mussa Mnyeti mmoja wa washiriki wa kikao hicho kutoka Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, alisema wanavyo vipengele ambavyo vipo kwenye sera kwa ajili ya kutetea haki za mtoto katika masuala ya kijinsia.

"Wizara ya Elimu ina sera ya kumlinda mtoto, lakini zipo sheria zinatumika kuwaadabisha watu wote wanaofanya vitendo vya kuvunja haki za mtoto katika masuala ya kijinsia lakini wadau, wananchi hatuna budi ya kulinda usawa wa kijinsia kwa watoto," alisema Mnyeti.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene (kushoto), akimkabidhi Mwenyekiti wa Kijiji cha Kisima wilayani Mpwapwa msaada wa madawati kutoka Kikundi cha Vijana cha Umoja Kisima. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Watanzania waoneshwa fursa biashara mtandao

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WATANZANIA wametakiwa kuacha matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii kwa kutumia fursa zilizoko katika Sekta ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kubuni biashara mtandao pamoja na kujifunza mbinu mbalimbali zitakazo wasaidia kujikwamua kiuchumi.

Hayo, yalibainishwa jana na washiriki wa kikao cha kujadili vikwazo na fursa za kidijitali kwa wanawake na watoto kilichoandaliwa na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali ya POLLICY na OMUKA HUB, yanayojihusisha na utoaji wa elimu ya matumizi sahihi ya mitandao ya kijamii katika mikoa ya pembezoni.

Mmoja wa washiriki kutoka Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Asia Juma, alisema wadau wanapaswa kuendelea kupeleka elimu kwa umma kuhusu matumizi sahihi ya TEHAMA.

Alisema, matumizi sahihi ya mitandao ya kijamii yatasaidia wananchi kujikwamua kichumi kwa kutumia fursa zilizoko katika sekta hiyo.

"Wananchi wanapaswa kutumia fursa zilizoko katika mitandao ya kijamii badala ya kuendeleza matumizi mabaya kwa kuwa katika mitandao ya kijamii zipo fursa nyingi kama vile kujifunza masuala ya lishe kwa watoto, afya matumizi ya biashara mtandao mamilioni mengi yapo huku hata waanzilishi wa mitandao kama Face book, WhatsApp, wametajirika kutokana na kubuni vitu vyenye tija," alisema. Alisema mitandao ya kijamii ikitumika vizuri itawezesha kukuza biashara za wajasiriamali wadogo kwa kuuza bidhaa zao maeneo mbalimbali kupitia simu zao za mkononi.

"Jamii inapaswa kutumia vifaa vya TEHAMA kushiriki kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla na hiyo ndiyo maana sisi serikali kuita uchumi wa kidijitali," alisema.

Mratibu wa mradi kutoka Shirika la POLLICY, Navina Mutabuzi, alisema wametoa elimu ya matumizi sahihi kwa makundi mbalimbali ya wanawake na vijana kwenye mikoa ya pembezoni.

Mutabuzi, alitoa rai kwa mashirika mengine na wadau wa TEHAMA na jinsia kuwasaidia wanawake na vijana wa mikoa ya pembezoni ambao utafiti unaonyesha kuwa bado wameachwa nyuma katika matumizi ya mitandao ya jamii.

Meneja wa Shirika la OMUKA HUB, Dorice Kaijage, alisema lengo la kutekeleza mradi huo ni kuwezesha makundi ya wanawake na vijana ambayo yameachwa nyuma.

Alisema ujuzi wa kidijitali ni muhimu kwa makundi yote ili kusaidia vijana kuondokana na matumizi ya kutuma picha (kupost) zenye maudhui mabaya.

"Mpaka sasa katika Wilaya ya Bukoba tumeshazifikia shule zaidi ya 15, vyuo vya kati VETA na vijana zaidi 1,000 tumewapa mafunzo ya umuhimu wa mitandao ya jamii," alisema.

Mmoja wa wanufaika wa mafunzo hayo makazi wa Wilaya ya Bukoba, Ester Kagaruki, alisema yamemsaidia kujifunza mbinu mbalimbali za kuboresha biashara zake.

"Mimi ninamiliki saluni nimetumia mitandao ya kijamii kujifunza mbinu na aina mbalimbali za misuko, lakini kupata wateja, nawashauri Watanzania kutumia mitandao hii kwa manufaa badala ya kutumia vitu ambavyo havina maudhui mazuri kwa jamii yetu," alisema.

## Chanzo kuongezeka ukatili nchini chatajwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

UKOSEFU wa elimu ya malezi kwa jamii ni sababu ya kuongezeka kwa kasi ya vitendo vya ukatili nchini.

Ofisa Maendeleo ya Jamii kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Vaileth Simon, alisema hayo juzi wilayani Chemba katika mafunzo ya utoaji elimu kwa wazazi na walezi yaliyoandaliwa na Shirika lisilo la kiserikali la Dorcas Aid International Tanzania Pamoja na Tunajali Development.

Simon, alisema hali ya ukatili kwa sasa ni kikwazo kwa sababu wazazi wengi wanashindwa kutimiza wajibu wao kutokana na kukosa elimu ya malezi kwa watoto katika familia na jamii kwa ujumla.

"Sisi mkakati wetu ni kuifikia jamii kwa kutoa elimu ya malezi chanya, lakini kuanzisha vikundi mbalimbali yakiwamo makundi ya wazazi. Pamoja na kuweka mikakati katika sera, mipango na haki za watoto ili watu wafahamu haki za mtoto, mambo ya ukatili na elimu ya malezi," alisema Simon.

Mratibu wa miradi ya watoto na wazee, Goodluck Kivuyo, kutoka ofisi za Dorcas Aid International Tanzania pamoja na Tunajali Development, alisema kutokana na watoto kukosa malezi, Shirika waliamuwa kuandaa mafunzo ya malezi na makuzi bora kwa watoto ili jamii ipaze sauti wanapokatiliwa.

"Kupitia miradi ya watoto na wazee tumeunda kamati, kutokana na utandawazi kuna masuala mengi yameibuka yanaathiri watoto wetu mfano suala la ulawiti, ambapo kila mwezi tunakutana na hizi kamati.

"Kupitia kamati ya watoto tumegundua kuna changamoto ya utoro kwa wanafunzi kwa hiyo mtoto anaweza kufika nyumbani mzazi asijue mtoto wake yupo darasa la ngapi.

Alisema kutokana na hali hiyo Dorcas International Tanzania na Tunajali Development ikaona umuhimu wa kuandaa mafunzo ya malezi na makuzi bora kwa watoto, leo tuna darasa la wazazi 150 ambao wanapatiwa mafunzo elimu ya kula na makuzi," alisema Kivuyo.

Nao wakazi wa Kijiji cha Chambalo, wilayani Chemba, Zainabu Juma, alilishukuru shirika hilo kwa kutoa mafunzo hayo kwa kuwa jamii ilikuwa haijui kumtumikisha mtoto kwa kupeleka kufanya kazi za ndani ni ukatili.

"Wito wangu mimi kwa wanajamii wa Chambalo haya tuliyofundishwa tuyazingatie, imetuhuzunisha sana kuona mtoto wa kiume wa miaka minne amelawitiwa au mzazi wa kiume kufanya mapenzi na mtoto wake wa kumzaa naiomba jamii tuwe makini.

"Kwa hawa wenye taswira kama hizi au maono kama haya yakuwafanyia mabinti au watoto wakiume kuwalawiti kwa kweli waache kabisa, vitendo hivi si haki kabisa hata mwenyezi Mungu pia hapendi," alisema.

Ofisa Ustawi wa Jamii Wilaya ya Chemba, Stella Kigoda, alisema hali ya malezi katika wilaya hiyo sio nzuri, mwaka huu wamepokea kesi za ukatili 20 huku akitaka ushirikiano wa Jeshi la Polisi pamoja na jamii ili kutokomeza vitendo hivyo.

Shirika la Dorcas Aid International Tanzania linatekeleza mradi wa wazee katika kijiji cha Chambalo Wilaya ya Chemba kwa kuwajengea uwezo wazee kujitegemea wenyewe kwa kuwapa elimu ya ujasiriamali, ufugaji wa kuku aina ya saso, kilimo bora na elimu kujua haki zao na kutafsiri sera ya wazee.

# Waziri aagiza vyuo vikuu kuwa na madawati kijinsia

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, amevitaka vyuo vikuu kuweka mazingira bora kwa wanafunzi wao kwa kuanzisha madawati ya kinjisia ili kuwajengea uwezo wa kuripoti kesi za ukatili na unyanyasaji wa kijinsia zinapotokea.

Aliyasema hayo jana katika hafla ya uzinduzi wa dawati la Jinsia la Chuo kikuu cha Zanzibar University (ZU), huko Tunguu Mkoa wa Kusini Unguja ukiwa na ujumbe wa 'Tupinge ukatili wa kijinsia vyuoni, tumlee tumuenzi na tumlinde mwana chuo'.

Alisema dhana ya kuanzishwa kwa dawati ni kutokana na wanafunzi kufanyiwa vitendo vya unyanyasaji na dawati hilo ni mkombozi kwao hasa kwa wanafunzi wa kike kwa sababu tatizo la udhalilishaji katika vyuo vikuu linajitokeza mara kwa mara.

Aidha, alisema wapo baadhi ya wanafunzi wanatumika vibaya hivyo amewashauri kuachana na tabia hiyo na badala yake kufuata taluma waliyoikusudia itakayowezesha kuweka mazingira yao ya baadaye kuwa bora.

Waziri Pembe alisema erikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania imefanya utafiti na kubaini matatizo mengi yaliyopo vyuoni ikiwemo vitendo vya ukali na unyanyasaji wa kijinsia vinavyo leta athari kwa taifa.

Waziri Pembe aliwataka wahadhiri kuielimisha jamii kuishauri serikali na kupanga mikakati bora itakayoleta maendeleo endelevu.

Hta hivyo, alisema malengo ya serikali ni kuona vyuo vyote vya Zanzibar vinaanzisha dawati la kijinsia ili kuwapa fursa wanafunzi kueleza matatizo yao na kupatiwa ufumbuzi wa haraka, hatua hiyo itawasaidia wanafunzi kubaki salama.

Msaidizi wa Chuo hicho, Juma Rashid Khamis, alisema dawati hilo limeanzishwa sio kwa huruma bali ni kuonyesha hisia na fursa mpya kwa wale wanaohisi wameonewa ili mwanamke aheshimu haki zake na mwanamume aheshimu haki zake.

Alisema kuwapo kwa dawati la jinsia katika chuo hicho ni kuingiza nadharia ya kitaaluma na kuona kuwa jinsia sio suala la kisiasa bali njia nzuri ya kumjenga mtoto wa kike kuwa muwazi kwa lolote analotendewa.

Wanafunzi wa chuo akiwamo rais wa serikali ya wanafunzi ,Said Hamad Salum, alisema dawati hilo litawawezesha wanafunzi kuripoti kesi zao ili haki iweze kutendeka.

Alisema kumekuwapo kwa vitendo hivyo katika vyuo wakifanyiwa wanafunzi ambao wamekuwa waoga na hawako wawazi kuripoti wanapofanyiwa vitendo hivyo kwa kuogopa kufelishwa katika masomo yao.




Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar, Riziki Pembe Juma akizindua dawati la jinsia katika Chuo Kikuu cha Zanzibar kilichopo Tunguu jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## SMZ kujenga jengo la kisasa ZAECA

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema itajenga jengo la kisasa la Ofisi za Mamlaka ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi (ZAECA) kwa ajili ya kutoa huduma zake kwa ufanisi mkubwa.

Hayo yalisemwa jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba Sheria, Utumishi na Utawala bora, Haroun Ali Suleiman, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Pandani Professa Omar Faki Hamad, aliyetaka kujua lini serikali itajenga jengo la kisasa la ofisi za mamlaka ya kupambana na rushwa.

Alisema ni kweli hivi sasa ZAECA ofisi zake hazina hadhi kulingana na majukumu yake ambayo ni kupambana na kudhibiti rushwa nchini.

Alisema juhudi zinafanywa kuona kwamba serikali inajenga jengo la kisasa lenye kulingana na hadhi ya taasisi hiyo iliyopewa majukumu ya kupambana na rushwa.

"Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, nataka niwaambie kwamba serikali ipo katika hatua za mwisho za kujenga ofisi ya kuzuia rushwa ambayo itakuwa na hadhi kulingana na majukumu yake," alisema.

Alisema maboresho makubwa yamefanywa katika ikiwamo kuweka mifumo ya kufuatilia kesi zote zinazohusu rushwa.

Alisema mifumo hiyo lengo lake kuona kesi hizo zinasikilizwa kwa wakati na kutolewa hukumu baada ya kukamilisha ushahidi.

"Tumefanya maboresho makubwa katika mamlaka ya kupambana na rushwa na uhujumu wa uchumi ZAECA ikiwamo kuweka mifumo ya kufuatilia mwenendo wa kesi zote zinazohusiana na mambo ya rushwa na uhujumu wa uchumi," alisema.

# 'Wajawazito kuchelewa kufika hospitali huchangia vifo'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya Zanzibar, Ahmed Nassor Mazrui, amesema vifo vya mama na mtoto vitokanavyo na uzazi vinatokana na sababu mbalimbali ikiwamo wajawazito kutofika kwa wakati katika vituo vya afya.

Alisema wajawazito wengi husubiri mpaka uchungu wa uzazi ukaze ndio hukimbilia hospitali na kuwafanya baadhi yao hujifungua njiani.

Alisema kufanyika kwa utafiti wa huduma za mama kabla na baada ya kujifungua kuhusu maradhi ya ukimwi na kifua kikuu pamoja na malaria, kutasaidia kuimarisha afya za kinamama nchini.

Aliyasema hayo jana katika hafla ya uwasilishwa kwa ripoti ya hatua ya awali ya utafiti kuhusu mradi wa kuwasaidia mama wajawazito na watoto kabla na baada ya kujifungua unaoendeshwa na chuo kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) kwa ufadhili ya Global Fund iliyofanyika Maruhubi, visiwni humo,

Waziri Mazrui alisema, mradi huo ni muhimu ambao umewajengea uwezo watendaji kutoka vituo 10 vya afya visiwani humo ili kupunguza vifo vya mama na mtoto vitokanavyo na uzazi.

Alisema vifo vya mama na mtoto vimepungua, ingawa hali bado sio nzuri kwa sababu kila watoto 100,000 wanaozaliwa kuna vifo 260 kila mwaka na malengo ya serikali ifikapo mwaka 2030 kuwa na vifo chini ya 70.

Mazrui alitaja sababu zingine zinazosababisha vifo hivyo ni kinamama kuchelewa kwenda kliniki kwa wakati wanapopata ujauzito, lishe duni ya mama wajawazito na uzembe kwa baadhi ya wahudumu wa afya.

Aliwataka Mama wajawazito kuhakikisha wanakula mlo mzuri hasa kipindi cha ujauziro ili kutokuwa na upungufu wa damu ambapo tatizo hilo husabbaisha kupoteza maisha ya mama na mtoto.


"Mjamzito asipokula vyakula vya lishe mtoto anayezaliwa huwa na uzito dhaifu lakini pia mama huwa na upungufu wa damu hivyo ni vyema kinababa kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa wake zao ikiwamo mlo bora ili kujifungua salama," alisema.

Kiongozi wa mradi huo kutoka SUZA, Aisha Juma Fakih, alisema, lengo la mradi huo ni kuboresha huduma za afya ya mama na mtoto katika kutoa huduma kabla na baada ya kujifungua na kutokomeza magonjwa ya Ukimwi, kifua kikuu na Malaria.

Mtafiti wa mradi huo kutoka SUZA, Dk. Salma Abdi Mahmoud, alisema utafiti uliofanywa kupitia mradi huo umebaini changamoto mbalimbali ikiwamo ukosefu wa huduma za afya, uhaba wa vifaa na miundombinu katika vituo vya afya ikiwamo majisafi na salama.

Alisema matarajio makubwa ni kuona wanaendelea kushirikiana na Wizara ya Afya ili kuepusha vifo vinavyotokana na uzazi.

Mradi huo ni wa miaka minne na umeanza kutekelezwa mwanzoni mwa mwaka huu ambao unatekelezwa na Chuo kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kwa kushirikiana na Liverpool School of Tropical Medicine chini ya ufadhili wa The Global Fund.





# Wanawake wapaza sauti kuachiwa familia

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

WANAWAKE wa Kijiji cha Masengwa, wilayani Shinyanga, wamelalamikia kutelekezwa na wanaume zao baada ya kuuza mazao yote na kuondoka na fedha.

Walibainisha hayo juzi wakati Nipashe ilipotembelea kwenye kijiji hicho katika msimu huu wa kilimo na kukuta familia nyingi wanaolima ni wanawake na watoto.

Katika kipindi hiki cha kilimo wanaume wengi wanadaiwa kutoonekana nyumbani wala kwenda shambani, badala yake wanasubiri wakati wa mavuno ambao hurudi nyumbani na kuuza mazao yote na kutekeleza familia zao.

Mmoja wa wanawake hao, Tatu Macheleka, alisema kipindi cha mavuno wanaume wanakuwa na sauti ya kuuza chakula na baadhi yao wakishauza wanakimbia na fedha zote na kuacha familia ikihangaika.

"Tunaomba serikali itoe elimu ya utunzaji wa chakula kwa waume zetu huku vijijini ili waache kutufanyia ukatili wa kututelekezea familia, sasa anapomaliza kuuza chakula ndani na kisha kunikimbia unadhani mimi nitawaleaje hawa watoto na shughuli zetu huku vijijini ni kilimo tu," alisema Macheleka.

"Mimi sina mwanaume tena naishi peke yangu, alishanikimbia siku nyingi tunachoomba kwa serikali ikiwezekana ipige marufuku uuzaji wa chakula ovyo vinginevyo wanawake wengi watatelekezewa familia," aliongeza.

Mwanamke mwingine, Janety Nkuba alisema mwanamke akitelekezewa familia na mume wake huanza kulima vibarua kwenye mashamba ya watu ili kupata fedha kidogo ambayo watanunua unga na kuwalisha watoto.

Mtendaji wa Kata ya Masengwa, wilayani Shinyanga, Hussen Mjaliwa alisema tatizo la wanaume kutelekeza familia lipo kijijini humo, lakini sio kwa ukubwa kama miaka ya nyuma, wanajitahidi kutoa elimu ya utunzaji wa chakula kwa kushirikiana na maofisa kilimo.

Alisema kipindi cha mavuno, ofisi yake inapokea kesi nyingi za ugomvi wa kuuza chakula pamoja na wanaume kulalamikiwa kutelekeza familia. Alisema wanatatua kesi hizo kwa kutumia njia ya usuluhishi wa pande zote mbili na kisha familia kuelewana na kuendelea kuishi kwa amani.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Masengwa, Zacharia Ntemi, alisema tatizo kubwa linalosababisha wanaume kutelekeza familia ni ukosefu wa elimu ya kujitambua, kuishi kwa mazoea na kuendekeza mambo ya zamani.



Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini, Patrobas Katambi ambaye ni Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Kazi, Vijana, Ajira na Wenye ulemavu (katikati), akikagua ujenzi wa soko kuu la Manispaa ya Shinyanga unaogharimu Sh. bilioni 1.8, (kushoto) ni Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga, Jomaary Satura. **PICHA: MARCO MADUHU**

## Hatima aliyekuwa DC Tabora kujulikana leo

**Na Halima Ikunji,** TABORA

KESI inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Tabora, Kitwala Komanya, imepangwa kutolewa uamuzi leo baada ya pande zote mbili kuwasilisha hoja za majumisho kwa maandishi.

Komanya ambaye aliengulіwa katika nafasi hiyo mwaka jana anakabiliwa na kesi ya madai ya fidia ya Sh. milioni 140 kutokana na vitendo vya udhalilishaji alivyomfanyia mwananchi Mgai Ntonge Januari 5, mwaka huu.

Katika shauri hilo namba 94 la mwaka 2021, mlalamikaji anataka alipwe Sh. milioni 80 kutokana na kuzuia uhuru wake, Sh. milioni 30 kutokana na tendo la kukamatwa na kushtakiwa kwa nia ovu na Sh. milioni 30 kwa kudhalilishwa utu wake.

Anadaiwa kuwa siku hiyo Komanya akiwa ni Mkuu wa Wilaya ya Tabora akiambatana na askari wa Jeshi la Polisi walifika nyumbani kwa mlalamikaji eneo la Ipuli na kumkamata na kisha kumdhalilisha.

Ntonge aliongeza kuwa Komamya akiwa na askari wawili wenye bunduki aina ya SMG, baada ya kumkamata walimdhalilisha mbele ya familia yake na majirani zake kwa kuamuru apige magoti barabarani.

Mahakama ya Mkoa mbele ya Hakimu Mkazi, Jovitt Katto, imefikia hatua hiyo baada ya kumaliza kusikiliza mashahidi wa pande zote mbili akiwamo Mkuu wa Polisi Wilaya ya Tabora, George Willbard, ambaye aliitwa kama shahidi wa mshtakiwa Kitwala Komanya.

Katika utetezi wake mbele ya Hakimu Katto huku akiongozwa na wakili wa kujitegemea, Issa Mavulla, Komanya alidai kuwa amefunguliwa shauri hilo kwa nia ya kumkomoa na kumkomesha.

Katto ni hakimu wa tatu kusikiliza shauri hilo ambalo awali lilianza kusikilizwa na Hakimu Sigwa Nzige, lakini mshtakiwa alimkataa ndipo likaamishiwa kwa Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Wilaya ya Tabora, Demotrio Nyakunga ambaye hakuendelea nalo.

Komanya alikana kuhusika na tuhuma zinazomkabili za vitendo vya udhalilishaji dhidi ya mlalamikaji, Alex Ntonge wakati wa uongozi wake.

Hata hivyo, mshtakiwa huyo alikiri kuambatana na Mkuu wa Polisi Wilaya ya Tabora, George Willbard, kwenda nyumbani kwa mlalamikaji kwa ajili ya kumkamata akituhumiwa kutumia mitandao ya kijamii kumdhalilisha.

# Wananchi washauriwa kupima afya zao

**Na Lilian Lugakingira,**
BUKOBA

WAKAZI wa Mkoa wa Kagera wameshauriwa kujenga utamaduni wa kupima afya zao mara kwa mara ili kubaini maambukizi ya magonjwa na kupata matibabu mapema.

Akizungumza wakati wa kongamano la wanawake katika Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera jana ambalo lilikwenda sambamba na uchangiaji damu, Mratibu wa Kitengo cha Damu Salama, Dk. Boniphace Meza, alisema kuwa tatizo la wananchi kutopima magonjwa mbalimbali limekuwa likisababisha baadhi ya damu inayokusanywa kukutwa na maambukizi, ikiwamo homa ya ini.

Dk. Meza alisema kuwa damu inayopatikana kwa wanafunzi shuleni ina usalama kwa kiwango kikubwa ikilinganishwa na ile inayopatikana katika jamii na kwamba ili kupunguza tatizo hilo inabidi wananchi wajenge utamaduni wa kupima afya zao na wale watakaobainika kuwa na maambukizi ya magonjwa watibiwe. "Shule zinachangia kwa usalama mkubwa kwa mfano tunaweza kuwatoa damu wanafunzi kama 200, majibu yakirudi mengi yanakuwa salama, maana kwa wanafunzi unaweza ukakuta asilimia kati ya 97 hadi 98 ni salama, lakini kwenye jamii tunaweza tukatoa damu nyingi tatizo wananchi wengi wanakuwa hawapimi magonjwa wanasahau, kwa hiyo wakati mwingine damu zao zinakutwa na magonjwa," alisema.

Mmoja wa wanawake waliojitokeza kuchangia damu, Olver Katemana, aliwasihi wananchi kuacha uoga na kujitokeza kuchangia damu.

"Maana asilimia kubwa wanaogopa, wapo wanaofikiri kwamba kuna matatizo, labda wakitolewa damu wataugua au watakufa, lakini kutolewa damu ni hali tu ya kawaida nimethibitisha hilo leo, kwa hiyo nawasihi hata wanawake wenzangu wajitokeze," alisema Katemana.

Mwananchi mwingine aliyejitolea damu, Eliana Tibaijuka, mkazi wa Kibeta, aliwaasa wanawake kujitokeza kuchangia damu ili kuokoa maisha ya makundi yanayohitaji huduma hiyo. Alisema damu hiyo itawasaidia wanawake wanaofanyiwa upasuaji wakati wa kujifungua, waliopata ajali na watoto wanaokumbwa na tatizo la upungufu wa damu.

Diwani wa Kata ya Kibeta, Annastella Alphonce, aliyeandaa kongamano hilo, alisema alifikia uamuzi huo ili kuwaweka wanawake pamoja kwa lengo la kujadili matatizo yanayowakabili yakiwamo ya kiuchumi na namna ya kukabiliana nayo.

"Kila mara utasikia damu inahitajika hospitali, kwa hiyo tukaona tujitolee kwa hili ili hata Rais wetu Samia Suluhu Hassan asikie kuwa kuna kinamama wanaojali na wanamuunga mkono kwa jitihada zake za kuhakikisha wananchi wanakuwa na afya bora," alisema Alphonce.

Kwa mujibu wa mratibu huyo, upatikanaji wa damu katika Mkoa wa Kagera mzuri kutokana na wananchi kuwa na mwamko wa kujitokeza kuchangia.

Alitoa mfano kuwa katika kituo cha damu kilichoko katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa kuna mahitaji ya chupa kati ya 180 hadi 200 kwa mwezi ambazo kwa sasa zipo.

## HABARI KIMATAIFA

# Marekani yaionya Belarus

**WASHINGTON, Marekani**

MAREKANI itaendelea kufuatilia kwa karibu iwapo nchi ya Belarus inataka kutoa msaada wa ziada kwa Russia katika vita vyake na Ukraine.

Wizara ya Mambo ya Nje ilisema jana kuwa iwapo itatokea, vikwazo vipya vitawekwa dhidi ya serikali ya nchi hiyo.

Msemaji wa wizara hiyo, Ned Price katika mkutano na waandishi wa habari alisema jaribio lolote la kitoa msaada litakuwapo ni sawa na uchokozi.

"Iwapo tutaona haya [majaribio ya kutoa msaada wa ziada] tunaona uwezekano wa hili, basi tutatoa jibu linalofaa kwa kuanzisha vikwazo zaidi," alisema.

Price pia alizungumzia kuhusu kauli ya Rais wa Russia, Vladimir Putin, aliyoitoa katika mkutano wa waandishi wa habari kufuatia mazungumzo na Rais wa Belarus, Alexander Lukashenko, kwamba hawatasita kulichukulia hatua taifa lolote ikiwa ni pamoja na Belarus.

Mwakilishi wa Wizara ya Mambo ya Nje alisema kauli ya Putin ni ya ukomo wa kiongozi asiyeweza kubadilika na maneno hayo yametoka kwenye midomo ya mkuu wa nchi, ambaye sasa anajaribu kuzitwaa nchi nyingine jirani zenye amani.

Utegemezi wa Lukashenka kwa Putin unaibua hofu kwa utawala wa Ukraine kwamba Rais wa Russia huenda akamlazimisha kujiunga na hatua za kijeshi dhidi yake. Wiki iliyopita, Kamanda Mkuu wa majeshi ya Ukraine, Valery Zaluzhny, alisema katika mahojiano na jarida la The Economist kwamba Russia inaandaa wanajeshi 200,000 kwa ajili ya mashambulizi mapya, ambayo yanaweza kuanzia kusini, mashariki, au hata kutoka katika eneo la Belarus mapema mwezi Januari.

Katika hatua nyingine, Ukraine inaimarisha ulinzi wa mpaka wake na Belarus kutokana na hofu ya Russia inaweza kuandaa mashambulizi mapya.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Yevhen Yenin, aliiambia BBC kwamba Ukraine itaimarisha mpaka wa Belarus kwa kutumia vikosi vya kijeshi.

Haya yanajiri wakati Vladimir Putin alisafiri kwenda Minsk kukutana na Rais wa Belarus, Alexander Lukashenko wa Belarus ambako inapakana na Russia na Ukraine.

Rais wa Urusi baadaye aliamuru kuimarishwa kwa mipaka ya Urusi na udhibiti wa kijamii ndani ya Urusi.

Alisema vyombo vya usalama vinapaswa kuzuia haraka jaribio lolote la kukiuka mipaka ya Russia kupambana na hatari zinazotoka nje ya nchi na kuwabaini wahaini na wahujumu.

Pia alisema huduma hizo maalum zinapaswa kuhakikisha usalama wa watu wanaoishi katika maeneo ya Ukraine ambayo Russia inadai kuwa yake.

Katika baadhi ya maeneo hayo ni Kherson hivi karibuni ilikumbwa na mabadiliko makubwa ya kijeshi.

Wizara ya ulinzi ya Russia ilitangaza kuwa wanajeshi wake walioko Belarus watafanya mazoezi ya kijeshi ya pamoja na Belarus.

Akijibu hili na ziara hiyo Yenin alithibitisha kwa kusema "Tunajenga safu zetu za ulinzi kuvuka mpaka na Russia na Belarus."

Wakati Belarus haijahusika moja kwa moja katika vita, iliruhusu wanajeshi wa Russia kutumia eneo lake kuzindua uvamizi mnamo Februari.

***BBC***



Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, akiwa kwenye ziara ya kushtukiza katika mji Bakhmut, baada ya vikosi vya Ukraine na Russia kupigana vikali. **PICHA: REUTERS**

# Mpango wa kuhamisha wahamiaji wazidi kupingwa

**LONDON, Uingereza**

BAADA ya Mahakama Kuu ya Uingereza kuhalalisha juzi mpango wa kuwapeleka nchini Rwanda wahamiaji wanaoingia kinyume cha sheria nchini humo, tayari kumeibuka ukosoaji mkubwa juu ya uamuzi huo.

Mara uamuzi huo kutolewa shirika la msaada la Christian Aid lilisema licha ya Rwanda kuwa katika mazingira magumu yatokanayo na athari za mabadiliko ya tabianchi, wizara ya mambo ya ndani ya Uingereza haikufanya tathmini juu ya hatari ya hali ya hewa ambayo wahamiaji hao wanaweza kukabiliana nayo ikiwa watapelekwa huko.

Chini ya makubaliano kati ya Uingereza na Rwanda yaliyofanyika mwezi Aprili, inakusudia kuwahamisha watu wanaowasili nchini humo kinyume cha sheria kuelekea taifa hilo la Mashariki mwa Afrika, lililo kwenye umbali wa zaidi ya kilomita 6,400 kutoka Uingereza.

Waandamanaji wa Uingereza wakipinga hatua ya wahamiaji kupelekwa nchini Rwanda.

Shirika hilo la misaada limebaini kuwa, uamuzi huo umechukuliwa licha ya ripoti iliyotolewa mwaka huu na wizara ya mambo ya nje ya Uingereza, ambayo iliangazia vitisho lukuki vinavyohusishwa na hali ya hewa ambavyo tayari vinaiathiri Rwanda huku utabiri ukionyesha kuwa hali itakuwa mbaya zaidi katika miaka ijayo.

***DW***

# Upinzani washtukia ugomvi wa Museveni na mwanawe

**Kampala, Uganda**

CHAMA cha upinzani nchini Uganda Forum for Democratic Change (FDC) kimesema kuwa kauli tata za kisiasa za mwana wa kiume wa Rais wa nchi hiyo, Yoweri Museveni, Jenerali Muhoozi Kainerugaba dhidi ya chama tawala zililenga kupotosha malengo ya upinzani katika mapambano dhidi ya mabadiliko ya utawala.



Akizungumza na waandishi wa habari katika makao makuu ya FDC mjini Kampala, Rais wa chama hicho, Patrick Oboi Amuriat, alisema 'uchochezi' wa Jenerali Mohoozi ni hatua iliyopangwa vyema ili kuonyesha mapigano baina ya baba na mwanawe wa kiume, ili kuchochea hisia kutoka kwa upinzani ambao unalengwa.

Akinukuliwa na gazeti binafsi la Uganda, The daily Monitor, alisema wanaamini hayo ni baadhi ya mambo ambayo yamepangwa vyema na kutekelezwa ili kuonyesha kuwa kuna vita kati ya baba na mwana.

"Tunafahamu kuwa hizi aina za mbinu ambazo Museveni amekuwa akihusika nazo ili kuendelea kubakia madarakani," limemnukuu gazeti la Daily Monitor Amuriat akisema.

Mara kadhaa Jenerali Muhoozi amekuwa akituma jumbe tata za kisiasa kwenye ukurasa wa mtandao wake wa Twitter, yakiwamo maandishi kwamba hana imani na chama tawala ambacho baba yake ni mwenyekiti.

Tarehe 27 Oktoba, Jenerali huyo mwenye nyota nne aliandika kwenye Twitter : "Njia pekee ninayoweza kumlipa mama yangu ni kwa kuwa Rais wa Uganda! Na nitafanya hilo bila shaka!"

***BBC***


**BILO STAR DEBT COLLECTOR CO. LTD**

**WE ARE DEALING GENERAL AUCTIONING, DEBT COLLECTION, EVICTION, INVESTIGATION AND REPOSSESSION, STORAGE, COMMISSION AGENCY AND GENERAL BUSINESS.**

**NOTISI YA SIKU (14) NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kampuni ya **BILO STAR DEBT COLLECTOR COMPANY LIMITED kwa idhini tuliyopewa na mteja wetu STANBIC BANK TANZANIA LIMITED** tunapenda kukutaarifu ndugu **TITAN VENTURE GROUP COMPANY LIMITED** unatakiwa kulipa deni unalodaiwa na mteja wetu. Kwamba unatakiwa kulipa deni hilo ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili. Pia tumeelekezwa kuwa ukishindwa kulipa deni hilo ndani ya siku (14) tutauza kwa mnada wa hadhara mali yako iliyowekwa dhamana ambayo ni kama ifuatayo:-

| JINA LA MDAIWA | MAELEZO YA DHAMANA NA AINA YA DHAMANA (GARI) | ENEO LA MNADA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| TITAN VENTURE GROUP COMPANY LIMITED | GARI AINA YA FORD RANGER PICK-UP YENYE NAMBA ZA USAJILI T 356 DUQ | Ghala ya BILO STAR lililopo Mbezi Beach Dar es Salaam | Mnada utafanyika tarehe 04/01/2023 kuanzia saa mbili na nusu asubuhi na kuendelea |

217202302

**MASHARTI YA MNADA**

Mnunuzi atakayefanikiwa kununua gari husika atalazimika kulipa 25% papohapo na kiasi kilichobaki 75% atatakiwa kulipa ndani ya siku 14 kuanzia tarehe ya mnada. Akishindwa kulipa 25% aliyolipa haitarudishwa na mnada utarudiwa.

**KWA MAELEZO ZAIDI**

**Fika ofisi zetu zilizopo Mbezi Beach au wasiliana nasi kwa simu namba 0719206984, 0716943424,0713552685 email: bilostarcompany@gmail.com , S.L.P 16095 DAR ES SALAAM.**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya TEMEKE kituo cha JUMUISHI mkoa wa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa mirathi na 2401/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU RAMADHANI MUSA TANDA KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETEWA NA MOSI RAMADHANI MUSA**

### TANGAZO

**(kanunin ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 24 mwezi 01 mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo
**Zingatia.** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakama kukaguliwa
Imetolewa leo **Tarehe 16 mwezi 12 mwaka 2022.**

## KUPOTEA KWA CHETI

**BABEL KAHALILI MBEMBELA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHA USAJILI WA KANISA LA NATIVE LAST CHURCH OF GOD MISSION CHENYE NAMBA **6346/14.**YEYOTE ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/486002/2022.**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA SONGEA LILILOKO SONGEA**
**MAOMBI MADOGO NA.649/2021**
**QEENTIN NTALA ——————— MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**YUSTIN BANDA ————————- MJIBU MAOMBI**

### WITO/KUITWA SHAURINI

Mjibu maombi unataarifiwa kuwa Muombaji amefungua shauri la mgogoro wa ardhi dhidi yako .Hivyo basi unatakiwa kufika shaurini bila kukosa binafsi au wakili wako, au wote kwa pamoja siku ya tarehe 30/01/2023 saa 3:00 asubuhi. Kumbuka pia nyaraka zote kuhusu mgogoro huu zipo hapa barazani kwa ajili ya kuleta hati zako za utetezi.

Kumbuka pia kushindwa kwako kufika shaurini kutapelekea baraza hili kusikiliza shauri hili upande mmoja bila kujali uwepo wako.
Imetolewa leo nami na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 20/12/2022.

MWENYEKITI
SONGEA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**FORM II**

**SMM 1994 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo ya mwambao wilaya ya bagamoyo ,mkoa wa pwani.ombi la ndugu ADAM IDDI KILUNGI kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi namba 81/2022 ya marehemu MOSI KONDO watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na marehemu huyo wanaalikwa kuja kuhudhuria kesio wakitaka mnamo tarehe 21/12/2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hii.

**Wosia wa marehemu.........................................**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.176 OF 2022**

**In the matter of the Estate of the late ROXANA DOSCA KIJAZI of Dodoma at Dodoma**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**

**BY ALFRED ELIA SEMANGO.**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

All PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above-named deceased Person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 28 Day of 11, 2023

Dated at Dodoma this 20 day of 12, 2022

RESIDENT MAGISTRATE

**FORM NO. 58**
**IN THE COURT OF DISTRIC T DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 146 OF 2023**

**In Matter of the Estate of the Late AGNES ANSELIMO MLENGERA**

**By 1. AZIZA ATHUMANI ABDI**
**2. .................................**

All Persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or latter of administration) is made to the above - named petitioner.
Objection to the grand should be field on or before the **03RD** day of **January / 2023.**
Dated at **Morogoro**, this **20th** day of **DECEMBER 2022**

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA CHETI



**BILLY DIONISI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye Index No. **P 0110-0559** Kilichotolewa na baraza la Mitihani kupitia ILBORU SECONDARY SCHOOL CENTRE mwaka 2004. Yeyote atakaekiona atoe taarifa Kituo chochote cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **DOM RB 35545/2022.**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**LEONARD MAGAMBO MASATU** anatangaza kupotelewa na cheti cha Chuo chenye namba **M.BSCED 0000 742** kilichotolewa na Chuo Kikuu cha Dar es salaam mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **GE/RB/4422/2022.**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE — DOCG

## TANGAZO LA AJIRA KWA KADA MBALIMBALI
## KUMBUKUMBU NO. MST-TZ-202 2 1216

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi, uendeshaji na matengenezo ya bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Hoima Uganda mpaka Chongoleani Tanzania ambako kunajengwa kituo cha kuhifadhi mafuta ghafi karibu na Bandari ya Tanga.

Daqing Oilfield Construction Group Co., Ltd. Kwa maana nyingine (DOCG), ambaye ni MKANDARASI mkuu wa ujenzi wa kituo cha kuhifadhia mafuta ghafi ya Mradi wa **EACOP, (MST). DOCG** inawatangazia watanzania wenye sifa na uzoefu kuomba nafasi mbalimbali za ajira zilizopo mkoani Tanga katika kata ya Chongoleani. Kama zifuatazo:

1. Mhandisi wa Mazingira (Nafasi 1)
2. Mhandisi wa Ghala (Mkaguzi)(Nafasi 1)
3. Afisa wa Usimamizi wa Zabuni (Nafasi 1)
4. Afisa Udhibiti wa Mipango (Nafasi 1)
5. Mhandisi /Afisa wa Manunuzi (Nafasi 1)
6. Mratibu wa Ujenzi (Nafasi 4)
7. Mhandisi wa Ujenzi (Nafasi 1)
8. Mhandisi wa NDT (Nafasi 1)
9. Mhandisi wa Kudhibiti Ubora (Nafasi 1)
10. Msimamizi wa Masuala ya Usalama, Afya na Mazingira mahala pa Kazi (Nafasi 1)
11. Msimamizi wa Usalama na Ulinzi (Nafasi 1)
12. Mfasiri na Mkalimani wa Kiingereza,Kichina na Kiswahili (Nafasi 1)
13. Afisa usafirishaji na uchukuzi (Nafasi1)
14. Afisa Msimamizi na Mdhibiti wa Nyaraka za ofisi ( Nafasi 1)
15. Meneja wa Mishahara (Nafasi 1)
16. Afisa wa uhasibu na kodi (Nafasi 1)
17. Mhandisi na Msimamizi wa unyanyuaji mizigo (Nafasi 1)
18. Mhandisi wa Umeme (Nafasi 1)
19. Fundi Bomba (Kadhaa)
20. Mpiga Ribiti (Kadhaa)
21. Fundi wa Kuchomelea (Kadhaa)
22. Fundi umeme (Kadhaa)

**SIFA ZA WAOMBAJI WA KAZI**
- Shahada ya kwanza katika masomo yanayo husiana na fani husika na wenye shahada ya Uzamili watapewa kipaumbele.
- Kwa wahitimu wa kidato cha IV na wenye cheti cha daraja II kutoka chuo cha VETA au NTA daraja la 4 kwa vyuo vilivyosajiliwa na NACTE au taasisi zingine zinzotambulika. (Hii ni kwa mafundi umeme,bomba na mafundi ribiti)
- Uzoefu usiopunguwa miaka mitano kwa nafasi zote.
- Mwenye uwezo wa kufanya kazi kulinga na muda uliopangwa
- Uwezo mzuri wa kuwasiliana kwa maandishi na kuongea kwa kutumia lugha ya kiingereza.
- Uzoefu katika uzimamizi na uongozi.
- Mwenye uwezo wa kushirikiana na wenzake na kutoa matokeo chanya
- Kipaumbele chake ni watu na mwenyeshabaa katika kufikia matokeo.
- Uwezo wa kutambua na kutatua changamoto katika kazi.

**VIGEZO NA TARATIBU KWA WAOMBAJI WA NAFASI ZOTE ZA AJIRA**
- Awe raia wa Tanzania.
- Asiwe na rekodi ya uhalifu
- Waombaji wote waambatishe Wasifu binafsi wenye anuani na namba za simu zinazopatikana pamoja na majina ya wadhamini.
- Maombi yote yaambatanishwe na vyeti vya taaluma, maelezo, nakala za vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa waliofikia ngazi hiyo. Vyeti vingine kulingana na mafunzo na uzoefu vinakubalika kulingana na nafasi ya maombi.
- Hati zifuatazo zinapaswa kuambatishwa katika maombi kulingana na nafasi ambayo mtu anaomba. Hati hizo ni pamoja na, (lakini sio hizi tuu zifuatazo pekeyake)
  I. Uzamili/Shahada/Stashahada ya Juu/Stashahada/Astashahada
  II. Cheti cha kuhitimu kidato cha IV na VI
  III. Cheti cha kozi ya Kompyuta
  IV. Vyeti vya kitaaluma (Vyeti vya kitaaluma kutoka kwa bodi husika.

Watu wanaovutiwa, wenye uwezo na nia ya kufanya kazi na DOCG, katika nafasi ziliyotajwa hapo juu katika kituo cha kuhifadhia mafuta Ghafi (MST) wanapaswa kutuma maombi kupitia barua pepe : Ofisi ya Rasilimali Watu ya **tz_hr@docgi.cn** saa au kabla ya saa 17:00 kwa Saa za Afrika Mashariki (EAT), 04 JANUARY , 2023 . Kumbuka kuandika namba ya tangazo kwenye maombi yako EOI kwa **MST-TZ- 20221216 DOCG** .Wakiaainisha nafasi wanazoomba na mahala wanapotoka

**WANAWAKE WANAHIMIZWA KUOMBA.**

**Tarehe ya mwisho ya kutuma maombi itakuwa siku 14 kutoka siku ya tangazo.**
**TAARIFA; HAKUNA KUAJIRI MLANGONI**
**Maombi ni bure kabisa, usilipe kuomba au kupata kazi Kwa maswali (saa za kazi): 0692117239, 0652178898 & 0764 467564**

**Imetolewa na ;-**
**Afisa Rasilimali Watu (Daqing Oilfield Construction Group International)**
**Katika siku hii ya tarehe 20 Desemba 2022**

2172203202

NORWEGIAN CHURCH AID

## TAARIFA KWA UMMA

Norwegian Church Aid Tanzania inatoa taarifa kwa umma yakuwa imepokea Ruzuku kutoka kwa Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Mitaji (UNCDF) kwa ajili ya Mradi wa Kuwawezesha jamii kiuchumi unaoendana na mabadiliko ya tabia nchi. Kwa maelezo zaidi soma hapa chini.

| | |
|---|---|
| Mfadhili | United Nation Capital Development Fund (UNCDF) |
| Sarafu ya Mfadhili | Dola ya Kimarekani |
| Kiasi cha ruzuku | 100,000 |
| Muda | Miezi 11 |
| Kipindi cha utekelezaji | 01 Novemba 2022 hadi 30 Septemba 2023 |
| Shughuli muhimu | i) Kuimarisha upatikanaji wa pembejeo za kilimo kwa wakulima wa mahindi Kwa kuwaunganisha na wasambazaji wa pembejeo kupitia mfumo wa kidijitali.<br>ii) Kuanzisha vikundi vya biashara ndogo na za kati vya utengenezaji wa mifumo midogo ya umwagiliaji wa njia ya matone na ikiwa ni pamoja na kutoa usaidizi wa kiufundi katika kubuni na kutekeleza muundo wa biashara.<br>iii) Kusaidia mamlaka ya serikali za mitaa kujifunza na kutumia njia za kidigitali katika kupata taarifa mbalimbali na kujifunza mambo ya husuyo kilimo<br>iv) Kuhamasisha na kusaidia wawekezaji wapya 1,500 (vikundi vya wazalishaji 45) juu ya mbinu bora za kilimo, upatikanaji wa pembejeo na masoko. |
| Mkoa/Eneo la Utekelezaji | Kigoma |
| Kwa maelezo zaidi wasiliana kupitia | Mkurugenzi<br>Norwegian Church Aid Tanzania<br>Plot 436,Mwai Kibaki rd,TCRS House 3rd Floor<br>P.O Box 3955, Dar Es Salaam<br>Tel:+2 55 787 770 811 na +255 22 2700252 |

217202702

## BURUDANI

# DRAKE
## SASA KUTOA USHAHIDI WA MAUAJI

RAPA wa Marekani, Drake ni miongoni mwa watu maarufu sita ambao wameorodheshwa kwa ajili ya kutoa ushuhuda kwenye shtaka la mauaji ya rapa XXXTentacion mwaka 2018 ambaye aliuawa kwa kupigwa risasi.

Mawakili wa utetezi wamewasilisha orodha hiyo yenye jina la Drake, Quavo, Offset, marehemu Takeoff, Tekashi 6ix9ine na Joe Budden ambao wametajwa kama mashahidi kwenye nyaraka hizo za mahakama.

Kwa upande wa Drizzy ametajwa kwenye shtaka hilo la mauaji ya XXXTentacion kufuatia bifu lao la mwaka 2017.


Ambapo marehemu XXXTentacion aliwahi kuibuka na kudai Drizzy ameiba midondoko yake kutoka kwenye wimbo wake wa kwanza "Look At Me" na kuitumia kwenye wimbo wake "KMT" wa mwaka 2017.

Baada ya mwaka mmoja wa kutupiana maneno na mvutano, akaunti ya Instagram ya XXXTentacion yaliandikwa maneno yasemayo "If anyone tries to kill me it was champagnepapi," akimtaja Drizzy kama mtu ambaye anatishia kuchukua uhai wake.

Miezi minne baadaye, rapa huyo aliuawa kwa kupigwa risasi mjini Florida, Marekani.



## VERA SIDIKA ATARAJIA MTOTO WA PILI



MREMBO maarufu nchini Kenya, Vera Sidika, ni mjamzito kwa mara nyingine ikiwa ni mwaka mmoja na nusu tangu kujifungua mtoto wake wa kwanza, Asia.

Vera amefichua kuwa anatarajia mtoto wake wa pili na mumewe Brown Mauzo na kueleza ni furaha kwake kupata mtoto mwingine.

Mauzo kwa upande wake alimshukuru Vera kwa kuwa mke bora kwake na mama mzuri kwa mtoto wao, Asia.

Mwanamuziki huyo alimhakikishia Vera kuhusu upendo wake mkubwa kwake na kukiri kuwa anafurahia hatua mpya katika ndoa yao.

"Ni baraka iliyoje!!! Mtoto wa pili yupo njiani, tunapokaribia hatua nyingine katika ndoa yetu, ninachotaka kusema ni asante kwa kuwa mke na mama bora," aliandika kwenye Instagram.

"Wewe ni zawadi kutoka kwa Mungu na nina bahati kuwa na wewe katika maisha yangu, nakupenda mke wangu," alisema.

Wawili hao wamekuwa kwenye mahusiano kwa zaidi ya miaka miwili na walijaliwa mtoto wao wa kwanza Oktoba mwaka jana.

## FRED VUNJABEI AMKANA JOKETI




MFANYABISHARA maarufu wa nguo, Fred Vunjabei, amezidi kusisitiza kuwa, Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo, ni dada yake tu na si vinginevyo.

Vunjabei ametoa kauli hiyo akiwa mkoani Kigoma kwenye uzinduzi wa duka lake jipya ambapo, alipata nafasi ya kuzungumza na wanahabari baada ya zoezi la uzinduzi kukamilika.

"Nilishasema na niseme tena, Jokate ni dada yangu ni kiongozi ambaye ameaminiwa na rais, anasapoti vijana kama ambavyo na mimi nimekuwa nikifanya. Muacheni dada wa watu yupo kazini huko atapaliwa bure," alisema.

Kwa muda mrefu, Vunjabei amekuwa akihusishwa kuwa na uhusiano wa kimapenzi na Joketi ambaye kwa sasa ni mjamzito.

HABARI MICHEZO

# SIMBA QUEENS, YANGA PRINCESS JOTO LAPANDA

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WAKATI joto la watani wa jadi 'dabi', Simba na Yanga kwa upande wa malkia wao likizidi kupanda kwa makocha wa timu hizo, Kocha wa Simba Queens, Charles Lukulu, amesema pamoja na kuendelea na maandalizi, wako tayari kwa mchezo huo utakaopigwa kesho, Alhamisi.

Simba Queens na Yanga Princess zitashuka katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kesho kumenyana kwenye mechi ya Ligi Kuu raundi ya tatu, zote zikiwa na alama tatu katika nafasi ya tano na sita baada ya kupoteza michezo yao ya ufunguzi ya ligi hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Lukulu alisema wanaendelea na mazoezi kwa ajili ya kujiimarisha kuelekea mchezo huo katika kuhakikisha wanapata pointi tatu ili kufikia malengo yao.

Alisema wamejiandaa vizuri na kikosi chake kipo tayari kwa ajili ya mchezo huo na anaamini utakuwa wa ushindani mkubwa uliopo kati ya timu hizo, lakini kila moja ikihitaji kupata matokeo mazuri.

"Tumejiandaa vizuri, mchezo utakuwa wa ushindani mkubwa kwa sababu tunataka kutetea ubingwa wetu, maandalizi tunayofanya ni tofauti na michezo ambayo imepita.

"Hii ni mechi kubwa sana, tutaingia na mbinu tofauti, tunawaheshimu wapinzani wetu wana timu nzuri na tuko imara kwa ajili ya kutafuta pointi tatu katika mchezo huu," alisema Lukulu.

Alisema wamefanyia kazi madhaifu ya kikosi chao na wataingia katika mchezo huo kwa tahadhari kubwa dhidi ya wapinzani wao kwa sababu wana wachezaji wazuri na kikosi imara.

Mbali na mechi hiyo ya kesho, ligi hiyo ya wanawake itaendelea leo katika viwanja mbalimbali nchini kwa ajili ya kusaka bingwa atakayekwenda kucheza Kombe la CECAFA wanawake ili kupata mshindi wa kwanza atakayewakilisha ukanda huo kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika.

Vinara wa ligi hiyo, Fountain Gate Princess leo watakuwa nyumbani, Uwanja wa Jamhuri Dodoma wakiikaribisha Mkwawa Queens kutoka Iringa.

Timu inayokamata nafasi ya pili, Baobab Queens leo itakuwa ugenini kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Dar es Salaam, kucheza na inayoshika nafasi ya tatu ya msimamo, Maafande wa JKT Queens, zote zina pointi nne.

Alliance Girls ambayo ipo nafasi ya nne, imesafiri hadi Karatu, Arusha kwenye Uwanja wa Black Rhino, ikiwa mgeni wa The Tigers Queens.

Wanaoshika mkia kwenye ligi hiyo mpaka sasa, Ceasiaa Queens wakiwa kwenye nafasi ya 10 bila pointi yoyote,

# Simba, Kagera Sugar vitani mechi ya kisasi

INATOKA UK. 32

Mexime amesema wana mechi ngumu mbili ambazo zinamuumiza kichwa, nazo ni ya leo dhidi ya Simba na inayofuata dhidi ya Geita Gold.

"Nina mechi ngumu mbili, hii na itakayofuata dhidi ya Geita Gold, inabidi mwalimu uumize kichwa, ninavyojua mechi itakuwa ngumu japo tunacheza Kaitaba, unajua hizi timu mbili za Simba na Yanga hazina nyumbani wala ugenini, mechi zote ni kama wapo nyumbani tu na hazina jinsi ya kuzielezea, zinajulikana uwezo wao, tena ngoja niijumlishe na Azam, zina wachezaji ambao wanatembea na matokeo.

"Mfano kwenye mechi dhidi ya Azam, walipata nafasi mbili tu zote walizitumia, sasa tulipata zaidi ya tano hatukuzitumia, tungekuwa na watu ambao kama wanao wenzetu wenye viwango kama vyao, wale wa kumaliza mechi tungetoka na ushindi, hivyo ni lazima uwe makini ukicheza na hizi timu," alisema Mexime wakati huu timu yake hiyo ikishika nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu baada ya kujikusanyia alama 22 katika michezo 16.

HAUPENYI...



Mchezaji wa timu ya Ruvu Shooting, Juma Ugando (kulia), akizuia mpira dhidi ya mchezaji wa Mtibwa Sugar, katika mchezo wa Ligi Kuu Bara uliopigwa Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam jana na kumalizika kwa timu hizo kutoka suluhu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# TPBRC na vikwazo ngumi za kulipwa

**Na Halfani Chusi**

RAIS wa Kamisheni ya Ngumi za Kulipwa Tanzania (TPBRC), Chaurembo Parasa, amesema tasnia hiyo inakabiliwa na upungufu wa wadhamini hali inayochangia kudidimiza ukuaji wake.

Kiongozi huyo aliyasema hayo Dar es Salaam jana, katika mahojiano maalum na Nipashe, lililotaka kujua changamoto zinazoukwamisha mchezo huo kuweza kupiga hatua zaidi hapa nchini.

Parasa alibainisha kuwa wadhamini walioko hawakidhi mahitaji kutokana na ongezeko la mabondia walioibukia kuupenda mchezo huo.

"Mabondia ni wengi sana, vijana wengi wamejiingiza katika mchezo huu wakiamini ni ajira, shida wadhamini ni wachache, sisi waratibu wa mchezo huu tunauwezo wa kuandaa pambano kila wiki," alisema na kuongeza;

"Kuna uhaba wa miundombinu wezeshi katika mchezo wa ngumi, hivyo serikali inapaswa kuchukua hatua za makusudi kukabiliana na kadhia hiyo.

"Tunaiomba serikali na wadau wa michezo kuyafanyia kazi mapungufu hayo ili tasnia hii iweze kufika mbali na kusaidia mabondia walioko nchini kutimiza ndoto zao," alisema.

Pia, aliwataka mabondia wote walioko nchini kuishi vizuri na jamii ikiwamo kujiepusha na ugomvi pamoja na kutofanya mambo ambayo hayastahili kwenye jamii.

Alisema mabondia wanapaswa kutambua kwamba wao ni kioo cha jamii, hivyo si vizuri kufanya vitu ambavyo havitailetea tasnia hiyo heshima na kwamba wakibaini hatua kali zitachukuliwa dhidi yao.

# Azam haipoi

INATOKA UK. 32

usajili huu utakuwa mkubwa sana, kocha amepanga kusajili wachezaji wawili ama watatu kwa ukubwa ambao watu hawatotegemea.

"Tayari mwalimu Kali Ongalla amewasilisha ripoti yake siku nne zilizopita na tayari ipo kwenye kamati husika inayoshughulika na masuala ya usajili, wanajaribu kuchanganua kama ni ya kutekeleza moja kwa moja ama kwa asilimia chache, tunasubiria kuona kamati itaamua nini baada ya kuipokea.

"Fei Toto, Dickson Job ni wachezaji wazuri ambao Azam tumekuwa tukihusishwa nao ama wamekuwa wakitajwa na timu nyingine, wote ni wazuri ambao kila timu ya Ligi Kuu itahitaji kuwa nao.

"Kwa Tanzania Fei Toto ni mchezaji mzuri sana, kwenye viungo washambuliaji wazuri ni miongoni mwao, hivyo tunasubiria ripoti ya kamati ya usajili kuona itaamua nini kama ni yeye ama ni mchezaji mwingine tusubiri tuone kwa kuwa ni wachezaji wenye mikataba na timu nyingine na tunaheshimu mikataba yao.

"Januari hii timu zinataka kujivika makoti ya usajili mzuri na kuwa kileleni kwa wakati mmoja, ila nasisitiza ninavyojua mimi Azam inataka kufanya usajili wa kushangaza watu," alisema Ibwe.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MESSI MKATABA MPYA

KLABU ya Paris St-Germain itafungua mazungumzo na mshambuliaji wa Argentina, Lionel Messi, mwenye umri wa miaka 35, baada ya ushindi wake wa Kombe la Dunia, mkataba wake wa sasa unakamilika msimu ujao wa majira ya joto. ***(RMC)***

### GARDON ATAKIWA EVERTON

KLABU ya Everton inakaribia kufikia mkataba mpya na winga wa England, Anthony Gordon mwenye umri wa miaka 21, ili kuzuia nia ya Chelsea kumnunua. ***(Telegraph)***

### MARTINEZ ATAKIWA BAYERN

KLABU ya Bayern Munich ina nia ya kumsajili golikipa wa Argentina na Aston Villa, Emilano Martinez, mwenye umri wa miaka 30. ***(MediaFoot)***

### SOMMER NAYE ATAKIWA

GOLIKIPA wa Borussia Monchengladbach na Uswisi, Yann Sommer mwenye umri wa miaka 34, yuko kwenye mazungumzo na Bayern Munich kuhusu uhamisho baada ya Mjerumani Manuel Neuer kuvunjika mguu. ***(Goal)***

### MBAPPE KUONDOKA PSG

MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa Ufaransa, Kylian Mbappe, mwenye umri wa miaka 24, anaweza kutangaza kwamba ataondoka PSG mwishoni mwa msimu huu, huku Real Madrid wakimtaka. ***(Sport)***

### ANCELOTTI HAITAKI BRAZIL

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, amejitenga na tetesi zinazomhusisha na kazi ya Brazil, akisisitiza kwamba anataka kusalia na mabingwa hao wa Ulaya. ***(Rai Radio 1 via Mail)***

### JURANOVIC AWINDWA BARCA

KLABU ya Barcelona inatamani kumsajili beki wa pembeni wa Celtic na Croatia, Josip Juranovic, mwenye umri wa miaka 27, lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka kwa Klabu ya Atletico Madrid na za Premier League. ***(Sky Sports)***

### SAKA MKATABA MPYA

KLABU ya Arsenal inatarajiwa kuanza mazungumzo na mshambuliaji wa England, Bukayo Saka, mwenye umri wa miaka 21, kuhusu mkataba mpya katika "wiki na miezi ijayo". ***(Caught Offside)***

### NAPOLI YATOA MSIMAMO

MKURUGENZI wa Napoli, Cristiano Giuntoli, amepuuza nafasi ya Newcastle United ya kumsajili mshambuliaji wa Georgia, Khvicha Kvaratskhelia mwenye umri wa miaka 21. ***(Sport Express, via Fabrizio Romano)***

### PICKFORD AFIKIRIWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inamfikiria golikipa wa England na Everton, Jordan Pickford, mwenye umri wa miaka 28 kama mbadala wa muda mrefu wa Mfaransa Hugo Lloris mwenye miaka 35. ***(Football Insider)***

### CUNHA AWANIWA

KLABU za Arsenal na Leeds United zimejiunga na mbio za kumsajili mshambuliaji wa Brazil, Matheus Cunha mwenye umri wa miaka 23, huku Atletico Madrid wakijiandaa kumuuza. ***(Goal)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# SABABU BRAZIL KUIPIKU ARGENTINA VIWANGO FIFA

●●● Mafanikio ya mikwaju ya penalti yana thamani ya pointi chache sana kuliko ushindi wa...

**NYON, Uswisi**

LICHA ya Argentina kushinda Kombe la Dunia kwa mara ya kwanza tangu mwaka 1986, haijachukua nafasi ya juu ya viwango vya Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), kwani Brazil ndio kinara.

Brazil ambao ni wapinzani wakuu wa Argentina barani Amerika Kusini, imeshika nafasi ya kwanza tangu Februari mwaka huu walipoiondoa Ubelgiji katika nafasi hiyo.

Lakini ingawa 'Selecao' walishindwa kutinga robo fainali, matokeo ya Argentina hayajatosha kuwapita.

Brazil ilishinda mechi tatu kwenye Kombe la Dunia, ikafungwa na Cameroon na kupokea kichapo cha mikwaju ya penalti mikononi mwa Croatia.

Argentina ilishinda michezo minne, ikapoteza mmoja kwa Saudi Arabia na wakashinda mara mbili kwa mikwaju ya penalti ikiwa ni pamoja na fainali ya Jumapili walipoifunga Ufaransa kwa mikwaju ya penalti 4-2.

Argentina walishinda Copa America 2021 na sasa ni mabingwa wa dunia, lakini haijatosha kushika nafasi ya kwanza.

Mafanikio ya mikwaju ya penalti yana thamani ya pointi chache sana kuliko ushindi wa muda wa kawaida.

Iwapo Argentina au Ufaransa wangeshinda fainali ndani ya dakika 120 wangeingia namba moja, lakini mikwaju ya penalti ilihakikisha kwamba Brazil isingeweza kupitwa.

Argentina na Ufaransa zote zimepanda kwa nafasi moja hadi ya pili na ya tatu, huku Ubelgiji ikishuka kwa nafasi mbili hadi nne baada ya kushindwa kuvuka hatua ya makundi.

England imebakia katika nafasi ya tano, huku wenzao waliofuzu robo fainali Uholanzi wakipanda kwa nafasi mbili hadi ya sita.

Croatia iliyomaliza katika nafasi ya tatu kwenye Kombe la Dunia wapo nafasi ya tano kutoka ya 12.

Italia, ambayo ilishindwa kufuzu Qatar, imeshuka nafasi mbili hadi ya nane.

Ureno haijabadilika katika nafasi ya tisa, huku Hispania ikishuka kwa nafasi tatu hadi 10.

Morocco na wamepanda kwani wapo nafasi ya 11.

## HABARI MICHEZO


SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,059,8

JACKPOT MECHI WIKI HII

TAREHE: 21,22 NA 23 DISEMBA 2022

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 21/12/22 | 22:00 | MSK Deinze vs Zulte Waregem | 2.67 | 3.41 | 2.39 |
| 02. 21/12/22 | 23:00 | UD Logrones vs Albacete Balompie | 2.93 | 3.23 | 2.36 |
| 03. 22/12/22 | 17:00 | Jamshedpur vs FC Goa | 2.52 | 3.25 | 2.52 |
| 04. 22/12/22 | 18:00 | OFI Crete vs Atromitos | 2.47 | 3.35 | 2.75 |
| 05. 22/12/22 | 20:00 | Aris Limassol vs Apoel Nicosia | 2.81 | 3.21 | 2.49 |
| 06. 22/12/22 | 20:00 | Omonia Nicosia vs Apollon Limassol | 2.42 | 3.15 | 2.95 |
| 07. 22/12/22 | 21:00 | CD Linares vs Racing Santander | 2.98 | 3.23 | 2.33 |
| 08. 22/12/22 | 21:00 | CD Eldense vs Burgos | 2.63 | 3.18 | 2.63 |
| 09. 22/12/22 | 23:00 | Gimnastic Tarragona vs Malaga | 3.09 | 3.18 | 2.29 |
| 10. 22/12/22 | 23:00 | Real Oviedo vs Granada | 2.83 | 2.98 | 2.59 |
| 11. 22/12/22 | 23:15 | Moreirense vs FC Arouca | 2.41 | 3.15 | 2.71 |
| 12. 23/12/22 | 11:45 | Brisbane Roar vs Western Sydney | 2.35 | 3.32 | 2.87 |
| 13. 23/12/22 | 14:30 | Perth Glory vs Wellington Phoenix | 2.78 | 3.38 | 2.38 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa


# BENZEMA ATANGAZA KUTUNDIKA DALUGA




**PARIS, Ufaransa**

KARIM Benzema ametangaza kustaafu soka la kimataifa, siku moja baada ya Ufaransa kufungwa na Argentina katika fainali ya Kombe la Dunia 2022.

Benzema alikosa michuano hiyo nchini Qatar kutokana na jeraha la paja na hakuweza kuichezea Ufaransa.

Alicheza mechi 97 na anashika nafasi ya tano kwenye orodha ya wafungaji mabao wa muda wote wa Ufaransa akiwa na mabao 37.

"Nilifanya juhudi na makosa niliyochukua ili kuwa hapa nilipo na ninajivunia hilo," alisema Benzema.

Benzema alituma ujumbe huo katika mitandao yake ya kijamii. "Nimeandika historia yangu na yetu inatosha."

Mshambuliaji huyo wa Real Madrid na Ufaransa alishinda tuzo ya Ballon d'Or mwaka huu kwa mara ya kwanza.

Benzema alifunga mabao 44 katika michezo 46 alipoisaidia Real kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya na Ligi Kuu Hispania, LaLiga msimu wa 2021-22.

# Ancelotti atakiwa kuinoa Brazil

**RIO DE JANEIRO, Brazil**

BRAZIL bado inakaribia kuafikiana na kutolewa kwao Kombe la Dunia katika robo-fainali na Croatia, wakijua lazima watafute kocha mpya wa kuwapeleka mbele.

Inaonekana kuna nia zaidi ndani ya Brazil ya kuteua kocha wa kigeni kwa mara ya kwanza kabisa, baada ya Tite kuondoka.

Jina la Pep Guardiola limetajwa, ingawa inaonekana kuwa ngumu sana kuiacha Manchester City.

Kocha wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, pia amekuwa gumzo sana nchini Brazil.

Inaonekana wangekuwa tayari kumpa Ancelotti ofa ikiwa angekuwa na nia yoyote katika nafasi hiyo.

Hata hivyo, alipoulizwa kwenye kituo cha redio cha Italia Radio1, Ancelotti alijibu kwamba ana furaha katika mji mkuu wa Hispania, Madrid.



"Kufundisha Brazil? Sijui nini kitatokea katika siku zijazo, ninaishi wakati huu. Mimi ni mkubwa na ninajisikia vizuri Madrid, bado tuna malengo mengi ya kufikia," alisema Ancelotti.

"Kuna wakati wa kufikiria juu ya siku zijazo. Nina mkataba unaoisha 2024 na ikiwa Real Madrid hawataniondoa, sitahama."

Ancelotti aliacha mlango wazi endapo atapenda kubadili mwelekeo katika siku zijazo, lakini anaonekana kutaka kuona mkataba unaendelea pale Madrid.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 63 hapo awali alisema kuwa hii itakuwa kazi yake ya mwisho na anakusudia kustaafu baada ya kuondoka Real Madrid.

HABARI MICHEZO


344,733/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 26/12/22 | 18:00 | Everton FC vs Wolverhampton Wanderers | 2.31 | 3.25 | 3.05 |
| 02. 26/12/22 | 18:00 | Bristol City vs West Bromwich Albion | 2.90 | 3.25 | 2.40 |
| 03. 26/12/22 | 18:00 | Rotherham United vs Stoke City | 2.90 | 3.25 | 2.40 |
| 04. 26/12/22 | 18:00 | Burton Albion vs Lincoln City | 2.37 | 3.30 | 2.90 |
| 05. 26/12/22 | 18:00 | Cambridge United vs Shrewsbury Town | 2.60 | 3.25 | 2.65 |
| 06. 26/12/22 | 18:00 | Charlton Athletic vs Peterborough United | 2.70 | 3.30 | 2.55 |
| 07. 26/12/22 | 18:00 | Exeter City vs Portsmouth FC | 2.65 | 3.35 | 2.55 |
| 08. 26/12/22 | 19:00 | FC Annecy vs AS Saint-Etienne | 2.90 | 3.25 | 2.37 |
| 09. 26/12/22 | 20:00 | Goztepe Izmir vs BB Bodrumspor | 2.50 | 3.35 | 2.65 |
| 10. 26/12/22 | 20:15 | Cardiff City vs Queens Park Rangers | 2.48 | 3.20 | 2.80 |
| 11. 26/12/22 | 22:45 | Royal Charleroi SC vs RSC Anderlecht | 2.80 | 3.45 | 2.38 |
| 12. 26/12/22 | 22:45 | Luton Town vs Norwich City | 2.75 | 3.30 | 2.50 |
| 13. 26/12/22 | 23:00 | Valenciennes FC vs Amiens SC | 2.46 | 3.20 | 2.85 |
| 14. 26/12/22 | 23:00 | Pau FC vs Paris FC | 2.95 | 3.20 | 2.38 |
| 15. 26/12/22 | 23:00 | Quevilly-Rouen Metropole vs Grenoble Foot | 2.46 | 3.05 | 2.95 |
| 16. 26/12/22 | 23:00 | SC Bastia vs SM Caen | 3.05 | 3.10 | 2.38 |
| 17. 26/12/22 | 23:00 | Nimes Olympique vs EA Guingamp | 2.90 | 3.25 | 2.40 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 21/12/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1538 | Myanmar vs Malaysia | 11.60 | 5.80 | 1.19 |
| 13:00 | 2988 | FC Talanta vs Ulinzi Stars | 2.80 | 2.85 | 2.75 |
| 13:00 | 3049 | Giresunspor vs Bursa Niluferspor | 1.37 | 4.64 | 6.38 |
| 14:00 | 1552 | Persib Bandung vs Persita Tangerang | 1.59 | 3.79 | 4.86 |
| 14:00 | 1844 | Tanzania Prisons vs Dodoma FC | 2.41 | 2.80 | 3.35 |
| 14:00 | 2767 | Gor Mahia vs Bandari | 2.43 | 2.80 | 3.30 |
| 14:00 | 4230 | Neroca FC vs Sreenidi Deccan FC | 3.65 | 3.45 | 1.87 |
| 15:00 | 3046 | Posta Rangers vs Vihiga Bullets FC | 1.74 | 3.27 | 4.59 |
| 15:00 | 5362 | Wazito vs Bidco United | 2.47 | 2.76 | 3.00 |
| 15:00 | 5585 | Nairobi City Stars FC vs Kariobangi Sharks | 2.60 | 2.95 | 2.90 |
| 15:00 | 5667 | Fatih Karagumruk vs Utas Usakspor A.s | 1.25 | 5.47 | 8.59 |
| 15:15 | 2629 | Sofapaka vs Kenya Police | 2.62 | 2.76 | 2.81 |
| 16:00 | 2034 | Espoir FC vs Gorilla FC | 2.81 | 2.71 | 2.66 |
| 16:00 | 2826 | AS Kigali vs Sunrise | 1.46 | 3.88 | 6.41 |
| 16:00 | 3429 | Rutsiro FC vs Bugesera FC | 2.65 | 2.75 | 3.05 |
| 16:00 | 3833 | Adama City FC vs Dire Dawa Kenema FC | 1.85 | 2.97 | 4.48 |
| 16:00 | 4066 | Geita Gold FC vs Azam | 2.46 | 2.34 | 1.94 |
| 16:00 | 4595 | Rwamagana City FC vs Mukura | 5.46 | 3.02 | 1.71 |
| 16:00 | 5766 | Musanze vs Police FC Rwanda | 2.53 | 2.77 | 2.91 |
| 16:30 | 1036 | Masitaoka FC vs Gaborone United | 5.80 | 3.60 | 1.61 |
| 16:30 | 3862 | Minerva FC vs Gokulam Kerala FC | 2.08 | 3.16 | 3.30 |
| 17:00 | 3882 | Alanyaspor vs Eyupspor | 1.91 | 3.60 | 3.36 |
| 17:30 | 3240 | Al Shabbab vs Sitra Club | 2.01 | 3.16 | 3.50 |
| 18:00 | 1437 | Asteras Tripolis vs Volos | 2.12 | 3.34 | 3.29 |
| 18:00 | 1636 | Al Masry Club vs Arab Contractors | 2.16 | 2.89 | 3.74 |
| 18:00 | 2192 | AEK Athens vs Lamia | 1.15 | 7.15 | 14.90 |
| 18:25 | 1589 | Al Ahli Jeddah vs Hajer Club | 1.61 | 3.41 | 5.45 |
| 18:30 | 5683 | Bahrain Club vs Al Ahli Manama | 2.96 | 2.86 | 2.42 |
| 19:00 | 1583 | Welayta Dicha FC vs Hawassa Kenema SC | 2.63 | 2.73 | 2.83 |
| 19:00 | 3896 | Kagera Sugar vs Simba | 5.72 | 2.74 | 1.30 |
| 19:00 | 5799 | Trabzonspor vs Samsunspor | 1.54 | 4.09 | 4.87 |
| 20:00 | 1640 | Doxa Katokopia vs EN Paralimni | 2.15 | 3.30 | 3.30 |
| 20:00 | 2021 | Nea Salamis vs AEK Larnaca | 4.40 | 3.55 | 1.78 |
| 21:00 | 1472 | CD Ibiza Islas Pitiusas vs Eibar | 4.69 | 3.59 | 1.72 |
| 21:00 | 2341 | PAS Giannina vs Olympiakos | 7.98 | 4.29 | 1.40 |
| 21:00 | 2569 | Atletico Saguntino vs Rayo Vallecano | 12.00 | 5.60 | 1.23 |
| 21:00 | 2599 | Merida UD vs Alaves | 3.33 | 3.23 | 2.15 |
| 21:00 | 3359 | Besiktas vs Sanliurfaspor | 1.08 | 8.36 | 18.48 |
| 21:00 | 3848 | Levante vs FC Andorra | 1.86 | 3.42 | 4.06 |
| 21:00 | 4736 | Numancia vs Sporting Gijon | 3.54 | 3.04 | 2.15 |
| 22:30 | 2915 | Ionikos Nikea FC vs Panathinaikos | 7.37 | 3.83 | 1.47 |
| 22:45 | 1166 | Charlton vs Brighton | 7.96 | 5.17 | 1.32 |
| 22:45 | 1508 | Celtic vs Livingston | 1.10 | 8.54 | 19.85 |
| 22:45 | 2328 | Blackburn vs Nottingham | 3.09 | 3.28 | 2.24 |
| 22:45 | 3314 | Coventry vs West Bromwich | 2.93 | 3.12 | 2.39 |
| 23:00 | 1085 | CD Arnedo vs Osasuna | 15.94 | 6.18 | 1.18 |
| 23:00 | 2639 | Pontevedra vs Tenerife | 3.29 | 3.24 | 2.16 |
| 23:00 | 3116 | Manchester Utd vs Burnley | 1.46 | 4.38 | 6.16 |
| 23:00 | 5037 | CD Coria vs Real Sociedad | 14.87 | 6.54 | 1.17 |
| 23:15 | 4415 | Porto vs Gil Vicente | 1.18 | 6.04 | 11.68 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# MAYAY AITAKA BAMMATA KUANZA 'KUPIKA' MEDALI

**Na Romana Mallya**

KAIMU Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Michezo nchini, Ally Mayay Tembele, amelitaka Baraza la Michezo ya Kijeshi Tanzania (BAMMATA), kuhakikisha wanakuwa na mipango ya muda mrefu ambayo pia itawezesha kupatikana kwa medali za kimataifa kupitia michezo.

Pia, ametaka waangalie namna watakavyoshiriki katika vyama na mashirikisho ya michezo kama ilivyojadiliwa miaka saba iliyopita.

Tembele aliyasema hayo Dar es Salaam jana wakati akifungua kikao cha utendaji cha BAMMATA ambacho ni cha mwisho cha kuamua tarehe na wapi kutafanyika mashindano ya michezo ya majeshi.

Mashindano hayo yanatarajiwa kufanyika mapema mwakani na kwa sasa wachezaji wapo kambini na yatashirikisha pia shughuli za utamaduni.

Akizungumza katika kikao hicho, kiongozi huyo amelitaka baraza hilo kutafsiri kwa vitendo Sera ya Maendeleo ya Michezo ambayo ndani yake yapo malengo sita likiwamo kuhamasisha Watanzania kushiriki katika michezo na mazoezi ya viungo.

Malengo mengine aliyataja ni upatikanaji wa viwanja na zana bora na za kutosha, kuandaa na kutayarisha wataalamu wa kutosha katika fani na taaluma mbalimbali za michezo na kuhakikisha timu na wachezaji wanafanya vizuri mashindano ya michezo ya kimataifa.

Pia kufanya utafiti katika michezo ya jadi kwa lengo la kuifufua na kuiendeleza pamoja na kujenga ushirikiano na mataifa mengine kwa kutumia tasnia hiyo.

Tembele alilikumbusha baraza hilo kuwa utunzaji wa kumbukumbu ni jambo muhimu unaosaidia kuendelea huku akitokea mfano mchezaji, Lionel Messi aliyeiongoza timu ya Argentina kupata ushindi, watu wana kumbukumbu za dakika alizocheza.

Mwenyekiti wa BAMMATA, Brigedia Jenerali Suleiman Gwaya, aliahidi kuyafanyia kazi maelekezo waliyopewa kwa lengo la kuiboresha zaidi sekta hiyo.

Brigedia Jenerali Gwaya alisema, "moja ya malengo ya kikao hiki ni michezo kufanya vizuri kimataifa, kamati hii inapanga mipango ya kuendeleza michezo kwenye vyombo vya ulinzi na usalama, tunapanga mipango ya namna ya kuendeleza wachezaji, kupata mafunzo mbalimbali kwa ajili ya walimu na waamuzi."




Mkuu wa Kitengo cha Usimamizi wa Thamani kwa Wateja wa MultiChoice Tanzania, Hilda Nakajumo, akihutubia hadhara Dar es Salaam jana, kuhusu ofa maalum ya kuboresha sikukuu ambayo wateja wa DStv watapata katika kipindi hiki cha sikukuu. **MPIGAPICHA WETU**

# DSTV YAJA NA OFA MSIMU WA SIKUKUU

**Na Mwandishi Wetu**

KAMA ambavyo imekuwa ikifanya misimu yote ya sikukuu, msimu huu wateja wote wa DStv wanapata tena mserereko ambapo kuanzia juzi, Desemba 19 hadi Januari 24, mwakani, ofa kabambe zimeanza kutolewa kwa kila mteja anayelipia kifurushi chake kupandishwa na kuunganishiwa kifurushi cha juu yake kwa mwezi mzima bila malipo ya ziada.

Akitangaza kuzinduliwa kwa kampeni hiyo ya msimu wa sikukuu, Mkuu wa Kitengo cha Thamani kwa Wateja wa MultiChoice Tanzania, Hilda Nakajumo, alisema ofa hii ni kwa wateja wote wa DStv watakaolipia vifurushi vyao katika kipindi hicho ambapo watatunukiwa kifurushi cha juu yake bila malipo ya ziada.

Alisema hata kama mteja kifurushi chake kilimalizika na alikuwa hajalipia, atapata ofa hiyo punde tu atakapohuisha kifurushi chake cha awali.

"Msimu huu wa sikukuu tunaileta familia ndugu na jamaa pamoja na ili kuhakikisha kuwa hawapungukiwi na burudani, tumeamua kuwazawadia ofa hii kabambe ili kuwawezesha kupata burudani ya hali ya juu kwa kufurahia chaneli nyingi zaidi za DStv zikiwamo katuni kwa ajili ya watoto, michezo, tamthilia, habari na makala mbalimbali," alisema Hilda.

Hilda amesisitiza kuwa wateja wa Compact Plus ambao watapandishwa mpaka kwenye kifurushi cha Premium wataweza kufurahia sikukuu hii pamoja na wapenzi wao huku wakiangalia vipindi pendwa zaidi ndani ya DStv.

Alisema kuna msimu mpya wa tamthilia pendwa ya 'The Good Doctor' kuanzia Desemba 5, mwaka huu ndani ya M-Net pamoja na filamu maarufu kila Jumapili kama 'The King's Man, The Bad Boys' pamoja na 'Moonfall'.

"Mteja anayelipia kifurushi cha Compact atapandishwa mpaka kwenye kifurushi cha Compact Plus ambapo ataweza kufurahia vipindi kama Real Housewives of Salt Lake City ndani ya 1Magic kuanzia Desemba 26 na pia atajionea msimu mpya wa 'The History of Christianity' ndani ya chaneli ya Curiosity kuanzia tarehe Desemba 25, mwaka huu," alisema.

Michezo
Jumatano Desemba 21
Nipashe



UKURASA 30

## Benzema atangaza kutundika daluga


Messi

# GOAT

## MCHEZAJI BORA WA WAKATI WOTE

### MATAJI

- La Liga x 10
- Supercopa x 8
- Ballon d'Or x 7
- Copa Del Rey x 7
- Champions League x 4
- Super Cup x 3
- Club World Cup x 3
- Golden Ball Awards x 2
- Ligue 1 x 1
- Copa America x 1
- World Cup x 1

### VIWANGO FIFA

1. Brazil
2. Argentina
3. Ufaransa
4. Ubelgiji
5. England
6. Uholanzi
7. Croatia
8. Italia
9. Ureno
10. Hispania

FIFA
For the Good of the Game

### SABABU BRAZIL KUIPIKU ARGENTINA VIWANGO...

"Mafanikio ya mikwaju ya penalti yana thamani ya pointi chache sana kuliko ushindi wa muda wa kawaida, hivyo..."

HABARI KAMILI UK. 29

# SIMBA, KAGERA SUGAR VITANI MECHI YA KISASI

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Simba leo kinatarajia kuwa na dakika 90 ngumu kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera, ambao mara kwa mara wamekuwa hawana bahati nao, itakapokabiliana na Kagera Sugar ikiwa ni mechi ya raundi ya 17 ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mara ya mwisho Simba kucheza kwenye uwanja huo, Januari 26, mwaka huu, dhidi ya timu hiyo, ikiwa ni mechi ya Ligi Kuu msimu uliopita, ilichapwa bao 1-0 lililowekwa wavuni na Mganda aliyewahi kuichezea timu hiyo, Hamisi Kiiza dakika ya 71 akitokea benchini.

Simba inataka kuuzima mzimu huo, pamoja na kutokuwa na matokeo mazuri mara kwa mara ikicheza kwenye uwanja huo dhidi ya Kagera Sugar.

Timu hiyo imekuwa ikipata matokeo mazuri dhidi ya Kagera Sugar mara nyingi ikicheza Dar es Salaam, ambapo msimu huu kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza ilishinda mabao 2-0 yaliyofungwa na Mserbia Dejan Georgijevic na Moses Phiri, Agosti 20, mwaka huu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Wakati Dejan akiwa hayupo, timu zote mbili zitakuwa na wafungaji wao, Phiri kwa upande wa Simba na Kiiza kwa upande wa Kagera Sugar.

Hata hivyo, timu hizo hazitokuwa na makocha wao waliokuwapo mara ya mwisho timu hizo zikicheza Kaitaba, Pablo Franco Martin kwa upande wa Simba na Kagera Sugar ilikuwa ikifundishwa na Francis Baraza ambao wote wameshatimuliwa na klabu zao.

Kaimu Kocha Mkuu wa timu hiyo, Juma Mgunda, alikiri mchezo huo utakuwa mgumu kutokana na uwezo wa Kagera Sugar kwa sasa pamoja na mwalimu wake Mecky Mexime, hivyo wamejiandaa vema na tahadhari zote zimechukuliwa.

"Tuko tayari kushindana na Kagera Sugar, mchezo utakuwa mgumu, tunawaheshimu wapinzani wetu ni moja kati ya timu nzuri, tunajua hilo na ndiyo maana tahadhari zote zimechukuliwa," alisema Mgunda.

Alisema matokeo ya msimu uliopita hayawezi kuwafanya wahofie chochote kwani wamejiandaa kushinda kwenye mechi hiyo.

"Moja ya kanuni ya 'fair play' ni kuheshimu mpinzani wako, tunawaheshimu, lakini haina maana kuwa sisi tunakwenda kinyonge, tunakwenda kushinda mechi hiyo, ingawa najua Mexime ni mdogo wangu na nimesoma naye kwenye kozi ya ukocha," alisema Mgunda.

Simba inahitaji ushindi huo kwa udi na uvumba ili kuweka hai matumaini ya kuweza kutwaa ubingwa msimu huu wakati huu ikiwa na pointi 37, huku ikikabiliwa na vita kali baina ya watani wao wa jadi, Yanga ambayo jana ilicheza dhidi ya Coastal Union na Azam FC itakayoshuka dimbani ugenini leo dhidi ya Geita Gold.

Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky

INAENDELEA UK. 28

## Azam haipoi kwa Fei Toto

**Na Hadija Mngwai**

AZAM FC imepanga kufanya usajili wa kishindo katika dirisha hili dogo kwa kusajili nyota wenye uwezo huku kiungo wa Yanga, Feisal Salum ' Fei Toto' akipaniwa vilivyo kusainishwa klabuni hapo.

Dirisha dogo la usajili kwa timu za Ligi Kuu Bara, Championship na First League, limefunguliwa tangu Desemba 16, mwaka huu huku likitarajiwa kufungwa Januari 15, mwakani.

Akizungumza na Nipashe jana, Kaimu Ofisa Habari wa Azam FC, Hashimu Ibwe, alisema wamepanga kufanya usajili wa kishindo katika dirisha hili dogo ambao utawashangaza watu wote na kudai kuhusu Fei Toto wanasubiria kamati kuona itaamua nini.

"Mshindo wa Azam katika

INAENDELEA UK. 28

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >